

**USHAWISHI WA KIASI CHA HABARI KINACHOPITISHWA KATIKA TAFSIRI:  
KIFANI CHA ‘MBINU ZA UTUNZAJI WA MITI KATIKA MISITU YA JAMII’ TAFSIRI  
YA ‘SOCIAL FORESTRY TECHNIQUES’**

**NA**

**ASIKO ANNE FLORENCE MUKOLWE  
C50/66790/2013**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA  
SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**NOVEMBA 2019**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili wa sanaa katika chuo kikuu kingine chochote.

**Sahihi.....**

**Tarehe .....**

**Asiko Anne Florence Mukolwe**

**(Mtahiniwa)**

Tasnifu hii limewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi na washauri walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Nairobi.

**Sahihi.....**

**Tarehe.....**

**Dr. Omboga Zaja**

**Idara ya Kiswahili**

**Chuo Kikuu cha Nairobi**

**Sahihi.....**

**Tarehe.....**

**Dr. S. M. Obuchi**

**Idara ya Kiswahili**

**Chuo Kikuu cha Moi**

## **TABARUKU**

Kazi hii namtabarukia marehemu mwanangu Fabian Mukolwe. Ulituacha wakati kazi yangu ya uzamili ilipopamba moto, sitawahi kusahau mchango wako katika kazi yenyewe na maisha yetu.

## SHUKRANI

Shukrani zangu natoa kwa wahusika mbalimbali ambao kama hawangekuwa kazi hii haingefikia kilele hiki. Ninaanza kwa kumshukuru Maulana ambaye neema zake zinatoshia. Alinibariki kwa fikira, fedha, wakati na kuniweka karibu na waja waliotia juhudi zao kunisaidia kukamilisha kazi hii.

Shukrani za pili nawapa Dkt. Omboga Zaja na Dkt. Samuel Obuchi ambao walichukua muda wao kusoma kazi yangu na kunielekeza kila mara bila kuchoka. Mwanzoni pia nilifanya kazi na Dkt. Ayub Mukhwana ambaye wasia wake hauwezi ukasahaulika. Tajriba ya Dkt. Omboga Zaja na uzoefu wa Dkt. Obuchi umedhihirika katika kazi hii. Rabana awape neema zake ili muendeleo kutoa wasomi wengine zaidi.

Shukrani zangu nyingine ziwaendee wahadhiri wangu wote walionifunza kozi za uzamili kwa bidii, ukakamavu na ujuzi wa hali ya juu. Sitawahi kuwasahau; Prof. Iribe Mwangi kwa mawaidha yake ya kila mara, Prof. John Habwe kwa maoni yake yenye manufaa hapo mwanzoni mwa tasnifu hii. Wahadhiri wa Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Nairobi ambao pia wanastahili pongezi kwa mafunzo yao yenye hekima ni pamoja na Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Mwenda Mbatia, Dkt. Prisca Jerono, Dkt. Omboga Zaja, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Amiri Swaleh na Prof. Evans Mbuthia.

Wenzangu wa darasa la uzamili pia wana nafasi ya kipekee katika moyo wangu. Hawa ni pamoja na Lilian, Sylveria, Agnes, Asha, Adeline, Carolyne, Flora, Winfred, Jackline, Wangeci, Bi. Gitonga, Nyambeki, Kemunto, Emily, Bosibori, Njeri, Polycarp, Chesebe, Misheck, John Bosco, Kevin, Mengistu, Saar, Jared, Mogusu, Mwangi na Roy. Kwa sababu ya ucheshi, uwazi na bidii zenye za mchwa, mlikuwa washirika wazuri sana, kozi ikaonekana nyepesi.

Shukrani hizi natoa kwa wataalam waliokuwa tayari kunijibu kila mara nilipokuwa na swali kuhusu istilahi za elimumisitu, Melvin Ouma kutoka Nakuru, Rosemary Gator Sabida kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii Huduma ya Misitu, Tanzania na Vuai Mkoko Hassan kutoka Wizara ya Kilimo na Maliasili, Idara ya Misitu na Rasilimali Zisizoejesheka, Zanzibar.

Ninawashukuru wazazi wangu, hasa marehemu babangu Mzee Antony Ogutu Asiko, ambaye kwa uthabiti wake alihakikisha amewekeza kwa elimu yangu. Bila bidii zake, utunzaji wa mamangu na

ushauri wa ami yangu Mzee Elijah Obare Asiko singekua hadi kiwango hiki. Siwezi nikamsahau bavyaa yangu Mzee Jacob Mukolwe kwani alithamini maendeleo yanayohusu masomo.

Nafasi hii naipa familia yangu, mume wangu mpendwa Michael na wanangu Marion, Stephen na marehemu Fabian, wanastahili shukrani za dhati kwa kuniruhusu nirudi masomoni, kuhudhuria mihadhara, kudurusu kwa muda mrefu na kutumia fedha kwa shughuli hizi. Ilibidi mjitolee mhanga ili kazi hii ifikie hatima yake. Mola awabariki.

Mwisho ni shukrani kwa walimu wenzangu; Bw. Hippolitus Omondi, mwalimu mkuu, kwa kunipa idhini ya kwenda katika Chuo Kikuu cha Nairobi mara kwa mara, Bw. Francis Malowa na Charles Otieno ambao walichangia kwa kupiga chapa na kutoa tasnifu hii. Ninawashukuru walimu wa Idara ya Lugha, hasa Kiswahili, Binti Carolyne Ochola na Esther Oduor, walioshikilia sehemu ya kazi niliyostahili kufanya nilipoondoka. Walimu wote wa Shule ya Upili ya Ndenga wanastahili shukrani kwa usaidizi wowote waliotoa. Kama nimemsahau mtu yeyote aniwie radhi, nina shukrani tele moyoni kwa kufikia mwisho wa utafiti huu.

## VIFUPISHO

<b>EM:</b>	Elimumisitu.
<b>HL</b>	Hadhira Lengwa.
<b>LC:</b>	Lugha Chanzi.
<b>LL:</b>	Lugha Lengwa.
<b>MC:</b>	Matini Chanzi.
<b>ML:</b>	Matini Lengwa.

## MAELEZO YA ISTILAHU

- Hewa mkaa:** hewa itolewayo baada ya kutumia oksijeni.
- Kilimomseto:** ni mfumo wa matumizi ya ardhi ambapo mimea, miti au mifugo hudhibitiwa kimaksudi katika eneo mahsusi kwa manufaa ya kijamii, kiuchumi na kimazingira kutokana na mahusiano baina ya vitu hivi vilivyomo.
- Mazingira:** yale yote yanayomzunguka binadamu; miti, mimea, maji, udongo, na wanyama, uzalishaji mfululizo wa mazao na huduma kutokana na miti.
- Mazingira endelevu:** ni mazingira ambamo miti na mimea imewakilishwa katika umri, na urefu mbalimbali, uzalishaji mfululizo wa mazao na huduma kutokana na miti. Pamoja na hayo ni mazingira ambayo hayana dalili za kubabaishwa na mmomonyoko wa udongo na ukame, na huwa na jamii anuwai ya wanyama.
- Tabianchi:** ni mabadiliko ya hali ya anga.
- Timbao:** Mali yoyote tu inayotokana na miti, kwa mfano; mbao.
- Uhifadhi wa mazingira:** Neno uhifadhi linatazamwa kama upangaji, ulimaji (uzalishaji), utunzaji na matumizi endelevu ya misitu mahususi, miti, vichaka na mimea katika maeneo ya kilimo na makaazi ya binadamu na wanyama wa pori.
- Viwango vya maisha:** inamaanisha uzima wa watu kwa jumla au viwango vya kuishi.
- Washika dau:** ni wanaonufaika na mazao, huduma na msaada kutoka kwa mazingira na maliasili, kama vile: wakulima, walimu, wanafunzi, wafanyi kazi wa umma na mashirika yasiyo ya serikali. Yeyote tu ahusikaye na mazingira.
- Washirika wa maendeleo:** Makundi au serikali zinazoungana na wahusika fulani ili kuleta maendeleo.
- Visumbufu:** wadudu na viumbe vyovyote viharibifu

## IKISIRI

Tafsiri bora ni zana inayoweza mawasiliano amilifu katika nyanja mbalimbali. Hata hivyo, pana visababishi vinavyoshawishi ubora na uamilifu huo wa tafsiri. Utafiti huu ulichunguza ushawishi wa kiasi cha habari zilizopitishwa katika tafsiri, kifani kikiwa kitabu *‘Mbinu za Utunzaji wa Miti katika Misitu ya Jamii’* ambacho ni tafsiri ya *‘Social Forestry Techniques’*. Utafiti wenyewe ulichochea na uhaba wa tafiti kuhusu kiasi cha habari zinazopitishwa katika tafsiri. Ni utambuzi wetu kuwa uelezaji wa hoja mpya, msamiati na istilahi ngeni za kimazingira, hasa uhimili wa tabianchi na uhifadhi wa misitu mara nyingi hufanywa kwa Kiingereza na hivyo tumetiwa ari ya kuchangia kuiboresha tafsiri. Tafsiri zinazohusu hoja hizi ni chache kama zipo, na zile tulizopitia zina upungufu mkubwa wa mchakato na ujumbe katika matini lengwa. Ukweli huu ukatuochochea kuchunguza vipengele vinne vya mchakato wa tafsiri; ubanaji, uzidishaji, upotezaji na upotoshaji wa habari zifikiazio matini lengwa na kupendekeza suluhisho linalohitajika upesi sio tu katika tafsiri bali pia katika uwanja wa masuala ya uhifadhi wa mazingira. Malengo ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza uwepo wa habari zilizobanwa katika matini lengwa kutoka katika matini chanzi, kuhakiki uwepo wa kiasi cha habari ambazo zimezidishwa katika matini lengwa ikilinganishwa na matini chanzi na kutathmini namna ambavyo kumetokea upotezaji na upotoshaji wa habari kutoka katika matini chanzi zikifikia matini lengwa. Nadharia iliyoongoza kazi hii ilikuwa ya *‘Skopos’* iliyoasisiwa na Vermeer ambayo inajulikana kama nadharia ya kitendo, na kitendo chenyewe kina kusudi ambapo alipendekeza tafsiri yenye kusudi fulani badala ya ulinganifu. Kutokana na uchanganuzi wa data zilizotokana na chapisho *‘Mbinu za Utunzaji Miti Katika Misitu ya Jamii’* tuligundua kuwa kusudi la tafsiri linaathiri vipengele vya mchakato wa tafsiri kama vile ubanaji, uzidishaji, upotezaji na upotoshaji. Vipengele hivi vinne vimeonekana kushawishi kiasi cha habari zinazopitishwa katika tafsiri kutoka katika matini ya lugha chanzi hadi lugha lengwa. Matokeo yetu pia yalionyesha kuwa upotezaji ulitokea kwa kiwango kidogo, upotoshaji kwa wastani na ubanaji na uzidishaji ndio ulitokea kwa kiwango kikubwa. Haya yanadhihirisha kuwa watafsiri walilenga kupitisha ujumbe kwa hivyo waliepuka vikwazo vilivyozuia mawasiliano kama istilahi zilizokosa visawe katika lugha lengwa, yaani Kiswahili. Uchunguzi wetu uligundua pia kuwa ingawa msamiati na istilahi za elimumisitu zilitumika kwa wingi katika matini chanzi, chache ndizo zilifika katika matini lengwa na hivyo kushawishi kiasi cha habari. Suala jingine lililoibuka ni kuwa nakala hiyo ilikuwa na msamiati ambao haukutafsiriwa na mwingine ambao hautafsiriki. Kuhitimisha, tumetoa pendekezo kwa vipengele vilivyochunguzwa kwa kutumia maelezo ya kutosha tu ujumbe unaohusu kinachokusudiwa kupitishwa, kujiepusha na maelezo ya ziada yanayolenga kando na kutafuta istilahi za elimumisitu ili kuelezea dhana za kisayansi kikamilifu. Mchango wa utafiti huu ni kusaidia kupendekeza uchapishaji wa toleo la pili la chapisho lilotafitiwa na jingine linalojumuisha istilahi za elimumisitu.

## YALIYOMO

<b>UNGAMO</b> .....	ii
<b>TABARUKU</b> .....	iii
<b>SHUKRANI</b> .....	iv
<b>VIFUPISHO</b> .....	vi
<b>MAELEZO YA ISTILAHU</b> .....	vii
<b>IKISIRI</b> .....	viii
<b>YALIYOMO</b> .....	ix
<b>SURA YA KWANZA</b> .....	1
<b>UTANGULIZI</b> .....	1
1.1 Usuli wa Mada .....	1
1.2 Tatizo la Utafiti .....	3
1.3 Maswali ya Utafiti.....	4
1.4 Malengo ya Utafiti .....	4
1.5 Sababu za Kuchagua Mada .....	5
1.6 Upeo na Mipaka .....	5
1.7 Yalioandikwa Kuhusu Mada.....	6
1.8 Msingi wa Nadharia .....	12
1.8.1 Mihimili ya nadharia ya kusudio.....	13
1.9 Mbinu za Utafiti .....	15
1.9.1 Muundo na eneo la utafiti.....	16
1.9.2 Uteuzi wa sampuli.....	18
1.9.3 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data.....	18
1.10 Hitimisho.....	18

<b>SURA YA PILI</b> .....	20
<b>VIPENGELE AMILIFU VYA TAFSIRI</b> .....	20
2.1 Utangulizi .....	20
2.2 Dhana ya Tafsiri .....	20
2.3 Dhima ya Tafsiri.....	21
2.4 Nadharia za Tafsiri .....	21
2.5 Habari Zilizobanwa .....	22
2.6 Habari Zilizozidishwa.....	24
2.7 Habari Zilizopotezwa .....	25
2.8 Habari Zilizopotoshwa .....	26
2.9 Msamiati na Isitilahi za Elimumisitu .....	28
2.10 Hitimisho.....	29
<b>SURA YA TATU</b> .....	30
<b>VIPENGELE AMILIFU VYA TAFSIRI VINAVYOBANA NA KUZIDISHA</b>	
<b>HABARI</b> .....	30
3.1 Utangulizi .....	30
3.2 Uchambuzi wa Ubanaji na Uzidishaji.....	30
3.2.1 Kuhusu ubanaji.....	30
3.2.2 Kuhusu uzidishaji.....	49
3.3 Muhtasari wa Matokeo ya Ubanaji na Uzidishaji .....	68
3.4 Hitimisho.....	69
<b>SURA YA NNE</b> .....	70
<b>VIPENGELE AMILIFU VYA TAFSIRI VINAVYOPOTEZA NA KUPOTOSHA</b>	
<b>HABARI</b> .....	70
4.1 Utangulizi .....	70
4.2 Kuhusu Upotezaji.....	70

4.3 Kuhusu Upotoshaji.....	77
4.4 Upotezaji na Upotoshaji wa Habari katika Mchakato wa Tafsiri .....	92
4.5 Masuala Ibuka .....	93
4.5.1 Msamiati na Istilahi za Elimumisitu.....	93
4.6 Hitimisho.....	96
<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>97</b>
<b>MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI.....</b>	<b>97</b>
5.1 Utangulizi .....	97
5.2 Muhtasari.....	97
5.3 Hitimisho.....	97
5.4 Mapendekezo .....	99
5.5 Sehemu za Kufanyiwa Utafiti Zaidi.....	100
<b>MAREJELEO.....</b>	<b>101</b>
<b>VIAMBATISHO.....</b>	<b>104</b>

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.1 Usuli wa Mada

Tafsiri hupitisha ujumbe asilia kwa nyenzo ya ishara tofauti tofauti za kiisimu. Mchakato wa tafsiri unaweza kuelezwa kuwa ni utoaji wa maana ya kimatini kutoka katika lugha chanzi (LC) hadi lugha lengwa (LL) kwa kutumia stadi maridhawa kiasi cha kuwa ujumbe asilia haupotoshwi wala kupotezwa. Pamoja na kwamba mtafsiri anaweza kutumia mbinu na stadi nyingi katika zoezi la kutafsiri, kuna uwezekano mkubwa kwamba mbinu zozote zilizotumikishwa katika zoezi hilo zinaweza kuathiri kiasi cha habari kinachopitishwa kutoka matini chanzi (MC) hadi matini lengwa (ML). Hali hizi zinazohusiana na kiasi cha habari kinachopitishwa kupitia kwa tafsiri zinaweza kutokea katika tafsiri nyingi na katika nyanja kama vile fasihi, sheria, matangazo ya aina mbalimbali, matibabu na makala ya dini miongoni mwa nyanja nyingine. Lakini, kwa sababu ya upekee wa sifa za nyanja husika, kuna kutofautiana juu ya kiasi cha habari kinachopitishwa kutoka MC hadi ML. Hii inatokana na kiwango cha utaalamu kinachojitokeza katika matini iliyokita katika nyanja maalum. Kwa mfano, kuna chukulizi kwamba matini ya kimatibabu inaweza kudhihirisha kiasi cha juu cha habari kinachopotea ikilinganishwa na matini ya kifasihi au hata kidini. Uhalisi huu hali kadhalika umeweza kujibainisha katika matini zinazohusiana na masuala ya mazingira. Hii inaweza kukisiwa kuwa inatokana na wasifu wa mazingira kama taaluma ambapo kumeibuka dhana, istilahi na msamiati mkubwa wa kuelezea mambo haya yanayoibuka.

Mbali na kwamba mikakati inayopendekezwa katika tafsiri inajumuisha ujuzi wa sarufi, msamiati na uelewa muruwa wa MC, uwezo wa kuhamisha maana kutoka matini ya LC hadi LL na kunasa mtindo wa matini asilia ili iwe kama utunzi asilia hasa, bado kuna kupotea na kupotoshwa kwa habari inayopitishwa katika tafsiri. Mikakati hii inastahili kutilia maanani majukumu ya tafsiri ndipo iweze kudhibiti kiasi cha habari kinachopitishwa. Mahitaji ya kimo cha chini ni kuwa hadhira lengwa (HL) waweze kuelewa matini namna ambavyo wasomaji asilia waliweza kuielewa. Kimo cha juu kinahusu kuishughulikia ML kihisia na kiakili, hali ambayo italeta makini katika ulinganifu wa kimatumizi (Reiss, 2000). Mikakati hii isipozingatiwa kunatokea upungufu kwa maana kwamba kuna ama mbano wa habari au uzidishaji wa habari kama ilivyoekezwa katika MC. Upungufu katika kazi zilizotafsiriwa hautaruhusu kutimiza malengo ya kazi yenyewe. Upungufu huu huenda

ukatokea kwa sababu ya kutoa tafsiri zisizotosha, zilizozidisha kiasi cha habari, zilizopoteza au zinazopotosha baadhi ya habari na haiwezi ikatumika kwa kutekeleza majukumu yanayostahiliwa.

Katika kazi hii utafiti ulikusudiwa kuangazia maswala yahusikayo na uhifadhi wa mazingira kama yalivyotafsiriwa kutoka Kiingereza hadi Kiswahili katika chapisho mahususi la Taasisi ya Utafiti wa Misitu, Kenya (Kenya Forestry Research Institute). Mazingira ni hali au mambo yanayomzunguka kiumbe katika sehemu aishiyo maisha yake. Katika muktadha wa kazi hii, mazingira yanasimamia mambo hai na mambo jengwa yanayotuzunguka au kwa lugha nyepesi, tunaweza kusema ujumla wa mambo yanayozunguka maisha. Mazingira asili hujumuisha vitu vitano vinavyotegemeana, navyo ni: hewa, maji, udongo, mimea na wanyama. Vipengele hivyo vyote hutekeleza kazi zao kwa mpango na uhusiano na uharibifu wa mojawapo huakisi hatari iwezayo kutukumba maishani. Pana masuala ibuka chungu nzima kuhusu uhifadhi wa mazingira (GoK, 2010; Mghanga, 2011). Masuala haya yanaathiri viwango vya maisha, kujirekebisha kwa mazingira yanayohusu mazao, kama timbao na huduma zitokanazo na maliasili.

Mambo yanayohusika katika viwango vya maisha nchini ni manne makuu kama: afya, uhakika wa chakula, viwanda na makao, ambayo ni msingi wa maendeleo endelevu. Mambo haya ya kimsingi yanaweza kuhujumiwa na changamoto kutokana na data na chapisho lisilo mwafaka kuhusu uhimili wa tabia nchi, ongezeko la viwango vya joto, uharibifu wa hewa kama vile ongezeko la hewa mkaa (Watkiss na wenzake, 2012), uhufadhi wa misitu, uchafuzi wa maji na kuzoa taka, udhibiti wake na utunzaji wa taka za elektroniki, vile vile udhibiti wa machafuko yanayoletwa na umwagikaji wa mafuta. Mambo haya yanaashiria kuwepo kwa haja ya kuibuka kwa maandishi yanayohusiana na mazingira. Kuibuka kwa mambo haya kuna maana ya kuibuka kwa mfumo mzima wa lugha, dhana, taaluma, msamiati na istilahi za elimumisitu (EM). Mambo haya ya kimazingira katika eneo la Afrika Mashariki yamekuwa yakiandikwa kwa Kiingereza. Si ajabu basi kwamba kumeibuka pia haja ya kuwa na kazi za Kiswahili. Pengine haja hii ndiyo iliyopelekea kuandikwa kwa kitabu: *"Social Forestry Techniques (1991)"*, ambayo imetafsiriwa kama: *Mbinu za Utunzaji Miti katika Misitu ya Jamii (1991)*. Kwa hivyo, kwa mtazamo wetu, anwani ya tafsiri yenyewe inaashiria matatizo yanayohusiana na kiasi cha habari kilichopitishwa katika tafsiri hii kwa njia mbili; kubadilishwa kwa mwelekeo wa habari yenyewe na kuibuliwa kwa uelewa tofauti na ule uliokusudiwa katika MC.

Tafiti nyingi zinazowafikia washika dau katika masuala ya uwanja wa mazingira ziko katika lugha ya Kiingereza. Ili kuufikia umma mpana inabidi kazi mbali mbali zitafsiriwe kutoka Kiingereza hadi Kiswahili ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu fulani. Tafsiri zinazotolewa katika uwanja huu wa mazingira zimeonyesha kutawaliwa na upungufu mkubwa wa uelewa wa kinachokusudiwa katika MC. Upungufu katika kazi zilizotafsiriwa hautaruhusu utimizaji wa malengo yanayotarajiwa na kazi zenyewe. Hii ni kwa sababu zimefanywa kwa namna ambayo habari zilizotolewa katika lugha asilia huenda siyo habari zinazofikia HL inayopokea tafsiri katika lugha lengwa (LL). Pana haja ya kutafsiri kazi hizi zinazohusishwa na taaluma ya kimazingira, haja yenyewe ikikabiliwa na changamoto za kitafsiri kama vile haja ya kudhibiti maana ya dhana za kimsingi katika masuala ya mazingira na kubuni istilahi sawia katika lugha ya Kiswahili, kuchunguza kuwepo au kutokuwepo kwa dhana hizi na kutambua michakato ya kijamii na kiufundi inayohusiana na uhifadhi wa mazingira.

Masuala yanayohusiana na kiasi cha habari kinachopitishwa katika tafsiri yanaweza kutokana na sababu nyingi ikiwa ni pamoja na uzidishaji wa uhalisi wa MC kutokana na nyongeza za maelezo, ubanaji wa uhalisi huo kutokana na kudondoshwa kwa mambo mengi yaliyo katika MC na pengine upotoshi na upotezaji wa maana ya MC kwa sababu ya uwezo wa lugha alionao mtafsiri au pengine kwa sababu ya mikakati anayoitumia katika utekelezaji wa tafsiri husika. Hali hizi zina athari ya moja kwa moja katika kuathiri kiasi cha habari kinachopitishwa kutoka MC hadi ML. Lakini, licha ya kwamba kuna tafiti nyingi katika lugha ya Kiswahili zilizoshughulikia tafsiri, hapana ushahidi wowote kwamba suala la kiasi cha habari kinachopitishwa katika tafsiri limewahi kujumuishwa katika tafiti hizo. Kwa hivyo, katika kushughulikia tafsiri ambazo zimekusudiwa kimsingi kutekeleza majukumu mahususi katika lugha lengwa, ipo haja ya kuangazia kiasi cha habari kinachopitishwa katika tafsiri. Hii ni kwa kuzingatia ukweli kwamba kiasi cha habari katika tafsiri ni kigezo muhimu katika utekelezaji wa majukumu yanayokusudiwa.

## **1.2 Tatizo la Utafiti**

Suala linalotafitiwa katika utafiti huu linahusu utathmini wa kiasi cha habari kinachopitishwa katika tafsiri kwa kuangazia chapisho la Kiingereza: *"Social Forestry Techniques"* lilotafsiriwa kwa Kiswahili kama, *"Utunzaji wa Miti Katika Misitu ya Jamii"*. Suala hili limechochewa na uelewa wetu kwamba njia moja ya kuhakikisha kwamba tafsiri ina uwezo wa kutekeleza majukumu

mahususi katika miktadha lengwa ni kukadiria kiasi cha habari kilicho katika matini lengwa ikilinganishwa na matini chanzi. Kwa mfano, katika chapisho la “*Social Forestry Techniques*” lililokusudiwa kufahamisha, kuelimisha na kuhamasisha umma kuhusu masuala ya uhifadhi wa mazingira, kuna haja ya kuchunguza kiasi cha habari kinachopitishwa katika tafsiri ya Kiswahili ya chapisho hili. Katika kuchunguza kiasi cha habari kinachopitishwa katika mchakato wa tafsiri ya kijitabu hiki katika Kiswahili, matatizo ya tafsiri yanaweza kugunduliwa na mikakati mwafaka kupendekezwa juu ya jinsi ya kuhifadhi habari katika mchakato wa tafsiri. Haya yakifanyika umma mpana utafikiwa na ile haja ya kuhifadhi mazingira itatekelezwa. Ushahidi wa awali unaojitokeza katika chapisho hili katika tafsiri yake ya Kiswahili ni kwamba baadhi ya habari kwa kweli zimebanwa, nyingine kuzidishwa, baadhi kupotezwa na nyingine kupotoshwa. Pengo hili litaonyeshwa kama lipo na kupendekeza njia za kuleta uimarishaji wa kazi kama hizo.

### **1.3 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu unachunguza toleo mahususi “*Social Forestry Techniques*” ambalo lilitafsiriwa kwa Kiswahili kama “*Utunzaji wa Miti Katika Misitu ya Jamii*”, kwa hivyo utafiti huu unalenga kujibu maswali ya utafiti yafuatayo;

- 1) je, ni kiasi gani cha habari zimebanwa katika matini lengwa kutoka katika matini chanzi?
- 2) Je, pana kiasi gani cha habari ambazo zimezidishwa katika matini lengwa ikilinganishwa na matini chanzi?
- 3) je, kumetokea kiasi gani cha upotezaji na upotoshaji wa habari katika matini lengwa kutoka katika matini chanzi?

### **1.4 Malengo ya Utafiti**

Utafiti huu unalenga kutekeleza malengo yafuatayo;

- 1) kuchunguza uwepo wa habari zilizobanwa katika matini lengwa kutoka katika matini chanzi.
- 2) kuhakiki uwepo wa kiasi cha habari ambazo zimezidishwa katika matini lengwa ikilinganishwa na matini chanzi.
- 3) kutathmini kiasi ambacho kimetokea cha upotezaji na upotoshaji wa habari kutoka katika matini chanzi zikifika katika matini lengwa.

### **1.5 Sababu za Kuchagua Mada**

Utafiti huu ulifanywa ili kuangazia suala la kimsingi katika utafiti wa tafsiri unaokita katika kutathmini kiasi cha habari kinachofikishwa katika matini lengwa kupitia kwa tafsiri. Hii ni njia moja ya kufidia sehemu ya tafsiri ambayo haijashughulikiwa. Tafiti nyingi za tafsiri zilizoko katika lugha ya Kiswahili ziko katika uwanja wa fasihi, sheria, matangazo, matibabu na dini, na nyingi zinaangazia masuala ya ulinganifu wa maana, udhaifu wa tafsiri na masuala sawia na hayo. Tafsiri za Kiswahili zinazojishughulisha na kiasi cha habari katika matini lengwa, kama zipo ni chache mno. Changamoto katika kazi hizi ambazo zimetafitiwa ni kuhusu usahihi au kuwepo kwa makosa, ulinganifu na mikakati. Hakuna ithibati kwamba kipengele cha kiasi cha habari katika tafsiri kimewahi kushughulikiwa, kwa hivyo, hali hii inahalalisha utafiti wa 'Kiasi cha Habari Kinachopitishwa katika Tafsiri': kifani cha *"Social Forestry Techniques"*. Mapitio ya awali ya chapisho hili yanaonyesha uwezekano wa tafsiri hii iliyotumiwa hapa kuonyesha mbano, uzidishaji, upotezaji na upotoshaji wa habari.

Tafsiri kama chombo muhimu cha mawasiliano huathiri shughuli mbalimbali katika maisha, mojawapo ikiwa mazingira. Iwapo habari zipo katika lugha fulani ambayo wananchi hawaelewi, inabidi itafsiriwe hadi katika lugha inayoweza kueleweka na wapokezi wa ujumbe au HL. Kwa sababu hii, pana haja ya kutambua pengo au upungufu katika ujuzi na kutoa ithibati tosha ili kudhihirisha mchango wa tafsiri kama mkakati unaoathiri uhifadhi bora wa mazingira kwa muda. Ni jukumu la mtafsiri kuchagua vitendo vya tafsiri kama mkakati unaohusika na uhifadhi bora wa mazingira. Washika dau wote katika mazingira wanaweza kunufaika na kazi hii, wakiwa watu binafsi, wafanyikazi wa umma, mashirika yasiyo ya serikali na washirika wa maendeleo. Mchango wa kazi hii utakuwa wa kupendekeza jinsi ambavyo tafsiri inavyostahili kufanywa katika uelezaji wa habari za ukuzaji miti kama mojawapo wa juhudi za uhifadhi wa mazingira, ili kuleta ulinganifu wa kimatumizi.

### **1.6 Upeo na Mipaka**

Utafiti huu ulijikita katika kijitabu cha *"Mbinu za Utunzaji wa Miti katika Misitu ya Jamii"* ambayo inachukuliwa kuwa tafsiri ya *"Social Forestry Techniques"*. Pia utafiti ulishughulikia masuala manne makuu: ubanaji, upanuzi, upotezaji na upotoshaji wa habari katika kitabu hicho wakati wa kufanywa kwa tafsiri yake, kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Kwa hivyo, kimsingi utafiti huu

ulikita kutathmini masuala haya kama njia ya kukadiria kiasi cha habari kinachopitisha kupitia michakato ya kutafsiri habari za kitaaluma na haukuyashughulikia masuala ya ulinganifu wa kimaana.

### **1.7 Yalioandikwa Kuhusu Mada**

Jakobson (1959) katika kazi yake ya "*On Linguistic Aspects of Translation*" aliasisi fikra tatu kuhusu tafsiri; tafsiri ndani ya lugha moja ambapo mtu hubainisha maana ya ishara za kiisimu katika lugha moja tu, pili ni tafsiri kati ya lugha mbili ambapo mtu hutafsiri matini kutoka LC hadi LL. Tafsiri hii ndiyo tafsiri ya kihistoria na iliyozoeleka kimaana kupitia urudiaji au unakili. Tatu ni tafsiri za kisemiotiki ambapo ishara za kiisimu hutafsiriwa maana kwa kutumia ishara zisizo za kiisimu. Hii ndiyo tafsiri ya uvumbuzi kwani ina dhana inayopita mipaka ya maneno. Katika kazi hii tafsiri kati ya lugha mbili ndiyo itashughulikiwa.

Akiwa pia katika shule hii ya Prague, mtafsiri na mwanahistoria wa fasihi, Levy (1967) aliandika insha iitwayo, "*Translation as a Decision Process*". Kutokana na hayo, waandishi na wananadharia wa miaka ya baadaye wamekuja kupendezwa na dhana kama utendaji, ufaafu na usemezaji katika tafsiri. Jambo linalotathminiwa katika kazi hii, ni kiasi cha habari katika mbinu za utunzaji miti, ikichunguzwa iwapo habari zilizofikishwa katika ML zinaakisi kikweli habari zilizoko katika matini chanzi ikilinganishwa na ML. Matarajio ni kuwa ufaafu na utendaji utawezekana ikiwa mambo yanayoleta upungufu kama vile ubanaji, uzidishaji, upotezaji na upotoshaji yatachunguzwa na mapendekezo kutolewa.

Waandishi mbalimbali kama Ali (1981), Aissi (1987), Pym (1990), Nord (1997), Dimitriu (2004), Muñoz (2012), Rahmatilla (2013) na wengineo, wanafuatilia mawazo ambayo yanakaribiana kuwa katika kazi za tafsiri uamilifu ndio muhimu ili kufanikisha matokeo bora. Wanaangazia pia, changamoto ambazo watafsiri hukumbana nazo katika matini zinazotafsiriwa na kuwa lazima zikwepwe. Changamoto hizi zinahusishwa na mikabala na makosa ya: kisarufi, kimaendelezo, kileksika na kisemantiki; kiuamilifu na diskosi pamoja na ubanaji, urudiaji na uzidishaji miongoni mwa mengine. Utafiti huu ulikusudia kutambua na kuwezesha suluhisho la kuimarisha kiwango cha machapisho yanayochunguzwa hapa. Pamoja na haya, utafiti huu pia ulishughulikia ushawishi wa kiasi cha habari zinazopitishwa na mchakato wa tafsiri kutoka katika MC hadi ML.

Makosa mbali mbali yanayojitokeza katika tafsiri za taarifa za habari za Sauti ya Kenya yamejadiliwa na Ali (1981). Alidhihirisha vile vile namna ambavyo tafsiri mbaya zinapotosha mawasiliano kati ya idhaa hii na wasikilizaji wake. Alitaja matatizo yakiwemo ukosefu wa ujuzi wa kutosha upande wa watafsiri, muda mfupi wa kuandika tafsiri pamoja na matatizo mengi yasiyofungamana moja kwa moja na lugha. Kazi hiyo ilichunguza tafsiri kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Utafiti huu vilevile unaangazia tafsiri kutoka Kiingereza hadi Kiswahili lakini katika kitabu cha taaluma ya mazingira cha "*Social Forestry Techniques*".

Aissi (1987) anaeleza kuwa mchakato wa tafsiri huongozwa na mikabala minne. Mikabala ya kisarufi iliyopendekezwa na Catford (1965) ambayo inachukulia tafsiri kama njia ya kuondoa tofauti ya kimuundo kati ya lugha tofauti. Mkabala wa kihusanishaji (*hermeneutic model*) uliopendekezwa na Steiner (1975) ambao unachukulia tafsiri kama maelezo na ufafanuzi wa matini chanzi. Mkabala wa hali uliopendekezwa na Vinay na Darbelnet (1958) unaosisitiza hali inayozingira tafsiri ya kazi husika na wala si maana. Mkabala wa umbo zalishi uliopendekezwa na Nida na Taber (1969) unaochukulia kuwa kimuundo lugha zote zinafanana. Mkabala huu ni toshelezi katika kutafsiri sentensi fupi fupi lakini una upungufu kazi ndefu zinapohusika. Aissi alitafiti mchakato na hatua za tafsiri kwa kuangazia lugha ya Kiingereza na Kiarabu. Mbali na kuainisha mikabala hiyo minne, anasema kuwa kila mkabala una upungufu wake na hivyo ili kuweza kupata tafsiri bora. Mtafsiri anapaswa kuwa na sifa mahususi; awe na umahiri wa lugha, maarifa ya sheria za lugha kifonolojia, kisintaksia na kimofolojia, uwezo wa kutohoa ujumbe kutoka kwa muundo wa kiisimu na kuchambua matini na ujumbe huo kisemantiki na kipragmatiki.

Mambo yanayochangia, kuathiri na kusababisha makosa ambayo yanaathiri lugha na mtindo katika ML yalisisitizwa na Mutie (1997). Alionyesha athari zinazotokana na mtafsiri kutozingatia muktadha ambamo lugha imetumika. Ukwasi wa mtafsiri kiisimu na kutozingatia muktadha ambamo lugha imetumika ni athari zilizobainika. Kutokana na utafiti wake aligundua kuwa ulinganifu wa MC na ML huathiriwa sana na tofauti za miundo ya lugha zinazotofautiana. Kila lugha ina muundo wake wa kipekee na sheria zake kifonolojia, kimofolojia na kisarufi. Pia tafsiri huathiriwa na tofauti za kimazingira na kitamaduni. Haya husababisha tofauti za kimaana na kifalsafa kwa sababu yote hufungamana na utamaduni maalum. Mtafsiri anapokosa kuelewa dhamira ya MC, kuelewa wajibu wake katika tafsiri na asipokuwa na utaalamu wa kazi

inayotafsiriwa kutatokea dosari katika tafsiri. Hata hivyo, anasema kuwa wakati mwingine mtafsiri hukosa kisawe na hivyo kuishia kutokuwa mwaminifu kwa mwandishi. Utafiti huo utasaidia utafiti huu kuelewa makosa ambayo hufanywa wakati wa tafsiri. Hata hivyo utafiti huo ulizingatia mambo yanayosababisha makosa hayo ilhali utafiti huu utazingatia makosa mahususi ya ubanaji, uzidishaji, upotezaji na upotoshaji wa ujumbe katika tafsiri.

Merkel (2001) katika kuchunguza uhusiano uliopo baina ya MC na ML, alitumia mkusanyiko wa tafsiri ya Linköping. Hapo lugha ya Kiingereza kilitumiwa kama MC na lugha ya Kiswidi kama ML, kazi ambayo iliundwa na kupakuliwa kwenye mtandao. Aligundua kwamba kuna njia mbili kuu za kuchunguza uhusiano uliopo baina ya matini chanzi na matini lengwa. Uhusiano unaweza kuchunguzwa kwa kuangalia matini hizo mbili kama kazi mbili tofauti zisizotegemeana. Njia ya pili ni kuchunguza uhusiano kwa kuangalia matini hizo kama ambavyo ni kazi mbili tofauti zinazotegemeana. Pia, anabainisha kwamba tatizo kuu katika tafsiri hiyo ni kuongezwa au kuondolewa kwa maneno, jambo lililoashiria kuwa tafsiri ile haikuwa kazi asilia bali ilikuwa mbinu ya kupitisha ujumbe. Anaongezea kwamba tafsiri hiyo iliundwa kwa kusaidiwa na vielelezo vya kiteknolojia hivyo ilichukua sana mwelekeo wa matini lengwa na kuacha ule mwelekeo wa matini chanzi. Kazi ya Merkel inasaidia utafiti huu kuelewa kuwa kuna uhusiano katika matini zilizotafisiriwa na pia inadokeza kuwa huwa kuna matatizo yanayokumba mchakato wa tafsiri. Hata hivyo ametaja kwamba huenda kukawa na kuongezwa au kuondolewa kwa baadhi ya maneno bali hakuonyesha hilo hutokea vipi na wala hakutoa hata mfano. Pia utafiti wake uliegemea mkusanyiko wa maandishi yaliyotafsiriwa kiteknolojia. Utafiti huu utaegemea matatizo mahususi yanayojitokeza katika kazi ya tafsiri na kuonyesha jinsi yanavyojitokeza katika matini lengwa. Pia utafiti huu utatumia kitabu na wala sio matini kutoka mtandaoni.

Vipengele vya kisarufi ni muhimu kuvizingatia katika tafsiri kama ilivyojadiliwa na Kihore (2005). Vipengele hivyo ni maneno au istilahi zinazosadifu muktadha wa maelezo na miundo ya sentensi inayofuata kanuni za lugha. Pia ameelezea kipengele cha miundo maalumu, yaani ile iliyofungana na mitazamo ya dunia ya wahusika wa lugha. Anasema kuwa, katika tafsiri kuna fahiwa zinazotakiwa kujitokeza ili maana iweze kudhihirika ilivyo katika LC. Mara nyingi, fahiwa huwa hazijitokezi wazi wazi tafsiri inapokuwa sisisi. Kwa hiyo, wakati mwingine inabidi muundo katika tafsiri unyumbuliwe ili uweze kudhihirisha hizo fahiwa. Maelezo ya Kihore yanasaidia utafiti huu

kugundua kuwa fahiwa ni muhimu katika tafsiri na vilevile katika kupitisha ujumbe husika. Hata hivyo Kihore anazungumzia tafsiri kwa mkabala wa kisarufi ilhali utafiti huu hautaingilia maswala ya miundo ya sentensi na kanuni za lugha. Utafiti huu ulijifunga katika ubanaji, uzidishaji, upotezaji na upotoshaji wa ujumbe katika tafsiri.

Pobocikova (2012) alitathmini ubora wa tafsiri iliyofanywa zaidi ya mara moja. Alitafiti kazi za kiuhandisi zilizotafsiriwa mara nne, kati ya lugha ya Czech na lugha ya Kiingereza kwa nia ya kubainisha makosa yanayofanywa katika vipashio vya tafsiri na kupendekeza namna ya kukwepa makosa hayo. Alichunguza tafsiri zilizofanywa na wataalamu wa tafsiri waliofanya kazi katika taasisi za tafsiri na wanafunzi wa tafsiri. Aligundua kuwa ML zilikuwa na makosa ya lugha; makosa ya kiuakifishi na makosa ya upangaji wa nomino na vitenzi katika sentensi. Anaeleza kuwa kosa lililokuwa na umara-tokezi mkubwa (frequency) ni kupotea kwa ujumbe ambao upo katika MC lakini haupo kwenye ML. Upotezaji huu hushawisi kiasi cha habari kinachofikia ML. Makosa mengine aliyogundua ni utohozi au uwasilishaji wa baadhi ya misamiati kwa sababu ya kukosa istilahi mwafaka katika LL. Anapendekeza kuwa ili kuepukana na makosa haya mtafsiri afuate maelekezi yanayopendekezwa na nadharia ya 'Skopos' katika nadharia ya Reiss na Vermeer (1984). Pia mtafiti achunguze uamilifu wa matini husika kabla ya tafsiri. Anapendekeza kwamba mtafsiri atafute neno mwafaka zaidi wakati wa tafsiri na baada ya tafsiri mtafsiri ahakikishe kwamba hajaondoa chochote na kwamba kazi inayofanywa na MC ndiyo itakayofanywa na ML. Kazi ya mtafiti huyu imesaidia utafiti wetu kuelewa makosa ambayo hutokea wakati wa tafsiri na namna ya kuepukana na makosa hayo. Utafiti wake pia unaegemea istilahi za taaluma ya uhandisi. Hata hivyo, mtafiti huyu hakuangazia vipengele vya ubanaji, uzidishwaji na upotoshaji wa habari, vipengele ambavyo utafiti huu ulinua kuchunguza. Pia utafiti huu kinyume na wake wa kiuhandisi, uliegemea tafsiri katika taaluma ya mazingira kuhusu kiasi cha habari katika ML.

Ahmed (2016) alichunguza ubanaji na upanuzi wa ujumbe katika mivigha ya mazishi ya nabii Mohammed katika dini ya Kiislamu. Alilinganisha tafsiri iliyofanywa na watu watatu wa mivigha hiyo hiyo. MC ya mivigha hiyo ilikuwa Kiarabu ilhali ML ya mivigha hiyo ilikuwa ni Kiingereza. Aligundua kuwa kila mwaandishi aliondoa baadhi ya ujumbe katika kazi ile na hivyo kuishia kuubana ule ujumbe hivi kwamba anayesoma MC aliupata ujumbe ule kwa njia tofauti ilhali aliyesoma ML asingeliupata kwa maana kwamba baadhi ya sifa za ujumbe huo zilidondoshwa. Pia

aligundua kuwa watafsiri wote watatu waliongezea ujumbe fulani hivyo kuishia kupanua ujumbe ule hivi kwamba anayesoma ML angelipata ujumbe huo ilhali anayesoma MC asingeliupata ujumbe ule ule. Aligundua kuwa uondoshaji na uongezaji ujumbe uliopo katika matini hii uliandamana na utamaduni wa Kiislamu. Vile vile ni kana kwamba watafsiri wale walifanya makosa haya ama kwa kujua au kotojua lakini kwa misingi ya kukidhi mahitaji ya waislamu. Utafiti huo ulisaidia utafiti huu kuelewa misingi ya ubanaji na upanuzi wa ujumbe. Pia unaonyesha umuhimu wa kuzingatia utamaduni husika katika tafsiri. Hata hivyo aliishia tu kuonyesha ubanaji uliotokea na upanuzi uliotokea katika matini husika. Mtafiti huyo hakuonyesha ikiwa ubanaji na upanuzi huo uliathiri kwa njia yoyote kiasi cha habari uliopitishwa na vilevile ikiwa kulitokea upotoshaji au upoteaji wa ujumbe. Ni maoni yetu kuwa ulinganifu wa tafsiri hauta tosheleza mahitaji ya ML katika tafsiri zenye kusudi. Utafiti huu utaegemea ubanaji na upanuzi wa ujumbe katika matini na vile vile upotoshaji na upoteaji wa ujumbe katika matini husika ili kubainisha ikiwa vipengele hivi vinaathiri kiasi cha habari au ujumbe unaopitishwa.

Muzaffar na Behera (2017) walishughulikia dhana za usawazishaji, uongezaji na udondoshaji wa ujumbe katika lugha ya Kiingereza na Urdu kwa kuainisha na kuchanganua data kutoka *Google* na *Bing*. Usawazishaji kama kipengele kilichaguliwa sambamba na uongezaji na udondoshaji ili kuangalia iwapo muundo wa MC na ML unafanana na kutofautiana. Waligundua kuwa katika tafsiri za mitandao, vipengele hivi havikuathiri maana ya ujumbe. Pia waligundua kwamba lugha na utamaduni ulikuwa na nafasi kubwa katika kiasi cha uongezaji na upotezaji wa MC na ML. Utafiti huo unasaidia utafiti huu kuelewa matatizo ambayo hujitokeza katika tafsiri. Hata hivyo, utafiti huo ulijikita katika tafsiri ya mitandao. Utafiti huu utaegemea tafsiri katika vitabu. Pia utachunguza vipengele mahususi ambayo huathiri kiasi cha habari ambazo hupitishwa wakati wa tafsiri.

Vitenzi vya mkao (simama, keti, lala) katika mazungumzo, vina umara-tokezi (frequency) mkubwa katika lugha ya Kiswidi kushinda lugha ya Kiingereza. Hata hivyo wanaojifunza Kiswidi kama lugha ya pili hutumia mkusanyiko wa tafsiri yake na Kiingereza na umahiri wao wa lugha ya Kiingereza kutafsiri vitenzi vya mkao, kwa hivyo umara-tokezi wa vitenzi hivyo unapungua wanapozungumza lugha ya Kiswidi (Viberg, 2016). Anaongezea kwamba kwa kawaida vitenzi hivi vya mkao vina umara-tokezi mkubwa katika lugha ya Kiswidi. Alipolinganisha tafsiri ya mazungumzo ya Kiswidi kama lugha ya kwanza na mazungumzo yake kama lugha ya pili,

aligundua kwamba vitenzi vya mkao vilikuwa vingi miongoni mwa wazungumzaji wa Kiswidi kama lugha yao ya kwanza ilhali vilikuwa vichache miongoni mwa waliozungumza Kiswidi kama lugha ya pili. Hali ambayo haikuwa kawaida na ilisababishwa na tafsiri. Utafiti wa Viberg unasaidia utafiti huu kuelewa kuwa tafsiri inaweza kuchunguzwa kwa kuangalia vipashio mbalimbali vya lugha kwa mfano nomino na kitenzi. Amejikita katika kipashio cha vitenzi hasa vitenzi vya mkao. Hata hivyo utafiti huo haujaangazia ikiwa umara-tokezi mkubwa au kupungua kwa vitenzi hivyo katika mazungumzo unabana, unazidisha, unapoteza au kupotosha ujumbe au unapitisha ujumbe unavyofaa. Utafiti huu unaangazia ubanaji, uzidishaji, upotezaji na upotoshaji wa ujumbe baada ya tafsiri.

Tathmini ya hatua za tafsiri kama nyenzo ya ufanisi wa mawasiliano katika tafsiri ilifafanuliwa na Jilala (2017). Ili kufikia lengo hilo, makala hayo yamefanya ufafanuzi wa hatua za tafsiri zilizopendekezwa na Jilala (2014) ambaye anapendekeza kuwa hatua za tafsiri kitamaduni ziwe; maandalizi, utafutaji wa visawe vya kitamaduni, uhusiano (kupima uhusiano wa ujumbe wa utamaduni chanzi na utamaduni lengwa katika MC na ML) na hatimaye uzalishaji wa ML. Jilala alitumia mifano ya matini za kitalii kuonyesha jinsi ambavyo hatua hizo zinafanyika kwa vitendo katika mchakato wa tafsiri. Ameweza kupima na kuonyesha ufaafu wa hatua hizo katika tafsiri. Aligundua kuwa ufanisi wa mawasiliano hutegemea uzingatiaji wa hatua bora za tafsiri ili kuondoa matatizo ya tafsiri. Anaeleza kwamba hatua za tafsiri ndizo kiungo muhimu katika zoezi la tafsiri na humwongoza mtafsiri katika kuteua mbinu mwafaka za kutafsiri na kuzalisha matini bora zaidi. Utafiti huo unapendekeza na kufafanua hatua za tafsiri. Hata hivyo haujaangazia matatizo ambayo hujitokeza katika tafsiri. Utafiti huu unaangazia matatizo ya ubanaji, uzidishaji, upotezaji na upotoshaji wa ujumbe ambayo hujitokeza katika tafsiri ili kung'amua ikiwa matatizo hayo yana athari yoyote kwa kiasi cha habari zinazopitishwa.

Tafiti hizo na mapitio ya maandishi yameangazia tafsiri kutoka LC hadi LL kwa kuegemea lugha mbalimbali za ulimwengu na lugha ya Kiingereza pamoja na Kiswahili na matatizo yanayojitokeza katika tafsiri. Hata hivyo, hamna utafiti uliongazia kiasi cha upitishwaji wa ujumbe kwa kuzingatia ubanaji, uzidishaji, upotezaji na upotoshaji wa habari. Utafiti huu unaangazia upitishwaji wa kiasi cha habari katika tafsiri kwa kuchunguza ubanaji, uzidishaji, upotezaji na upotoshaji wa habari unaojitokeza katika tafsiri ya "*Social Forestry Techniques (1991)*" ambacho kimeandikwa na

kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili kama "*Mbinu za Utunzaji Miti katika Misitu ya Jamii (1991)*". Pia utafiti huu kinyume na ambazo zimefanywa unajikita katika tafsiri katika taaluma ya mazingira kiisimu na kwa kuchunguza kiasi cha habari kinachofika katika ML huku habari zenyewe zikitarajiwa kutekeleza majukumu ya kuhamasisha uma kuhusu uhifadhi wa mazingira kwa upandaji wa miti.

### **1.8 Msingi wa Nadharia**

Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni nadharia ya kitendo, kitendo chenyewe kikiwa na kusudi. Nadharia hii iliasisiwa na Vermeer (1978). Alitumia neno 'Skopos', neno la Kiyunani linalomaanisha shabaha au kusudio kuelezea makusudio na tendo la tafsiri. Matini lengwa ndiyo ilipewa umuhimu wote na nafasi kubwa. Kusudio linalofaa tafsiri ndilo lina umuhimu wote huku ulinganifu wa kiisimu ukiachwa nyuma. Huu ulikuwa mtazamo mpya wa kuangalia tafsiri na ambao haujafungwa na ile desturi ya kawaida ya kuipa matini asilia umuhimu. Vermeer (1978) alipata kuwa, kulingana na nadharia ya kitendo, kila tendo lina kusudio, na kwa vile kila tafsiri ni tendo vile vile, lazima iwe na kusudi.

Reiss (1984) naye aliasisi ugawanyaji wa kusudio lile lile aliloeleza Vermeer (1978) katika aina tatu za matini. Kwanza aliongea juu ya matini zinazoarifu na ambazo zinatoa habari kimantiki, pili; alieleza kuhusu matini za kielezi ambazo zinatumia lugha kisanaa, na ya tatu; matini za kutenda kazi ambazo ni za kidayalojia na hutoa majibu. Kwa mujibu wa Reiss (1984), upitishaji wa mambo ya kiutendaji ya MC ndiyo itatoa tathmini ya ML. Reiss na Vermeer (1984) wanatoa kanuni ya kusudio kuwa tendo la tafsiri linategemea shabaha ya kazi yenyewe. Kuwa kazi itakayotokea ndiyo inampa mtafsiri mtindo atakaotumia. Wanaongezea kuwa kila matini hutolewa kwa kusudi maalum na inastahili ifae kusudio hili. Hii ni kanuni inayosema kuwa: tafsiri, ufasiri, uzungumzaji na kuandika kwa njia ambayo itawezesha matini kufaa katika muktadha ambamo itatumika na watu wanaonua kuitumia kwa njia hasa wanayotaka iwafae.

Mwasisi mwingine, Holz-Manttari (1984) aliongeza maelezo ya tendo la kitafsiri, kuwa nadharia hii ina misingi yake katika nadharia ya kitendo. Aliongea kuhusu tafsiri kuundwa kwa njia ya kugusia aina zote za uhamishaji unaofanyika baina ya tamaduni mbali mbali. Kwake yeye tafsiri inaelezwa kama tendo changamano linaloundwa kufaulisha kusudi mahususi. Anahimiza

uchanganuzi wa majukumu ya wahusika na hali za muktadha ambamo vitendo vyao vinafanyika. Madhumuni hasa ya tendo la tafsiri ni kuruka vikwazo vya kitamaduni na kilugha kupitia viwasilishi vya ujumbe vinavyotolewa na wataalam.

Vermeer (1989a) katika Nord (2005) aliendelea kueleza azimio na kusudio huku akigawanya makusudio matatu yanayowezekana:

- 1) kusudi la jumla linalolengwa na mtafsiri katika mchakato wa tafsiri,
- 2) kusudi la mawasiliano linalolengwa na ML katika muktadha huu,
- 3) kusudi linalolengwa na mkakati na utaratibu,

Vermeer (1989a) alieleza kuwa shabaha na kusudio ndiyo muhimu.

Nord (1991) katika kuondoa utata alitoa pendekezo la kutofautisha shabaha na kusudio. Alisema mpelekaji ujumbe ana wajibu wa kupambanua kusudio na kwa kutumia matini anajaribu kufaulisha kusudio fulani. Anaendeleza kauli kuwa mtafsiri hupokea habari na maagizo ya kimsingi lakini hapo baadaye ana uhuru wa kutekeleza maagizo haya. Nord ameyaita maagizo ya tafsiri, ambayo yanataja agizo lake na kusudio. Amri ya kutafsiri ndiyo inatoa hasa lengo la kipande cha tafsiri kuwa mtafsiri lazima afasiri habari za MC kwa kuchagua vile vipengele vyake ambavyo vinalingana kwa karibu sana na mahitaji ya muktadha lengwa.

### **1.8.1 Mihimili ya nadharia ya kusudio**

- i) Tafsiri yoyote inategemea kusudi lake. Mhimili huu ulitumiwa kuonyesha kusudi la kutafsiri kitabu "*Social Forestry Techniques*" ambacho kimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza hadi "*Mbinu za Utunzaji Miti katika Misitu ya Jamii*" ambacho kimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Je, lengo la kutafsiri kitabu hiki lilikuwa lipi? Kwa nia gani? Mhimili huu ulisaidia kujibu maswali haya hivyo kuweza kuonyesha kiasi cha ujumbe kilichopitishwa na tafsiri ya kitabu "*Social Forestry Techniques*".
- ii) ML ni toleo la habari katika tamaduni chanzi na tamaduni lengwa. Nguzo hii ilitumiwa kuonyesha utamaduni asilia uliondikiwa katika kitabu hiki na pia kuonyesha utamaduni lengwa uliotafsiriwa kitabu hiki. Ni nguzo hii ndiyo itakayomwezesha mtafiti kugundua habari iliyopotoshwa na kupotezwa katika tafsiri iliyolenga tamaduni lengwa.
- iii) ML haianishi toleo la habari kwa njia inayoweza kurejeshwa katika matini asilia.

- iv) ML lazima iwe na mshikamano wa ndani. Mhimili huu ulitumiwa kutimiza malengo na kujibu maswali; je kuna habari zilizobanwa katika tafsiri ya "*Social Forestry Techniques?*"; je, kuna habari zilizozidishwa katika tafsiri ya "*Social Forestry Technique?*" Mhimili huu ndio uliotumiwa kukusanya data zinazoonyesha habari ziliziobanwa au kuzidishwa.
- v) ML lazima iwe na mshikamano na MC. Mhimili huu ulitumiwa kukusanya data inayoonyesha kuwa matini lengwa inafanana na matini chanzi. Ni mhimili uliotumiwa kuonyesha habari zilizopotoshwa na hata kupotezwa katika tafsiri ya "*Mbinu za Utunzaji Miti katika Misitu ya Jamii*".
- vi) Sheria hizi tano zinachukua mfuatano wa moja kwa moja bila kuacha hata moja, kanuni ya kusudio ikitawala.

Nadharia ya kusudio (Vermeer, 1978) ilitumika katika utafiti huu kwani madhumuni au lengo hasa la kazi hii lilikuwa kuchunguza kiasi cha habari kinachopitishwa katika tafsiri kwa umma unaolengwa. Tafsiri ya kitabu "*Social Forestry Techniques (1991)*" yaani "*Mbinu za Utunzaji Miti katika Misitu ya Jamii (1991)*", ilifanywa ili ilete matokeo fulani, yaani; wasomaji waweze kupata, kuelewa na kukuza uelewa wa masuala yanayohusiana na kuhifadhi mazingira, hususan ukuzaji na utunzaji wa miti. Uchunguzi unafanywa iwapo habari zenyewe kutoka MC zinafika katika ML kwa kiasi kinachofaa huku ikitathminiwa kama pana mambo haya manne: ubanaji, uzidishaji, upotezaji na upotoshaji.

Nadharia ya kazi hii imetokana na vipengele na matakwa ya tafsiri ndani ya taswira ya nadharia. Inatumia nadharia ya ulinganifu wa kusudi inayozingatia umbo na maudhui ya ujumbe. Inasisitiza haja ya kuandika yanayoweza kutumika pekee au yanayolingana na yenye makusudi. Nadharia hii pia inaleta ulinganifu baina ya matini ya asilia na iliyotafsiriwa vile vile kuangazia sehemu za kiisimu kama: msamiati, sarufi, sintaksia na muundo wa lugha asilia. Mambo haya, yataweza kuwa na ushawishi mkubwa katika kiasi cha habari kwa kuzingatia habari zilizobanwa, zilizozidishwa, zilizopotezwa, na zilizopotoshwa. Haya yanatarajiwa kuchangia uelewa ulio imara na utendaji au utekelezaji wa maagizo. Uchanganuzi utafanywa moja kwa moja kutokana na machapisho katika Kiambatisho 1.

## 1.9 Mbinu za Utafiti

Katika sehemu hii ufafanuzi wa mbinu za utafiti unatolewa pamoja na muhtasari wa habari zilizotolewa katika kila sura kuelezwa. Majedwali yalitumiwa kutathmini kiasi cha habari zinazopatikana katika ML pia yamejumuishwa ili yachangie katika kuchambua uwepo wa ubanaji, uzidishaji, upotoshaji na upotezaji wa habari zenyewe katika mchakato wa kutafsiri matini za kiuhamasishaji katika taaluma ya utunzaji misitu. Pamoja na haya tunachunguza uwepo wa istilahi mpya zilizoibuka ili kutosheleza uelezaji wa dhana mpya katika mazingira kwa udumishaji wa maendeleo katika utafiti unaohusu tafsiri.

Utafiti huu ulikuwa ni wa kitaamuli kwani ulichukua mwelekeo wa kiufafanuzi, kiuelezaji na kiuchanganuzi pamoja na kuhusisha masuala ya kitakwimu ya moja kwa moja. Hii ni kwa sababu data zilizokusanywa ni zile zisizo za kitakwimulakini data zenyewe ziliwasilishwa kitakwimu katika jedwali. Maelezo yaliyotolewa yalitokana na matini za tafsiri za Kiingereza na Kiswahili kwa minajili ya kuthibitisha mambo manne ya kimsingi; ubanaji, uzidishaji, upotezaji na upotoshaji wa kiasi cha habari ya matini chanzi katika michakato ya kuhawilishwa kutoka matini chanzi hadi matini lengwa. Utafiti wa kitaamuli huwa umeandaliwa na kuelezwa katika kazi hii, (Creswell, 2009). Tumetumia maelezo japo pana sehemu ndogo ambayo imewasilishwa kwa takwimu (Buliba na wenzake, 2014). Utafiti huu vile vile ni wa kimaktaba

Utafiti huu ulihusu kudurusu vitabu mbali mbali, tasnifu, majuzuu na majarida; kwanza kwa kufanya mapitio ya maandishi yaliyoandikwa kuhusu mada hii na pili kwa kusoma nakala hizi mbili za vitabu; "*Social Forestry Techniques*" (1991) ambacho kimeandikwa na kimechapishwa kwa lugha ya Kiingereza na tafsiri yake ya Kiswahili "*Mbinu za Utunzaji wa Miti katika Misitu ya Jamii*". Vitabu hivi vimeandikwa na 'Social Forestry Training Project, Kenya/Japan'. Tulivichambua kwa mielekeo na misingi ya nadharia tuliyochunguza. Pamoja na haya tulipekuapekua mtandaoni ili kuongeza ujuzi kuhusu tafsiri na vipengele vile tulivyochunguza. Udurusu na njia hiyo nyingine ulitudhihirishia mianya kwenye tafsiri zenye kusudi na kutuelekeza katika kutoa mapendekezo ili kuziba mianya hii.

Katika utafiti huu kitabu cha Kiingereza cha "*Social Forestry Techniques*" na tafsiri yake iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili "*Mbinu za Utunzaji wa Miti katika Misitu ya Jamii*" viliteuliwa kupitia uteuzi makusudi (Neuman, 1997). Aina hii ya uteuzi ina uwezo wa kuchagua kitu kimoja, hasa kitabu, mwingoni mwa vingine. Hii ilituwezesha kudhibiti ulengaji wa taaluma mahususi. Patton (2002) pia anaeleza kwamba uteuzi wa kimakusudi unatumiwa kwa sababu ya kuaminika na kusadikika kwa data wala si kwa sababu ya usimamiaji au ujumuishaji. Anaongezea kuwa uteuzi makusudi hutumiwa kuchagua palipo na data nyingi mwafaka kwa utafiti husika. Kwa kuchambua vitabu viwili: "*Social Forestry Techniques*" na tafsiri yake, maneno, virai na sentensi zilikusanywa. Uchambuzi ulifanywa kwa kutumia mwongozo uliowakilishwa na jedwali. Mwongozo ulihusu ubanaji, uzidishaji, upotoshaji na upotezaji wa habari. Data zilikusanywa, kuchanganuliwa na kuwasilishwa kupitia kwa jedwali. Matokeo yalijadiliwa na mapendekezo kutolewa.

### **1.9.1 Muundo na eneo la utafiti**

Utafiti huu umekuwa wa kitaamuli kwa misingi kwamba data zilizokusanywa ni zile zisizo za kitakwimu. Utafiti huu ulifanyiwa maktabani; kwanza kwa kufanya mapitio ya maandishi yaliyoandikwa kuhusu mada hii na pili kwa kusoma nakala hizi mbili za vitabu; "*Social Forestry Techniques*" (1991) ambacho kimeandikwa na kuchapishwa kwa lugha ya Kiingereza na "*Mbinu za Utunzaji Miti katika Misitu ya Jamii*" (1991) ambacho ni tafsiri ya kile cha Kiingereza na kimeandikwa na kuchapishwa kwa lugha ya Kiswahili. Vitabu vyenyewe vinahusu masuala ya mazingira hususan utunzaji wa misitu na vinatumika nchini Kenya, na kuandikwa na 'Social Forestry Training Project, Kenya/Japan'.

Nakala hiyo ya Kiingereza, kijitabu ambacho ni matokeo ya miradi ya ushirikiano wa "Kenya/Japan Social Forestry Training Project" ikiwa ni mkusanyiko wa hoja za mihadhara inayojaribu kujibu maswali ya wananchi kuhusu shida zilizoibuka kuhusiana na uhifadhi wa mazingira. Mihadhara hii ilitolewa katika Chuo cha Mafunzo ya Misitu kilichoko katika eneo la Kitui kuanzia mwaka wa 1988. Hoja hizi za ukumbusho zilikusanywa ili kuwekwa kama kumbukumbu na kutumiwa kama marejeleo kwani hapakuwa na kitabu maalum kwa utekelezaji wa mradi huu. Chuo hiki hutoa huduma za mafunzo kwa watu kutoka sehemu za nusu-jangwa na maeneo kame katika eneo la Mashariki ya Kenya. Waandishi wa kitabu hicho walitambua thamani isiyopimika ya mazingira katika maisha ya binadamu. Katika miaka ya hivi karibuni, thamani hii imeonekana kuhatarishwa

zaidi kutokana na uharibifu wa mazingira hususan uharibifu wa misitu, ndio maana katika Sura ya Nne tuliangazia na kuchunguza habari zilizo katika nakala hiyo ya Kiingereza pamoja na tafsiri yake ya Kiswahili. Kitabu chenyewe kina sura kumi na mbili na kurasa 108, kila sura ikiwa ni mchango wa mtaalam tofauti na kuzungumzia mambo na mbinu mbali mbali katika hatua za ukuzaji miti. Sura zenye zing vichwa vifuatavyo:

Katika Sura ya 1, maelezo ya faida au umuhimu wa miti umetolewa. Hapa wajibu wa miti katika maisha, mashambani, katika uchumi na mazingira yameelezwa kwa fasili pamoja na kutolewa hitimisho linalohimiza wajibu wa miti na kuonya kuhusu hatari za ukataji miti. Sura ya 2 ni maelezo ya maeneo ya mashambani ambapo miti inaweza kupandwa na aina ya miti yenye manufaa imetajwa, pamoja na michoro na majina chini yao, michoro mwafaka inayomwezesha msomaji kutambua aina ya miti inapatikana pia katika sura nyingine.

Sura ya 3 inahusu mbegu za miti ni muhimu katika upandaji wa miti na hilo ndilo lengo la mafunzo ya ukusanyaji, utunzaji, upimaji wa ubora, uhifadhi na kutibu mbegu yametolewa kwa njia nzuri. Sura ya 4 nayo inahusika na miche ambapo maarifa kuhusu uanzilishaji, uotaji na ukuzaji wa bustani yameorodheshwa. Sura ya 5 inatoa maelezo ya ulinzi wa bustani la miche kutokana na visumbufu hasa wadudu na magonjwa mbalimbali ya miche na katika sura ya 6, ufafanuzi wa usimamizi wa kitalumiche na wajibu wa mnyapara wa bustani umetolewa. Katika sura ya 7, maelezo ya usimamizi wa kila siku ya kazi, orodha ya wafanyi kazi, mambo ambayo yanasaidia kupanga kazi na kubashiri shughuli zitakazohitajika mwaka unaofuata yametolewa. Sura ya 8 ni sehemu muhimu sana ya kitabu hiki kwani ndiyo inayompa msomaji ujuzi wa mbinu za upandaji na utunzaji. Jambo tunalohitaji kutanabahi hapa ni kuwa, licha ya hali na changamoto zisababishwazo na hali ngumu ya hewa, udongo, na wanyama wasumbufu kuangamiza miche iliyohamishwa, maarifa duni ya utunzaji ndicho kisababishi kikubwa cha kuangamia kwa miche. Muhtasari wa mambo mawili muhimu; miti ya matunda iliyopendekezwa na mbinu za uzalishaji wa matunda husika umetolewa katika sura ya 9. Hii ni kwa sababu mazao yao ambayo ni matunda yanaweza kumpa mkulima mapato kifedha tena ni chakula bora cha aina ya vitamini. Mifano ya miti ya matunda iliyopendekezwa hapa (miembe, mipapai na michungwa), jinsi ya kupanda na wadudu wasumbufu kwa kila mojawapo ndiyo ujumbe usiopimika wa sura hii. Sura ya 10 imetoa maagizo yanayohusu kupandikiza na kuchipua miti kama mbinu zilizoelezwa katika sura hii pamoja na sababu za

kupandikiza, kilimomseto kimetolewa kama mbinu inayojumuisha mimea na misitu katika shamba moja. Wakati huo huo, mifugo pia hutunzwa pamoja na hii misitu na mimea. Sura ya 11 na Sura ya 12, zinatoa ufafanuzi kuhusu mitindo mbalimbali ya mbinu hii pamoja na faida zake na kuzugumzia uhifadhi wa udongo, visababishi vya mmomnyoko wa udongo na jinsi ya kukabiliana navyo.

Kitabu chenyewe (MC), ni kichochezi na ni kama safari ya kiakili, michakato yenyewe ikielezwa hatua kwa hatua

### **1.9.2 Uteuzi wa sampuli**

Utafiti huu umetumia kitabu cha Kiingereza cha "*Social Forestry Techniques*" na tafsiri yake iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili "*Mbinu za Utunzaji wa Miti katika Misitu ya Jamii*". Vitabu hivyo viwili vimeteuliwa kupitia uteuzi makusudi (Neuman, 1997). Aina hii ya uteuzi ina uwezo wa kuchagua kitu kimoja, hasa kitabu, miongoni mwa vingine. Hii itawezesha ulengaji na udhibiti wa taaluma mahsusi. Patton (2002) pia anaeleza kwamba uteuzi wa kimakusudi unatumiwa kwa sababu ya kuaminika na kusadikika kwa data wala si kwa sababu ya usimamiaji au ujumuishaji. Anaongezea kuwa uteuzi makusudi hutumiwa kuchagua palipo na data nyingi mwafaka kwa utafiti husika.

### **1.9.3 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data**

Kwa kuchambua vitabu viwili: "*Social Forestry Techniques*" na tafsiri yake, maneno, virai na sentensi zilikusanywa. Uchambuzi ulifanywa kwa kutumia mwongozo ulioundwa. Mwongozo ulihusu ubanaji, uzidishaji, upotoshaji, upotezaji wa habari na istilahi za elimumisitu (EM), masuala ibuka yalioyojumuisha msamiati ambao haukutafsiriwa pia yaliongezwa. Data zilikusanywa, kuchanganuliwa na kuwasilishwa katika Sura ya 4. Matokeo yalijadiliwa na mapendekezo kutolewa katika Sura ya 5 ya utafiti huu.

### **1.10 Hitimisho**

Katika sehemu hii tulifafanua njia ambazo zimetumika kuteua, kukusanya na kuchanganua data katika kitabu cha "*Social Forestry Techniques*" zilizohawilishwa hadi tafsiri yake; "*Mbinu za Utunzaji Miti katika Misitu ya Jamii*". Tumeleza nakala hizi mbili kama eneo la utafiti. Njia zenyewe zilitumiwa kuelekeza kutathminiwa kwa vipengele vinne vya mchakato wa tafsiri; ubanaji,

uzidishaj, upotoshaji na upotezaj, vinavyoweza kushawishi kiasi cha habari, pamoja na dhana na istilahi za EM zinazoweza kufanikisha tafsiri hii ya kusudi. Pamoja na hayo, masuala yaliyo ibuka, msamiati ambao haukutafsiriwa ndio haukuweza kupuuzwa. Matokeo ya mbinu hizi yalijadiliwa kwa fasili katika sura ya nne.

## **SURA YA PILI**

### **VIPENGELE AMILIFU VYA TAFSIRI**

#### **2.1 Utangulizi**

Katika sura hii, tafsiri yenye kusudi imechunguzwa ikihusishwa na vipengele vya mchakato wa tafsiri kama; ubanaji, uzidishaji, upotezaji na upotoshaji, nafasi ya msamiati na istilahi za kitaaluma kwa minajili ya kuzihusisha na muktadha wa MC na kiasi cha habari kinachofikia msomaji katika ML. Katika kazi hii, uchunguzi uliofanywa pia unachangia kuimarisha mbinu za uchanganuzi katika sura ya tatu na nne.

#### **2.2 Dhana ya Tafsiri**

Taaluma ya tafsiri imekua kwa kasi kikubwa. Dhana za taaluma mbalimbali kutoka enzi za kale hadi sasa zimeweza kutufikia kwa njia ya tafsiri. Newmark (1988) anaeleza kuwa tafsiri ni uhawilishaji wa maana kutoka lugha moja hadi nyingine, kwani kutafsiri ni kutoa maana ya matini katika hali ambayo mwandishi alikusudia. Shughuli ya tafsiri inaweza kumakinika kwa kuzingatia mambo mawili; jambo la kwanza ni kwamba matini inayoshughulikiwa lazima iwe katika maandishi, na pili, matini ya LC na LL japo kila mara huwa na matarajio ya kudhihirisha ulinganifu si lazima zilingane moja kwa moja. Kwa misingi hii, Catford (1965) asema kuwa, mawazo katika tafsiri ni mawazo yanayolingana na wala si mawazo yaliyo sawa. Hii inatokana na ukweli kuwa tofauti za kiisimu, kitamaduni, kihistoria na kimazingira kati ya lugha hufanya iwe vigumu kutafsiri mawazo ya lugha moja bila kupoteza, kupotosha au kubadili maana hata kama ni kwa kiwango kimoja tu. Anaendeleza hoja kwamba, mradi mkubwa alionao mtafsiri ni kujaribu kuleta ulinganifu mzuri kati ya MC na ML na kusudi la tafsiri licha ya tofauti zisizoepukwa.

Anavyoeleza Njenga (2014) tafsiri ni mchakato wa kuhamisha ujumbe ulioandikwa katika LC hadi katika ujumbe ulioandikwa katika LL kwa lengo la kutimiza ulinganifu wa maana. Ulinganifu huu pia unaweza kuzingatiwa katika kiwango cha umbo na pia uamilifu wa MC na ML. Ikiwa kuna uhusiano kamili wa umbo na uamilifu wa MC na ML, maana inayojitokeza itakuwa sahihi. Kama umbo tu ndilo lina uhusiano na hakuna uhusiano wa uamilifu basi maana itakuwa tata. Uhusiano wa uamilifu ukiwepo na umbo lisiwe muhimu, basi maana itakuwa sahihi. Ikiwa hakuna uhusiano

wowote wa umbo na uamilifu wa LC na LL, hakutakuwa na maana yoyote; yaani hakuna tafsiri iliyofanyika.

### **2.3 Dhima ya Tafsiri**

Newmark (1988) anatoa maelezo kuwa tafsiri hutimiza majukumu kama vile, tafsiri hutumika kwenye vyombo vya habari. Tafsiri pia ni njia ya mawasiliano kwani hutumika kama njia ya kuwasiliana miongoni mwa mataifa mbalimbali. Hutumiwa kutolea maelezo ya biashara, kama maelekezo ya jinsi ya kutumia bidhaa zinazouzwa nchi za nje. Anasema kuwa ni muhimu tafsiri zifanywe kwa usahihi ili kufanikisha mawasiliano. Tafsiri ni nyenzo ya kueneza tamaduni za mataifa mbalimbali kwa mfano utamaduni wa Kirumi uliathiriwa sana na utamaduni wa Kiyunani kutokana na tafsiri. Newmark anaendelea kusema kuwa tafsiri huwa kama mbinu ya kujifunza lugha. Mazoezi ya kutafsiri humfanya mtu asome kwa undani na makini zaidi vipengele vingi vya kiisimu vya lugha anayotafsiri ili aweze kutoa tafsiri nzuri inayokubalika. Tafsiri huwa kama kiliwazo cha nafsi kwa mtafsiri. Tafsiri humburudisha na kuridhisha nafsi ya mtafsiri kadri anavyotatua matatizo yake ya kitafsiri. Tafsiri pia ni mbinu ya kuhamisha maarifa na ujuzi. Maarifa kote duniani hugunduliwa na jamii moja halafu kuhamishwa kwa jamii nyingine kupitia tafsiri.

### **2.4 Nadharia za Tafsiri**

Nadharia za tafsiri ni maelekezo ya vipengele mbalimbali vya tafsiri vinavyopaswa kuzingatiwa katika kazi ya kutafsiri. Nadharia hizi huchunguza na kutoa mbinu zinazofaa kutumika katika kazi ya tafsiri. Catford (1965) anaeleza kuwa dhima muhimu ya nadharia za tafsiri ni kuonyesha mbinu za tafsiri zinazofaa kutumiwa kufasiri aina mbalimbali na tofauti tofauti za matini. Nadharia hutoa msingi, sheria na vidokezo vya kutafsiri matini na kuhakiki tafsiri, yaani matini ambazo zimekwisha tafsiriwa. Kulingana na Catford, sababu zilizopelekea kuanzishwa kwa nadharia za tafsiri ni; wingi wa makosa katika tafsiri ambazo tayari zimechapishwa. Ni nadra kupata tafsiri ambazo hazina makosa. Pili ni kuwepo kwa idadi kubwa na inayoendelea kuongezeka ya asasi zinazojishughulisha na kazi ya tafsiri. Tatu, mfumko wa istilahi katika taaluma mbali mbali hasa za sayansi na teknolojia na vilevile haja ya kuzisanifisha ili kuwezesha tafsiri kati ya lugha na nyingine kufanyika kwa ufanisi zaidi. Kazi hii ilichunguza, miongoni mwa mambo mengine, istilahi zinazoibuka katika uwanja huu wa EM.

Nadharia hushughulikia mambo yafuatayo katika mpangilio wake; kubaini na kufasili tatizo la tafsiri, ikiwa hakuna tatizo la tafsiri, basi hakuna nadharia ya tafsiri. Pili ni kuonyesha vipengele vyote vinavyopaswa kuzingatiwa katika kutatua tatizo la tafsiri lililobainishwa. Kisha kuorodhesha njia zote zinazowezekana kufanikisha tafsiri husika. Mwisho ni kupendekeza hatua zinazofaa zaidi kutekeleza zoezi la tafsiri ikiwemo mbinu mwafaka zaidi kwa matini mahususi inayoangaziwa. Kunazo nadharia kadhaa za tafsiri. Utafiti huu utaongozwa na nadharia ya Kusudio (Vermeer, 1978). Nadharia hii huchukulia kwamba tafsiri hufanywa kwa kusudi fulani. Kitabu cha "*Social Forestry Techniques*" kilitafsiriwa katika Kiswahili na kuwa "*Mbinu za Utunzaji wa Miti katika Misitu ya Jamii*" kwa nia ya kupanua kuhamasisha uelewa wa masuala ya uhifadhi wa mazingira kwa hadhira pana. Yaani iweze kuwafikia wananchi anuwai ili waweze kujua namna na jinsi ya kuhifadhi na kutunza miti.

## **2.5 Habari Zilizobanwa**

Ubanaji unaweza kuelezwa kama kitendo cha kupunguza ukubwa wa kitu au kukifupisha, unaweza kuwa mchakato wa kuwa mdogo au kilichofinywa kwa juzuu, wingi au upeo. Huu ni mchakato ambamo maneno, virai na sentensi, na sehemu nyingine linganifu hudondoshwa ili kupata uamilifu wa MC kama juhudi za kutosheleza mahitaji ya wapokezi wanaolengwa. Ni mbinu ambayo ni ya kimaksudi na inayopewa motisha katika taaluma mbali mbali ili kutekeleza majukumu maalum. Ili kufaulu katika kupata tafsiri zinazokubalika katika tamaduni lengwa, mtafsiri huwa hana budi kubana baadhi ya hoja. Hapa ubanaji huwa ni mbinu hasa katika mchakato wa tafsiri na sio makosa. Madhumuni mengine huwa ni kuepuka kuibua maana zisizo za kawaida (Nida, 1964).

Ubanaji huhitajika mahali ambapo athari fulani inahitajika katika wapokezi wa ML, sababu nyingine ya udondoshaji huu ni; kuwasilisha habari muhimu pekee kati ya habari nyingi zisizohitajika, kuwasilisha habari nyingi kwa maneno machache, iktisadi ya maneno, kuhakikisha kukubalika kwa msamiati na istilahi za kitaaluma na uepukaji wa vikwazo vya kiwakati, kimawanda na kiutamaduni. Ubanaji hutokea iwapo; hapana msamiati wa kutosha ama kabadala chake, istilahi za kitaaluma ambazo zimetumika katika MC na hazina visawe katika ML, au pana mgongano wa kitamaduni kati ya LC na LL. Mtafsiri huwa hana budi kutumia ubanaji iwapo hapana ulinganifu wa habari katika LL na hivyo kushindwa kuziandika upya. Maneno huenda pia yakakosa tafsiri zinazolingana, ikawa mtafsiri hana budi kuyaacha na hatima ikawa ubanaji. Matokeo ni kuwa

anayesoma MC hupata ujumbe kwa njia tofauti na anayesoma ML, maoni yanayolingana na ya Ahmed (2016).

Ni maoni potovu kuwa ubanaji hupotosha au kupunguza uzito wa maana, kwani haya yamechunguzwa katika kazi hii kama mikakati maalum ya kutekeleza majukumu fulani. Ubanaji pia ni suluhisho la kukwepa uelekezaji mbovu wa msomaji. Matini chanzi katika kazi hii inatokana na nakala ya Kiingereza “*Social Forestry Techniques*” ambayo inachunguzwa iwapo ina maneno na istilahi za kigeni ambazo zimechujwa, kuachwa nje au vibadala vyao kutumiwa na hivyo kuleta ubanaji wa habari. Mfano wa ubanaji;

**Kiingereza:**

‘before sedentary agriculture started, wild plants including trees had given people a large percentage of their diet such as fruits and nuts’ (pg. 8).

**Kiswahili:**

‘kabla ya kilimo cha sasa kuanza, mimea ya pori ikiwa pamoja na miti ilitokea kuwa ndicho chakula cha babu zetu’ (uk. 8).

Katika mfano huu, maneno ‘*sedentary*’ na ‘*percentage*’ hayakutafsiriwa moja kwa moja, watafsiri wangetumia maneno kama ‘*kukaa mahali pamoja*’ na ‘*asilimia*’, ili kuibua tafsiri kama “*kabla ya kuasisiwa kwa kilimo cha kusalia mahali pamoja, mimea mwitu ikijumuisha miti iliwapa watu asilimia kubwa ya mlo wao kama vile matunda na kokwa*” dhana ambazo huenda zisieleweke na wapokezi wanaolengwa kwa namna inayotarajiwa. Mtafsiri anastahili kulenga uwasilishaji wa dhana za MC zinazotaribu kulingana na istilahi sawia katika ML, lakini katika nadharia ya ‘Skopos’ habari zenyewe katika matini lengwa ziwe zinatoshwa tu yaani ziwe na kiasi fulani cha uaminifu kwa matini asilia na ziweze kutosheleza kuasisi au kubainisha kusudio. Ubanaji unaweza kutumiwa iwapo matini imejaa istilahi za kisayansi na kiufundi ili kuweka mambo bayana kwa wapokezi fulani wanolengwa. Ubanaji umechunguzwa pia kwa minajili ya kuonyesha manufaa yake katika kupitisha ujumbe unaohusu upandaji na utunzaji wa miti. Hali za kawaida zinazozua ubanaji hazijahimizwa sana katika kazi hii isipokuwa kutajwa tu.

## 2.6 Habari Zilizozidishwa

Uzidishaji unahusu matumizi ya maneno, virai, istilahi na hata sentensi kwa kuzipanua katika ML kuliko namna ambavyo imetokea katika MC. Hii ina maana kuwa, sifa za kisintaksia na kileksika za lugha huenda zikawa chanzo cha uzidishaji. Katika kuhamisha habari kutoka MC hadi ML lazima elementi ya kisemantiki izingatiwe. Iwapo ujumbe umejitokeza katika ML na haupo kwenye MC, basi ujumbe huo umeongezwa au kuzidishwa. Matumizi ya masmiati na istilahi za kitaaluma na miundo mbalimbali ya sentensi zinaweza kuzua uzidishaji usioweza kuepukika. Uzidishaji pia hutokea wakati ambapo maelezo au ufafanuzi zaidi na ujumulishaji wa habari unatolewa na katika kutoa mahusiano hasa za kimsingi baina ya hoja, habari huongezwa. Uzidishaji ni mojawapo wa mikakati itumiwayo na watafsiri kuleta uelewa wa ML na wapokezi wanaolengwa. Lugha mahsusi inaweza kuhitaji maneno mengi zaidi ya lugha nyingine kuelezea dhana ile ile, mfano mmoja wa sentensi iliyotafsiriwa kutoka katika kitabu cha “Social Forestry Techniques” hadi katika nakala ya Kiswahili; *‘Mbinu za Utunzaji Miti katika Misitu ya Jamii’* ni:

### **Kiingereza:**

'This is probably the most common tree for charcoal making in dry areas in Kenya' (pg. 15).

### **Kiswahili:**

'Aina hii ya miti aghalabu hupatikana kwa wingi katika zile sehemu kavu za Kenya na ni mashuhuri kwa uchomaji wa makaa (uk. 16).

Sentesi hii katika Kiingereza ina maneno 15 ilhali katika Kiswahili imetafsiriwa kwa maneno 21, kuna maneno 6 ya ziada. Huu ni uzidishaji kwani, kama watafsiri wangesema: 'Pengine mti huu ndio unaopatikana kwa wingi kwa uchomaji makaa katika maeneo kame ya Kenya', haingezua uzidishaji wa kiwango hicho cha maneno 6. Kwa kawaida, uzidishaji unazua tafsiri ya mzunguko ambayo inaweza kuashiria uwezo wa mtafsiri kutokuwa na ustadi wa kutumia maneno au istilahi za moja kwa moja.

Katika kazi hii tumejaribu kuthibitisha kiasi cha uzidishaji katika tafsiri huku tukihusisha na nadharia ya 'Skopos' ambapo tafsiri hufanywa kwa kusudi fulani. Maandishi yanayorudiwa, kama katika tafsiri hujaribu kuleta athari fulani kwa kufanya dhana zieleweke kwa njia fulani. Dhana na maagizo yakieleweka kwa njia maalum iliyonuiwa mambo mahsusi yatatekelezwa katika kikundi

fulani cha watu. Utekelezaji huu ukifaulu basi kusudi lililolengwa litaweza kuimarisha hali fulani, kwa mfano, katika muktadha wa kazi hii, ukuzaji miti kwa minajili ya kuhifadhi mazingira.

## **2.7 Habari Zilizopotezwa**

Upotezaji unahusu kutojumuishwa kwa habari fulani katika ML ilhali habari husika zinapatikana katika MC. Habari zikipokelewa na kutafsiriwa kwa njia isiyo kamilifu, basi kiasi fulani cha habari hupotea. Maneno, virai na sentensi zikibadilishwa au kufafanuliwa kwa njia isiyobeba habari zote kutoka MC hadi ML upotezaji hutokea. Upotezaji unaweza kuathiri kusudi la tafsiri kwa njia chanya au hasi. Kupotea kwa habari mahususi huchangiwa na mambo tofauti tofauti, kama vile zile habari ambazo zinaweza kuepukika na zisizoweza kuepukika. Hoja zinazochangia upotezaji huu hutokana na; tofauti za kitaaluma, tofauti za mazingira ya lugha asilia na lugha lengwa, ubunifu mwingi katika mchakato wa kutafsiri zaidi ya mahitaji katika MC, na matumizi ya vabadala vya maneno fulani.

Viwango vya upotezaji vinaweza kuangaliwa kiisimu, yaani kimofolojia na kisintaksia. Kimofolojia kila lugha ina maneno yake mahsus ambayo hutumika kurejelea vitu mbalimbali, ambapo inaweza kutokea kwamba lugha moja ina msamiati mpana katika eneo fulani hivi kwamba visawe vya msamiati huo havipatikani katika lugha nyingine. Hali hii inakuwa changamano zaidi ikiwa lugha asilia imeendelea zaidi kiteknolojia na kitaaluma kuliko lugha lengwa. Katika hali kama hii upotezaji huweza kutokea. Kisintaksia, kila lugha ina muundo wake wa kisarufi unaokubalika. Namna ambavyo lugha mbili zinazohusika katika tafsiri hutofautiana kimuundo na kiuamilifu ni chanzo kinachoathiri kiasi cha habari zinazopitishwa katika tafsiri kutoka matini chanzi hadi matini lengwa. Kwa mfano; katika nakala ya Kiingereza “*Social Forestry Techniques*”, imeelezwa, na kutasiriwa ifuatavyo:

### **Kiingereza:**

‘This is a well known agroforestry species’ (pg. 14).

### **Kiswahili:**

‘Hii ni aina ya miti inayojulikana sana katika kilimo cha mimea na misitu...’ (uk. 16).

Nomino ‘miti’, limetumiwa katika ML ilhali halipo katika MC. Istilahi ‘*species*’ na ‘*agroforestry*’ ni istilahi za kitaaluma na lazima zitafutiwe visawe vinavyoafiki, kama vile: ‘*species*’ (spishi), na ‘*agroforestry*’ (kilimomseto), (Nshubemuki na wenzake, 1999). Katika hali kama hizi mtafsiri

anatarajiwa kuwa mbunifu kwa kutumia mbinu kama vile utohozi na mikopo ya msamiati wa kitaaluma hata kama msamiati huo haujapata ukubalifu mkubwa. Kwa kufanya hivi kiasi kikubwa cha habari zinazoweza kupotezwa kinazuiwa. Ili kuepukana na upotezaji wa habari ambazo ni muhimu au za kimsingi katika matini inayotafsiriwa, mtafsiri lazima azingatie mada, taaluma na muktadha ambamo lugha asilia imetumiwa, asipofanya hivyo huenda asilete fahiwa inayotarajiwa katika ML. Katika kuelewa muundo wa lugha kifonolojia, kimofolojia na kisarufi, mtafsiri ataepukana na tafsiri sisisi ambayo haizingatii muktadha na fahiwa ya tafsiri husika (Mutie, 1997; Kihore, 2005). Tafsiri sisisi haipendekezwi katika utafiti huu bali ni tafsiri inayotumia hali hii ya upotezaji kutosheleza mahitaji ya wapokezi wa ML ndiyo mojawapo wa vipengele vinavyochunguzwa.

## **2.8 Habari Zilizopotoshwa**

Kupotosha ni kule kuibua tafsiri isiyo sahihi katika matini lengwa ikilinganishwa na uhalisi wa matini chanzi. Katika muktadha ya tafsiri ni kule kuibua tafsiri isiyo sahihi kwa maana kwamba habari au tafsiri nzima kwa jumla katika matini lengwa inatofautiana kimaana na kiuamilifu na maana iliyokuwa imekezwa katika MC. Hoja zikiwasilishwa kwa njia isiyo ya kweli basi husemekana kuwa zimepotoshwa. Kubadilika kwa ukweli kidogo ni jambo lisiloweza kuepukika katika tafsiri. Ugumu wa tafsiri ni kuwa haiwezi kuchukuliwa tu kama zoezi la kulinganisha maneno na visawe vyao, bali ni kupata vikundi vya maneno vinavyokaribiana kimaana bila kuzua utata. Huenda habari zikibanwa au kuzidishwa kupita kiasi kinachohitajika zinaweza kuzua upotoshaji.

Upotoshaji wa habari pia hutokea pale ambapo kuna ukosefu wa msamiati au hapana istilahi za kitaaluma za kutosha. Upotoshaji unaweza kutokea kwa sababu ya tofauti za miundo ya lugha na tamaduni, hali ambayo husababisha kukatizwa kwa mawasiliano (Mwangi, 2016). Upotoshaji pia hutokea pale ambapo pana uibushaji wa uelewa mbadala au hata kinzani, au pale ambapo mtafsiri ana udhibiti duni wa mada inayotafsiriwa. Tofauti za kisemantiki, kiisimu na kitamaduni zinaweza kusababisha ukosefu wa ushikamano wa maana ya ujumbe unaojitokeza (Jilala, 2017), hali ambayo inajulikana kama upotoshaji. Sababu nyingine isababishayo upotoshaji ni kuwa mwandishi wa MC na mwandishi wa ML huwa na mitindo tofauti ya matumizi lugha kwani chukulizi zao ni tofauti kuhusu maana ya maneno, viwango vya maneno na hata tajriba zao kuhusiana na mada au taaluma mahususi. Lugha ya kitaaluma inatofautiana katika taaluma mbali mbali na kawaida yao ni kuwa na

msamiati na istilahi maalum kwa kila rejista. Inabidi mtafsiri awe na ujuzi wa istilahi hizi ili aweze kuzielewa na kujaribu kuzitafsiri. Tafsiri mbaya zinaweza kuhusishwa na ukosefu wa mawasiliano bora au upotoshaji wa mawasiliano (Ali, 1981). Ujumbe katika tafsiri ukiathiriwa huenda wasomaji wa ML wakakosa ujumbe unaopatikana katika MC. Athari hii, tofauti na inavyoaminiwa kuwa inapotosha, inaweza kukidhi mahitaji fulani (Ahmed, 2016; Muzaffar na Behera, 2017). Hata hivyo, nia ya mtafsiri lazima iafikiane na kusudi la tafsiri (Kamau, 2008).

Changamoto kwa mtafsiri ni kuwa LC na LL hutofautiana kileksika, kisarufi na katika mfumo wa sauti au kifonolojia. Lugha asilia mara nyingi huwa na hali ambazo ni ngeni kwa mazingira ya lugha ya pili, hali ambayo inaweza kusababisha upotoshaji wa habari, mada na hata tafsiri nzima kwa jumla. Ufuato ni mfano wa upotoshaji kutoka katika tafsiri ya kitabu kinachochunguzwa katika utafiti huu;

**Kiingereza:**

‘the disadvantage is that the collectors prefer easily climbable trees, which may not be desirable’ (pg. 30).

**Kiswahili:**

‘madhara ni kwamba wanaokusanya mbegu hupanda miti ambayo ni rahisi kupanda na ambayo labda haina mbegu nzuri (uk. 31).

Katika mfano huu, watafsiri wamekwepa kutafsiri maneno: ‘*prefer*’ na ‘*desirable*’ ambayo yangeweza kutafsiriwa kama ‘pendelea’ na ‘faa zaidi, tamanika’ ili kuibua tafsiri kama “hitilafu iliyoko ni kwamba wakusanyaji hupendelea miti inayopandika kwa urahisi, jambo ambalo huenda lisiwe la kutamanika”. Hatimaye habari zikipotoshwa zitakosa kuimarisha kusudi la tafsiri na mawasiliano kwa wapokezi kwa jumla. Katika kazi hii athari ya vipengele vitatu vya kwanza; ubanaji, uzidishaji na upotezaji, vinatathminiwa pamoja na upotoshaji katika ML na kusudi lake. Ili kufanikisha kusudi la tafsiri husika watafsiri hawana budi kuimarisha uwezo wa kuelewa lugha asilia pamoja na LL, na kuwa na umilisi katika lugha hizi mbili kitaaluma na kufanya utafiti kuhusu istilahi za kitaaluma.

## **2.9 Msamiati na Isitilahi za Elimumisitu**

Ili kufanikisha tafsiri zenye kusudi mahususi kama vile uhamasishaji wa juhudi za utunzaji misitu, mikakati maalum inayohusiana na ukopaji, utohozi na ubunaji inahitajika. Mikakati inayoupatia ubunaji kipaumbele itawezesha sekta ya misitu kutumia lugha yetu ya taifa ili kuwafikia wananchi kwa urahisi. Hii inamaanisha kuwa kuna haja ya ubunaji ambao utaendeleza Kiswahili hasa katika taaluma na viwango mbalimbali. Ni wazi kuwa tafsiri za kitaaluma haziwezi kufanyika kwa ufanisi pasi na ubunaji wa msamiati na istilahi maalum. Hivi ni kusema kwamba ung'amuzi wa msamiati na istilahi za elimumisitu (Nshubemuki na wenzake, 1999) utakuwa kiunganishi muhimu cha kukivusha Kiswahili kutoka katika matumizi ya kawaida kwenda katika matumizi ya kitaaluma.

Tafsiri katika taaluma zitafanikishwa kwa uelewa muruwa wa lugha asilia na LL na hoja za taaluma husika. Istilahi za kitaaluma na visawe vyake vimepatikana kwa kurejelea machapisho mbalimbali ya istilahi sanifu za Kiswahili, kurejelea nakala zilizoandikwa na waundaji istilahi na kushauriana na wataalam anuwai wa misitu na elimumisitu. Changamoto katika mbinu hizo zimekuwa uhaba wa machapisho hayo na visawe vya istilahi kwa Kiswahili, matatizo ambayo yananiwa kusuluhishwa na kazi hii japo kwa kiwango kidogo.

Kimsingi utafiti huu unapendekeza tangu awali kwamba ili kuweza kufanikisha uhamasishaji wa masuala ya utunzaji misitu na mazingira kwa jumla, kuna haja ya kupanua maarifa ya elimumisitu na mazingira kwa ujumla ili kuweza kufikia jamii pana. Maarifa hayo yanaweza kujumuisha kubuniwa kwa istilahi na usambazaji wa istilahi hizi kupitia kwa tafsiri za aina hizi. Tafsiri hizi zinapaswa kuwa na zaidi ya matumizi mazuri ya maneno, mfanano wa istilahi na uibushaji wa maarifa yanayoweza kuenezwa kwa upana katika jamii. Ili kufanikisha tafsiri katika taaluma mahususi kama hii ya utunzaji misitu, inahitajika kuwepo kwa uelewa wa lugha, ufahamu wa kina wa tamaduni zinazohusika, usasa wa kitaaluma na kisera na jamii ambamo maamuzi husika yanafanywa. Mtafsiri wa matini za elimumisitu na mazingira lazima awe na msingi wa uelewa wa dhana za kisayansi na vilevile uelewa wa muktadha wa ulimwengu halisi ambamo sayansi hujibainisha. Mtafsiri huyo anapaswa kuwa amaeishi katika zaidi ya tamaduni mbili, awe na mafunzo na tajriba katika sayansi ya mazingira kwani hili huzuia uundaji na uamuzi wa sera bila kutilia maanani miktadha ya kitamaduni (Jackson na wenzake, 2017).

Haja ya kueneza maarifa kuhusu mazingira ulimwenguni kote imezua uvumbuzi wa aina mbalimbali kama vile uvumbuzi wa vifaa vya kutafsiria istilahi za taaluma ya mazingira na elimumisitu (Abranyi, 2016). Vifaa hivi, kwa mfano programu za mtandao, vinaendelea kuwa hitaji kuu katika orodha ya tajriba na uwezo wa mtafsiri yeyote yule wa taaluma hii. Vifaa hivi vinavumbuliwa ili kuokoa muda wa kutafsiri na kuu zaidi ni kuibua tafsiri inayoweza kuaminika, kuthibitika na kutegemewa. Hata hivyo, mtafsiri anastahili kutumia vifaa hivi kwa tahadhari ili kujiepusha na upotoshaji. Utaaluma wa mtafsiri, umilisi na tajriba ni maswala muhimu yanayopaswa kuzingatiwa na mtu yeyote yule anayefanya kazi katikati ya lugha na tamaduni mbali mbali. Unahitajika umilisi mkubwa kuhamisha dhana, istilahi na maana mbalimbali za mazingira na elimumisitu kutoka lugha moja hadi nyingine kwa kutegemea utamaduni mmoja na mwingine (Carmen, 2014). Tafsiri za istilahi za kisayansi zinazohusiana na mazingira, elimumisitu na binadamu huandamwa na changamoto na matatizo mbalimbali. Hivyo basi utafiti huu unachangia kuweza kupitisha maarifa juu ya nafasi ya tafsiri katika kuendeleza taaluma ya mazingira. Utafiti huu pia unachangia suluhu kwa matatizo yanayokumba tafsiri ya istilahi na ujumbe unaohusu masuala ya mazingira na binadamu. Msamiati na istilahi za elimumisitu (Nshubemuki na wenzake, 1999) ni sehemu muhimu ya vipengele vya tafsiri yenye kusudi, dhana iliyotafitiwa katika kazi hii. Katika utafiti huu msamiati na istilahi za elimumisitu zinatathminiwa ili ziweze kuchangia katika uchanganuzi wa data kutoka katika chapisho "*Mbinu za Utunzaji wa Miti katika Misitu ya Jamii*".

## **2.10 Hitimisho**

Vipengele vinavyozuliwa na mchakato wa tafsiri kama ubanaji, uzidishaji, upotoshaji na upotezaji ndivyo vinachunguzwa katika utafiti huu. Ubanaji, uzidishaji, upotezaji na upotoshaji ujumbe vinaonekana kujisimamia. Hata hivyo, vipengele hivi vinategemeana, yaani kila kimoja kinategemea kingine, hivi kwamba kimoja kinaweza kuathiri majukumu ya kingine kwa njia chanya au hasi na hivyo kuishia kuathiri kiasi cha habari katika ujumbe unaopitishwa katika mchakato wa kutafsiri. Ubanaji, uzidishaji na upotezaji ni vipengele vinavyoweza kusababisha upotoshaji. Msamiati na istilahi za elimumisitu ni viunganishi muhimu vya vipengele hivyo vinne katika kuimarisha kiasi cha habari katika tafsiri. Inabidi mtafsiri aimarishe umilisi wake katika misimbo za kitaaluma katika MC ili afaulu katika kutoa tafsiri yenye kusudi.

## SURA YA TATU

### VIPENGELE AMILIFU VYA TAFSIRI VINAVYOBANA NA KUZIDISHA HABARI

#### 3.1 Utangulizi

Katika sura hii tulichunguza na kuchanganua ili kubainisha mikakati ya tafsiri zilizotumika katika juhudi za kutekeleza na kufanikisha tafsiri yenye kusudi au malengo mahususi. Tafsiri yenyewe, "*Mbinu za Utunzaji Miti Katika Misitu ya Jamii*" ilichambuliwa ili kuthibitisha ubainikaji wa malengo haya. Malengo haya yaliegemea katika kushawishi kiasi cha habari kinachopitishwa katika mchakato wa kutafsiri kama inavyojitokeza katika toleo hili. Uchanganuzi ulifanywa iwapo kulikuwa na sababu nyingine ya ushawishi wa habari katika ML. Sehemu ya 3.2 uchambuzi na 3.3 mjadala wa matokeo yanazungumzia kuhusu kutokea kwa vipengele vya mchakato wa tafsiri.

#### 3.2 Uchambuzi wa Ubanaji na Uzidishaji

##### 3.2.1 Kuhusu ubanaji

##### Ubanaji S1

###### 1. Kiingereza:

‘Trees and their by-products are essential for rural life and have great economic value to rural households both directly and indirectly’ (pg. 9).

###### Kiswahili:

‘Miti na bidhaa ambazo hupatikana kutoka kwa miti ni vitu vya lazima katika maisha ya mashambani na wakati huo huo huwa ni muhimu kiuchumi katika uendelezaji wa maisha mashambani’ (pg. 11).

Katika mfano huu, mambo mengi kama vile maneno ‘*by-products, economic value, directly and indirectly*’ yamebanwa. Katika tafsiri ya aina hii, kilichobanwa si maneno au mafungu ya maneno tu bali pia, dhana, habari na maarifa yanayobebwa na maneno hayo. Hii ina maana kwamba mtafsiri anawajibikia hadhira lengwa ili kuiwezesha kupata ufahamu wa masuala kama; *by-products*—bidhaa ziada, *economic value*—thamani ya kiuchumi, *directly*—moja kwa moja, *indirectly*—sio ya moja kwa moja. Kwa hivyo kubanwa kwa mambo haya kumbana kiasi cha habari kinachopitishwa kutoka matini chanzi hadi ML.

## Ubanaji S2

### 1. Kiingereza:

This is a real multi-purpose tree, fast growing giving high yields of firewood and timber is also high quality for poles and construction (pg. 16).

### Kiswahili:

Mti huu una manufaa sana. Unakua kwa haraka hutoa kuni nzuri na mbao zake ni za hali ya juu sana kwa matumizi ya nguzo na mbao za ujenzi (uk. 17).

Kimsingi katika kifungu hiki habari inayowasilishwa inaangazia wingi wa manufaa ya mtu unaozungumziwa yakijumuisha ukuaji haraka, mazao mengi yanayojumuisha kuni, mbao, pamoja na boriti yaani nguzo za kujengea. Hata hivyo, katika mfano hapo juu una ubanaji kwani neno ‘*real*’ halikutafsiriwa ikiwa na maana kwamba ule msisitizo uliokusudiwa haujitokezi. Pengine mtafsiri angeanzisha sentensi kwa kusema; ‘Huu ni mti ambao kwa kweli una manufaa mengi’.

### 2. Kiingereza:

*Acacia nilotica* has similar characteristics and uses (pg. 15).

### Kiswahili:

*Acacia nilotica* una manufaa kama yale ya miti ya jamii iliyotajwa hapo juu (uk. 16).

Ubanaji umefanyika katika mfano 2 kwani maneno, ‘*characteristics and uses*’ yameachwa nje, hayakutafsiriwa. Neno ‘*characteristics*’ lingetokea kama sifa. Dhana inayokusudiwa na neno *characteristics* ingefikishwa katika ML kama ‘sifa mahsusi’. Ubanaji umetokea hapa kwani dhana ya ‘*uses*’ ndiyo imetafsiriwa kama sifa mahsusi. Ubanaji huu huenda ukawa umesababishwa na ukosefu wa ujuzi wa EM. Kwa misingi hii, kamusi inatosha kumpa maana na ujumbe wa msamiati husika. Kuna baadhi ya misamiati ambayo tayari kamusi zinatoa maana yake na inajulikana kwa jamii lengwa na jamii chanzi. Neno ‘*characteristics*’ ni neno la kawaida inayopatikana katika kamusi. Kwa hiyo mtafsiri hakuhitaji utafiti wowote ili kujua kisawe cha neno hilo katika Kiswahili. Hali hii inafanya hadhira kupata maana na ujumbe finyu kinyume na ilivyokusudiwa katika MC.

### 3. Kiingereza:

This tree is indigenous to tropical America (pg. 18).

### Kiswahili:

Mti huu ulitoka misitu ya Marekani (uk. 19).

Hapo katika mfano 3, ubanaji upo kwani maneno, ‘*Indigenous*’ na ‘*tropical*’ hayakushugulikiwa. Neno ‘*indigenous*’ linaweza kutafsiriwa kuwa “mti huu una wenyeji asilia wa sehemu za kitropiki za Marekani”. Kiswahili kinaruhusu neno ‘*tropical*’ kufanyiwa utohozi na kuibushwa katika Kiswahili kama –a kitropiki. Kwa hivyo, kuhusiana na uwasilishaji wa kiasi cha habari kinachohusu maarifa, uasilia wa miti hii haujafikishwa katika matini lengwa.

**4. Kiingereza:**

This tree is commonly found in home compounds and along streets planted for ornamental purpose (pg. 18).

**Kiswahili:**

Mti kwa kawaida hupatikana katika viwanja vya nyumbani na kwenye barabara za miji kwa minajili ya kutoa umaridadi (uk. 19).

Mfano huu wa 4, unaonyesha ubanaji kwani kitenzi ‘*planted*’ katikati ya maelezo ya mahali mti huo hupatikana unaonyesha kuwa mti huo unapandwa kwa minajili ya upambaji na urembeshaji wa mahali. Neno lenyewe likidondolewa na kuachwa kwenye MC tafsiri haidhihirishi maana hii. Kimsingi inaonekana kwamba huu ni udhaifu wa mtafsiri kwani haya ni maelezo ya moja kwa moja yanayoweza kufikishwa katika lugha lengwa bila shida—“Mti huu kwa kawaida hupatikana katika nyua za nyumba na hupandwa kwenye barabara za miji kwa ajili ya urembeshaji”. Kwa hivyo habari zinazohusiana na mahali pa upanzi wa mtu huu zinabanwa na hazifiki katika ML.

**5. Kiingereza:**

*Leucaena leucocephala*, this is also a tree from Central America but nowadays widely introduced into the tropics all over the world (pg. 21).

**Kiswahili:**

Mti huu ulitolewa Marekani ya kati lakini siku hizi unakuzwa katika maeneo yote ya joto duniani (uk. 22).

Katika mfano 5, maneno ‘*also*’ na ‘*introduced*’ hayakutafsiriwa, na hii imezua maana tofauti. Neno ‘*also*’ lingetafsiriwa, sentensi hiyo ingekuwa, ‘Huu pia ni mti uliotoka Marekani ya kati’. Vile vile neno ‘*introduced*’ likiachwa inaonekana kama mti huu umekuwa tu, na sio kuwa ndipo unaanza kukuzwa katika maeneo yote ya joto. Hata hivyo maneno ‘*also*’ na ‘*introduced*’ maneno ya kawaida ambayo hayahitaji utafiti wowote.

## **6. Kiingereza:**

This is known as a fast growing tree but only under suitable conditions and it does not grow well in areas with drought (pg. 21).

## **Kiswahili:**

Mti huu hukua upesi ikiwa hali ya hewa ni nzuri na haiwezi kuwa vizuri katika maeneo ambayo kiangazi huweko (uk. 22).

Mfano wa 6, pia ni mfano wa ubanaji kwani ‘*this is known as a fast growing tree*’ inastahili kuwa ‘mti huu unajulikana kwa ukuaji upesi’. Sentensi kama hii inadhihirisha udhaifu wa mtafsiri ikitiliwa maanani kwamba haina dhana wala istilahi za kitaaluma ambazo zingeweza kuangaliwa kama kikwazo. Mtafsiri anatumia mbinu ya mzunguko hata pale ambapo tafsiri husika inaweza kujitokeza moja kwa moja. “Mtu huu unajulikana kama mti unaokua upesi ila tu katika hali zilizo nzuri na ukuaji wake haufanyi vizuri katika maeneo yaliyo na hali za kiangazi”. Hii inadhihirisha kwamba ubanaji hautokani tu na ukosefu wa istilahi sawia katika lugha LL, maana wakati mwingine ubanaji ni matokeo ya kushindwa kwa mtafsiri kudhibiti matini anayoitafsiri.

## **Ubanaji S3**

### **1. Kiingereza:**

There is a limit of the length to which long-handled tools can be used for collecting seed (pg. 29).

### **Kiswahili:**

Kuna kiwango ambacho vifaa vya kutoa mbegu vinaweza kutumiwa (uk. 31).

Katika mfano wa 1, ubanaji umedhihirika kwani ‘*long-handled tools*’ ingetafsiriwa kama vifaa vyenye mipini mirefu. Katika tafsiri kama hii, mtafsiri anaweza kulaumiwa kuwa amezembea kwa sababu hii ni sentensi ambayo inatafsirika moja kwa moja. “Kuna ukomo wa kimo cha urefu ambapo zana zenye mipini mirefu zinaweza kutumika kuokota mbegu”. Kwa hivyo, katika hali kama hii maarifa na ushauri kuhusiana na matumizi ya zana mahususi, ukusanyaji wa mbegu na shughuli zinazowiana nazo ni mambo yaliyobanwa na kupunguza kiasi cha habari kinachopitishwa katika mchakato huu wa tafsiri.

### **2. Kiingereza:**

In some cases collectors climb trees barefooted or with the help of rope which ties both feet together to press them against the trunk of the tree (pg. 30).

**Kiswahili:**

Nyakati zingine wanaokusanya mbegu hupanda miti hii wakiwa miguu mitupu au wakisaidiwa na kamba (uk. 31).

Katika mfano 2, ujumbe wa kimsingi unahusu mbinu za ukweaji wa miti kwa ajili ya ukusanyaji wa mbegu na undani wa maelezo unakita juu ya namna ambavyo kamba, kama zana ya utenda kazi wa ukweaji miti inavyofungwa ili kuidhibiti miguu kwa kuiweka pamoja, lakini mtafsiri anabana habari hii ikizingatiwa kwamba dhana ya ‘kufunga miguu’ ili kudhibiti ukweaji na dhana ya kushika shina ‘katika mti’ zimeachwa nje kwa kudondoshwa.

**3. Kiingereza:**

‘In the case of shrubs or trees with low branches the collector would stand on the ground and pick seeds from branches which he can reach’ (pg. 30).

**Kiswahili:**

Ikiwa ni kukusanya mbegu kutoka kwa vichaka au miti iliyo na matawi mafupi, mkusanyaji anasimama ardhini ili kutoa mbegu zilizoko kwenye matawi (uk. 31).

Katika mfano 3, habari ya kimsingi inahusiana na uchunaji pamoja na ukusanyaji wa mbegu zenye manufaa kutoka kwa miti. Zaidi ya hayo MC inazungumzia ukusanyaji mbegu kutoka vichakani au kutoka kwa miti iliyo na kimo kifupi kwa maana kwamba matawi yake yanaweza kufikiwa hata kama mtu amesimama ardhini. Lakini pamoja na umuhimu wa habari hizi ambazo zimekitwa katika baadhi ya maneno kama vile ‘*which he can reach*’ mtafsiri ameyaacha nje bila kuyatafsiri na ilhali maneno kama ‘matawi ambayo anaweza kuyafikia yangetumiwa na kwa njia hiyo kuhakikisha kufikishwa kwa habari za kimsingi zilizokusudiwa.

**4. Kiingereza:**

Some of the trees will not germinate if they stay on the tree for too long (pg. 28).

**Kiswahili:**

Aina zingine za mbegu hazichipuki zikikaa sana kwa mti kabla ya kuvunwa (uk. 30).

Katika mfano huu, kinachozungumziwa ni ubora wa mbegu, athari ya mbegu kusalia mtini kwa muda mrefu na uwezekano wa mbegu hiyo kutochipuka kwa haraka wakati imepandwa. Badala ya mtafsiri kuhawilisha habari hii anajaza mambo mengine mapya ambapo katika maneno ‘*stay on the tree for too long*’ yalitafsiriwa kama ‘zikikaa sana kwa mti kabla ya kuvunwa’ kunaibua nyongeza za habari ‘kabla ya kuvunwa’. Hii ni hali inayosababisha mchanganyiko wa mambo.

**5. Kiingereza:**

Easy to coppice (pg. 29).

**Kiswahili:**

Huchipuka haraka ikikatwa (uk. 30).

Katika mfano huu wa 5, neno 'ikikatwa' kwa Kiswahili imeleta nyongeza ya hoja. Katika mfano huu uzidishaji umetokea kwa sababu ya mtafsiri kutokuwa na ujuzi usiotosha kutafsiri '*coppice*' bila kuongezwa maneno ya ziada likawa 'ikikatwa'.

**6. Kiingereza:**

Most seed extraction process of the cones and woody or leathery fruits requires pre-drying of the fruits to extract the seeds easily (pg. 31).

**Kiswahili:**

Shughuli ya kutoa mbegu kutoka kwa maganda ya matunda ya mviringo na mengine yenye ngozi ngumu huhitaji kukaushwa kwanza (uk. 32).

Katika mfano huu wa 6, dhana hii ya '*woody or leathery fruit*' imekosa kufika kwenye ML. Hii inakosesha wapokezi wa ML dhana hii, pengine kwa kukosa msamiati sawia. Maneno haya yangetafsiriwa kama 'tunda la kufanana kama mbao au ngozi'.

**Ubanaji S4****1. Kiingereza:**

In large nurseries (i.e, women group nurseries and school nurseries) considering the work efficiency, the use of watering cans, wheel barrows etc, should also be considered (pg. 37).

**Kiswahili:**

Katika bustani za miche ambazo (kwa mifano, zile za makundi ya akina mama na zile za shule) utumiaji wa birika za kunyunyizia maji, wilibaro na kadhalika ni sharti ziwekwe kwenye orodha ili kuhudumia bustani barabara (uk. 39).

Katika mfano huu wa 1, maneno '*considering the work efficiency*' yamebanwa katika tafsiri yake kwani hayakutafsiriwa. Kinachojaribu kuwasilishwa ni kuonyesha namna ambavyo kazi nyingi inathibitishwa katika bustani za miche. Neno 'wilibaro pia linastahili kutafsiriwa kama 'toroli au bero'. Sababu za upungufu huu unaweza kuwa ukosefu wa istilahi hizi.

**2. Kiingereza:**

The time to start establishing a nursery firstly depends on the time to plant seedlings (pg. 37).

**Kiswahili:**

Wakati wa kuanzisha bustani ya miche hutegemea (uk. 39).

Katika mfano huu habari zilizo katika sehemu ya pili ya sentensi zilibanwa, kwa hivyo si wazi wakati wa kuanzisha bustani ya miche kunategemea nini? Sehemu ya pili ya sentensi hii ingekuwa ‘wakati wa kupanda miche’. Hali hii inawezekana kuzuliwa na uzembe wa watafsiri. Uzingativu wa maana na ujumbe sawia katika MC na ML ungesaidia katika kufanya uteuzi wa visawe mwafaka ili kufanikisha mawasiliano na lengo la tafsiri. Ubanaji huu huifanya hadhira ya ML kukosa maana na ujumbe muhimu ambao unapatikana katika MC.

**3 Kiingereza:**

Dirty water, e.g. soapy water or chemical waste should not be used for watering (pg. 40).

**Kiswahili:**

Maji machafu kama yale yenye kemikali au ya sabuni yasiruhusiwe kutumika kwa minajili hii (uk. 43).

Hapa si dhahiri kuwa maji hayo machafu na ‘uchafu wenye kemikali’ usitumiwe kunyunyizia maji. Kwa sababu ya tafsiri hafifu, dhana ya ‘uchafu wenye kemikali’ umebanwa na haukufikia ML. Hali hii inaweza kusababishwa na ukosefu wa msamiati mwafaka. Sehemu ile ya kunyunyizia maji imetafsiriwa kama ‘kwa minajili hii’ hali ambayo inazua utata wa kimaana. Hadhira ya ML haipati dhana ya unyunyiziaji maji kikamilu kupitia kwa kifungu ‘kwa minajili hii’. Kwa hiyo maana na taarifa anayoipata hadhira lengwa ni tofauti sana na ile inayopatwa na hadhira chanzi. Pia hadhira chanzi na hadhira lengwa wanapata dhana na picha mbili tofauti.

**4. Kiingereza:**

There are many factors which cause damage to the seedlings in the nursery. Among them, biotic factors like pests are mentioned in Chapter 5 (pg. 41).

**Kiswahili:**

Kuna namna nyingi ambazo zinaletea miche uharibifu inapokuwa kwenye bustani. Uharibifu Kama huo ni ule uliotajwa katika Sura ya 5 (uk. 44).

Mfano huu umeonyesha ubanaji wa hoja kuhusu ‘*biotic factors*’ ambayo inaweza kuwa ‘hoja kuhusu viumbe hai na haribifu’, pana ubanji hapa kwani hoja hizi hazikufikia ML. Udondoshaji wa dhana ya viumbe hai inafanya sentensi kuwa na maana finyu kwa HL ikilinganishwa na maana iliyokusudiwa katika hadhira chanzi. Hali hii inasababishwa na ukosefu wa ujuzi wa istilahi za EM.

**5. Kiingereza:**

Strong wind encourages evaporation from the surfaces and the seedlings can also be damaged physically by the sand carried by the winds (pg. 41).

**Kiswahili:**

Upepo mkali hukausha unyevunyevu na hivyo basi hukausha bustani ya miche (uk.44).

Katika mfano huu, mbali na ukaushaji, uharibifu wa kubebwa na changarawe haukutajwa katika ML na huu ni ubanaji wa hoja. Sababu ya ubanaji huu inawezakuwa ukosefu wa makini.

**6. Kiingereza:**

These damages may occur when the tissue of the seedlings are soft or weakened by some reasons (pg. 41).

**Kiswahili:**

Uharibifu huu unaweza kutokea miche inapokuwa ni dhaifu (uk. 44).

Hapa, baada ya ule udhaifu pana habari zilizoachwa nje wakati wa kutafsiri zihusuzo sababu zilizodokezwa katika MC na hazikufikia ML, hii nayo ni hali inayosababishwa na kutokuwa makini. Ujuzi na umilisi wa LC na LL ni muhimu katika tafsiri.

**Ubanaji S5****1. Kiingereza:**

Seedlings are delicate and susceptible to attacks by various pests and diseases as well as some meteorological conditions (pg. 43).

**Kiswahili:**

Miche huwa ni nyororo na hivyo kuna uwezekano wa kuharibiwa na wadudu na magonjwa aina nyingi. Hali ya hewa pia huharibu miche (uk. 46).

Katika mfano huu neno '*delicate*' limetafsiriwa kama 'nyororo' ilhali linaweza pia kumaanisha wepesi wa kuharibiwa. Hali hii, imezua utata wa dhana hii katika ML.

**2. Kiingereza:**

Damages by such pests and diseases seriously weaken or sometimes even kill the seedlings unless they are properly protected before the attacks or treated after the attacks without any delay (pg. 43).

**Kiswahili:**

Uharibifu utokanao na wadudu na magonjwa huharibu vibaya miche na hata wakati mwingine hukausha miche ikiwa hatua za dharura hazichukuliwa (uk. 46).

Hapa dhana ya ‘*before the attacks or treated after the attacks without delay*’ haikufikishwa katika ML kama ‘kuinga miche inastahili kufanywa kabla ya uharibifu au mara tu unapotokea’ kwa hivyo, habari hizi zimebanwa na sababu ya uwezekano wa kutokuwa makini.

**3. Kiingereza:**

There are several types of damages caused by biotic factors (pg. 43).

**Kiswahili:**

Kuna aina nyingi za uharibifu ambazo husababishwa na wadudu (uk. 46).

Katika mfano huu, maneno ‘*biotic factors*’ yametafsiriwa kama wadudu na kuacha dhana ya viumbe vingine. Tafsiri mwafaka ingesema ‘viumbe hai’ dhana inayojumuisha viumbe vingine pia. Katika hali hii, badala ya kuacha kutafsiri maneno ‘*biotic factors*’ na kupoteza maana iliyonuiwa, ufafanuzi ama maelezo yake yangetumiwa katika ML. Sababu hapa inawezakuwa ukosefu wa ujuzi wa istilahi za EM.

**4. Kiingereza:**

However, even in cases where cleanliness is maintained, an attack by the insects could occur (pg. 43).

**Kiswahili:**

Hata hivyo bustani ikiwa safi wadudu wanaweza kuweko (uk. 46).

Katika mfano huu, dhana ya kuwepo kwa wadudu ndiyo imehawilishwa hadi ML lakini dhana ya kushambuliwa na wadudu ‘*an attack by the insects*’ hayakutafsiriwa, yamebanwa. Hali hii huenda ilichangiwa na ukosefu wa msamiati ‘kushambulia’.

**5. Kiingereza:**

They eat a part of or the whole leaf and retard the photosynthetic ability of the seedlings (pg. 43).

**Kiswahili:**

Wadudu hawa hula zile sehemu ambazo hutengeneza chakula cha mti au miche kwa hivyo miche kama huu hauwezi kutengeneza chakula chake wenyewe na hivyo hukauka (uk. 46).

Hapa maneno haya ‘a part of or the whole leaf’ hayakujumuishwa katika tafsiri pengine ni kwa sababu sehemu muhimu zaidi yenye uamilifu hapa ni ile dhana ya ‘*photosynthetic ability*’ (uwezo usanidimwanga) wa iliyotafsiriwa kama ‘sehemu ambazo hutengeneza chakula’ badala ya ‘uwezo wa kutengeneza chakula’. Inawezakuwa istilahi hizi za EM kwa Kiswahili wachanganya watafsiri.

## Ubanaji S6

### 1. Kiingereza:

Management includes a wide range of crucial matters, i.e. planning of the operation, procurement of tools and materials, labour management, supervising the work, recording the activities, etc (pg. 48).

### Kiswahili:

Usimamizi unajumulisha mambo muhimu kama vile kupanga shughuli za bustani, ununuzi wa vifaa na zana za bustani, usimamizi na utekelezaji wa kazi na kadhalika (uk. 52).

Katika mfano huu, dhana zinazodokezwa na ‘*supervising the work*’ na ‘*recording the activities*’ hazikujumishwa katika tafsiri kama ‘usimamizi wa kazi’ na ‘kuweka rekodi za shughuli’. Hii inweza kusababishwa na kutokuwa makini, kwani tafsiri hiyo imeachwa bila kukamilishwa.

### 2. Kiingereza:

Details and target of the job should be explained and understood (pg. 49).

### Kiswahili:

Maelezo kamili ya zile kazi zitakazotekelezwa huelezwa kinaganaga na kueleweka na wafanyikazi wote (uk. 52).

Hapa neno ‘*target*’ ambalo linaweza kuwasilisha ujumbe katika MC kama ‘lengo’ au ‘shabaha’ limebanwa na halikutafsiriwa pengine ni kwa kukosa huu msamiati linganifu.

### 3. Kiingereza:

Nursery foremen should be appointed from among the people who have most of the characteristics (pg. 49).

### Kiswahili:

Msimamizi wa bustani ya miche huwapangia wafanyikazi zile kazi watakazozitimiza (uk. 53).

Hapa kauli kuhusu, ‘*from among the people who have most of the characteristics*’ (kutoka kwa watu ambao wana wingi wa sifa zinazohitajika) imebanwa na haikufikia ML na zile kazi atakazofanya ndizo zimetajwa. Pengine ilichukuliwa kuwa maelezo haya yangefidia yale ambayo huenda watafsiri hawakuwa nayo.

## Ubanaji S7

### 1. Kiingereza:

Accumulated data may reveal some new findings and knowledge (pg. 51).

**Kiswahili:**

Kumbukumbu zilizowekwa vizuri husaidia kupanga kazi na pia hutumika kubashiri na kupanga kazi ya mwaka unaokuja (uk. 56).

Katika mfano huu pana ubanaji kwani kinachobashiriwa ni ujuzi ambao umedokezewa na maneno ‘*may reveal some new findings and knowledge*’ na hakikufikia ML. Sababu hii inawezakuwa lile lengo la kutimiza uamilifu kwani HL wanatakikana kupata ujuzi unaotosha tu.

**Ubanaji S8****1. Kiingereza:**

An uncountable number of trees have been planted by rural people since the extension service started, however, it seems that only a few trees have survived (pg. 54).

**Kiswahili:**

Tangu shughuli za maafisa wa nyanjani kuanzishwa, miti mingi imepandwa. Lakini ukiangalia miti hiyo ni michache sana imesalia (uk. 59).

Katika mfano huu, ubanaji umetokea kwani maneno ‘*by rural people*’ ambayo yanaonyesha kuwa wapandaji miti walikuwa watu wa mashambani, yamedondoshwa katika tafsiri. Pamoja na hayo, maneno ‘*extension service*’ imaanisha huduma za nyanjani. Huenda ujumbe watafasiri hawakutaka kuhusisha miti iliyopandwa na watu wa mashambani kwa sababu ni michache sana imesalia.

**2. Kiingereza:**

Although the harsh environment such as drought, poor soil, wildlife, grazing animals and so forth account for the low survival, poor knowledge and techniques to control them or to protect trees from them are the main reasons (pg. 54).

**Kiswahili:**

Hata ijapokuwa hali ngumu ya hewa ndicho chanzo cha kuangamiza miche iliyopandwa kama vile ukame, udongo usio na rutuba, wanyama na kadhalika, maarifa duni ya utunzaji wa miche kutokana na hali mbaya ya hewa na uharibifu wa wanyama ndicho chanzo kikubwa cha kuangamia kwa miche iliyopandwa (uk. 59).

Katika mfano huu dhana ya ‘mazingira makali’, ambayo imedokezewa na ‘*harsh environment*’ imebanwa na kukosa kutafsiriwa, pengine kwa kudhaniwa kuwa ni sawa na ‘hali ngumu ya hewa’ kwa sababu ya kurahisisha ujumbe unaofikia HL.

**3. Kiingereza:**

When the trees are very young, especially in the first dry season, it is advisable to shade the trees to protect them from strong sunshine which damages young shoots and shallow roots and encourages the evaporation from the soil surface (pg. 56).

**Kiswahili:**

Miti inapokuwa ingali michanga sana, haswa katika mwezi wa kwanza wa kiangazi, inashauriwa kuwekea miti hii uvuli ili kuilinda kutokana na jua kali ambayo huharibu mizizi na michupuko na kukausha udongo (uk. 62).

Katika mfano huu, dhana zinazodokezwa na maneno '*shallow roots*'- (mizizi ya kina kifupi)- '*encourages*' - (saidia), na '*evaporation*'- (vukiza) hazikuhawilishwa hadi ML kwa hivyo ubanaji umetokea. Hizi ni istilahi za EM na zinahitaji utafiti ili kumudu matumizi yake.

**4. Kiingereza:**

It is also easily observed in the field that young trees were malformed and the growth has slowed down because they lost many leaves where necessary materials and energy for their growth are being made (pg. 58).

**Kiswahili:**

Utafiti uliofanywa unaonyesha kwamba miti iliyochengwa inatokezea kuwa na ulemavu au kasoro fulani na miti kama hii inakua pole pole kwa sababu ilipoteza majani mengi na majani haya ndiyo hutengeneza miti chakula (uk. 63).

Katika mfano huu, maneno yafuatayo yametafsiriwa kwa njia inayobana ujumbe unaofikia ML kwa kupewa tafsiri isiyo mwafaka; '*it has been observed in the field*' (imeonekana nyanjani), na '*where necessary materials and energy for their growth are made*'- (mahali ambapo vifaa na nguvu ya kuyakuza inatengeneza). Haya yanaweza kusababishwa na ukosefu wa msamiati mwafaka na vile vile kuufanya ujumbe uwe sahili kwa HL.

**5. Kiingereza:**

In Kenya, people tend to cut off the branches of small trees probably to let them grow in height. However, this is a misunderstanding. When trees are very young, cutting off their branches is rather harmful. Insects and diseases may be able to invade into trees through the injury made by pruning (pg. 58).

**Kiswahili:**

Nchini Kenya, watu hupendelea kupunguza matawi ya miti michanga labda ili miti hiyo iwe mirefu lakini haya ni makosa. Kukata matawi ya miti michanga ni makosa kwa sababu hii ni njia haribifu (uk. 63).

Hapa maneno haya '*Insects and diseases may be able to invade into trees through the injury made by pruning*' yamedondolewa na hayakujumuishwa katika tafsiri. Kudondolewa kwa hoja hizi kumeleta ubanaji kwani hoja hii ya kinachoweza kudhuru miti michanga haikutajwa. Ubanaji huu huenda ukasababishwa na ukosefu wa visawe vya maneno haya katika Kiswahili. Tafsiri mwafaka

ilistahili kuwa ‘Wadudu na mimea inaweza kuingilia miti kupitia kwa jeraha lililoletwa na upogoaji’.

**6. Kiingereza:**

Spot weeding and cleaning of the plantation site are important to keep them away and poisoned bait is to be used with care- strictly when the damage is serious since it is harmful to other animals and humans (pg. 59).

**Kiswahili:**

Kupalilia na kuondoa kwekwe shambani husaidia kuwafukuza panya. Utumiaji wa chambo cha sumu ni mzuri lakini ni hatari kwani sumu hiyo inaweza kuuwa wanyama wasiodhamiriwa kuuawa (uk. 65).

Hapa maneno ‘*spot weeding*’ hayakutafsiriwa kikamilifu na mwishoni mwake, neno ‘*humans*’ halikutafsiriwa. Kwa kuogopa kutoa tafsiri isiyo sahihi, watafsiri wamedondoa maneno haya na kusahau hata kuta maneno ‘*spot weeding*’-‘upaliliaji doa’, ‘*humans*’- ‘binadamu’ athari ya HL kukosa hoja hizi ni hatari kwani wanaweza kudhani sumu hiyo si hatari kwa binadamu.

**7. Kiingereza:**

Change and wash your clothes well after using chemicals (pg 59).

**Kiswahili:**

Badilisha nguo zako baada ya kunyunyiza dawa (uk. 65).

Katika mfano huu, neno ‘*wash*’ (osha) halikutafsiriwa. Kutojumuisha neno hili kuna hatari ya HL kudhani kuwa si muhimu, athari yake inaweza kuhatarishwa afya ya wapokezi.

**Ubanaji S9**

**1. Kiingereza:**

Does well in high rainfall but dry period is essential at flowering and fruiting. Flowering depends on photoperiodism, temperature and dry period (pg. 61).

**Kiswahili:**

Maembe hukuzwa vizuri katika maeneo ya mvua nyingi lakini majira ya kutoa maua yawe kavu. Hali pia iwe hivi wakati wa kuzaa maembe. Majira ya kutoa maua hutegemea kiasi cha joto na majira yasiyo na mvua (uk. 67).

Katika mfano huu, istilahi ‘*photoperiodism*’ (muda wa mwangaza) ambalo ni msamiati wa EM, limebanwa na halikutafsiriwa. Hali hii huenda ilisababishwa na kukosa kisawe chake kwa Kiswahili, kwa hivyo ile dhana iliyokusudiwa haikufika katika MC.

## **2. Kiingereza:**

Soils should be rich and well drained with a pH of 5.5-7.5 (pg. 61).

### **Kiswahili:**

Udongo uwe wenye rutuba na tifutifu unaopitisha maji (uk. 67).

Hapa tafsiri ya 'pH' yalibanwa na hayakutafsiriwa. Hii ni kwa sababu kisawe chake hakipo katika Kiswahili na wasayansi huitaja tu kama 'kipimo pH'. Kudondoa herufi hizi kunasababisha ukosefu wa hoja hii muhimu kwa MC, hali ambayo inaweza kuleta upungufu wa habari na hivyo kuathiri shughuli hizi za upandaji.

## **3. Kiingereza:**

Transplanting is carried out after the seedlings have taken four months in the nursery (pg. 61).

**Kiswahili:** (Sentensi hii ya Kiingereza haikutafsiriwa).

*Tafsiri: Kupandikiza kunafanywa baada ya miche kumaliza miezi minne katika bustani.* Kukosa kutafsiri sentensi hii kunakosesha MC habari muhimu, sababu inawezakuwa kuogopa kupotosha HL kwa sababu ya uwepo wa istilahi '*transplanting*'.

## **4. Kiingereza:**

Mango weevil, Small larvae enter the fruits and attack the seeds. There may be a hard white area in the flash. Fruits may fall early or rot in storage (pg. 61).

### **Kiswahili:**

Viwavi wa miembe, mabuu wadogo huingilia matunda ya mwembe na kisha kushambulia mbegu za mwembe. Kwa sababu hii miembe huanguka mapema kabla hayajakomaa au kuoza yakihifadhiwa (uk. 68).

Katika mfano huu, maneno '*there may be a hard white area in the flash*' yamebanwa na hayakutokezea katika tafsiri.

## **5. Kiingereza:**

Stem rot, this is a soil borne fungus disease common in poorly drained soils. The trunk of the tree rots and the base and leaves wilt (pg. 62).

### **Kiswahili:**

Kuoza shina, huu ni ukungu ambao hutoka kwenye udongo ambao hupatikana kwa wingi katika udongo usio tifutifu. Shina la mti huoza na kufifia (uk. 69).

Katika mfano huu, maelezo kuwa 'huu ni ugonjwa wa ukungu' yamebanwa na hayakutokezea.

**6. Kiingereza:**

Green mould, common in stored fruits although it may be observed in the orchard (pg. 65).

Control; care should be observed when harvesting to avoid abrasion and wounding of the fruit (pg. 65).

**Kiswahili:**

Ukungu wa kijani kibichi, ukungu huu haswa hushambulia matunda yaliyohifadhiwa isipokuwa hata hivyo pia huonekana kwenye matunda yaliyoko kwenye bustani (uk. 72).

Jinsi ya kuzuia ukungu wa kijani kibichi: Wakati wa kuvuna machungwa uangalifu mkubwa ni lazima kuchukuliwa ili machungwa yahifadhiwe kwa muda mrefu na machungwa kuwekwa dawa (uk. 72).

Katika mfano huu, maneno; *to avoid abrasion and wounding of the fruit* yamebanwa na hayakutafsiriwa.

**6. Kiingereza:**

Sword suckers, suckers that are formed from bud low on the corn and bear narrow sword leaves, plucked from the plant when they are 0.6-1.2 m in height and about 15 cm in diameter (pg. 66).

**Kiswahili:**

Zile chipuka kutoka kwenye shina na huwa na majani membamba yenye umbo la upanga (uk. 75).

Haba habari hizi ‘plucked from the plant when they are 0.6-1 m in height and about 15 cm in diameter’ yamebanwa na hayakutokezea.

**8. Kiingereza:** Mulch should be kept away from the stool (pg. 67).

**Kiswahili:**

Migomba chipukizi kutoka maeneo yenye viwavi hawa iwekewe tahadhari ili kuzuia kutapakaa kwa viwavi hawa shambani (uk. 75).

Hapa tafsiri ya sentensi hiyo haikufanyika. Tafsiri ingekuwa; matandazo yanastahili kuwekwa mbali na kinyesi.

**Ubanaji S 10**

**1. Kiingereza:**

Helps propagate clones that can be conveniently reproduced by other methods, e.g. cuttings, layers, division or other sexual methods (pg. 71).

**Kiswahili:**

Huasidia kuzalisha jamii ya miti ambayo kwayo haiwezi kuzalishwa kwa nia yoyote ile (uk. 80).

Katika mfano huu maneno ‘*cuttings*’, ‘*layers*’, ‘*division*’, na ‘*other sexual methods*’ yamebanwa na hayakutafsiriwa.

**2. Kiingereza:** Overgrowth at, above or below the graft union (pg. 71).

**Kiswahili:** (haikutafsiriwa).

Tafsiri; kukua zaidi katika, juu ya au chini ya kiunganishi cha tumba.

**3. Kiingereza:**

Remove side roots and thorns from the lower part of the root stock (pg. 73).

**Kiswahili:**

Ondoa mizizi ya kando kando ya shina asili kutoka sehemu ya chini (uk. 82).

Katika mfano huu, neno ‘*root stock*’ limetafsiriwa kama sehemu ya chini.

## Ubanaji S11

**1. Kiingereza:**

Most energy needs and other benefits have been satisfied from the trees (pg. 76).

**Kiswahili:**

Matumizi yetu ya nishati kwa kiasi kikubwa inapatikana kutokana na miti (uk. 85).

Katika mfano huu, maneno ‘*other benefits*’ yameondolewa na hayakutafsiriwa.

**2. Kiingereza:**

The optimum spacing between rows is around eight metres but also depends on the crops and their shade tolerance and the tree species with its consequent shading effect (pg. 77).

**Kiswahili:**

Kipimo kinachopendekezwa kutoka mstari mmoja hadi mwingine ni karibu mita nane lakini hii hutegemea na aina ya mimea vile mimea hii hustahimili uvuli (uk. 87).

Hapa maneno haya ‘*and the tree species with its consequent shading effect*’ hayajazingatiwa katika tafsiri.

### **3. Kiingereza:**

Live fence consists of dense hedges or thickets usually planted around a garden or farm to protect it from free ranging livestock (pg. 79).

### **Kiswahili:**

Ua la miti huwa ni kitalu au vichaka ambavyo huwa vimepandwa kuzunguka boma au nyumba ili kuzuia mifugo kuingia shambani au uwanja wa nyumbani (uk. 89).

Maneno '*free ranging*' yamebanwa na hayakutafsiriwa.

### **4. Kiingereza:**

Shrubier species are used and the shrubs and trees are tightly spaced (0.5-1 metre), and they are intensively pruned to maintain a compact, dense barrier (pg. 79).

### **Kiswahili:**

Jamii ya miti yenye kichaka ndiyo hupendelewa na miti hii hupandwa ikiwa imefanyana (mita 0.5-1) na huchengwa vilivyo ili kukuza kichaka ambacho hakiwezi kupenyeka (uk. 89).

Hapa maneno '*compact, dense*' hayakutafsiriwa kikamilifu.

### **5. Kiingereza:**

Live fences can also be established to protect fallow lands and/or denuded areas due to overgrazing and to allow the area to be rehabilitated by the natural regeneration or planting certain tree species (uk. 89).

### **Kiswahili:**

Ua la miti pia hupandwa ili kuzuia mifugo kuingia mashamba ambayo yameachwa kumea nyasi au sehemu zilizoharibiwa na wanyama, na kuachwa bila mimea yoyote (uk. 89).

Maneno haya '*fallow lands*', 'rehabilitated' na '*natural regeneration*' hayakutafsiriwa, yamebanwa.

## **Ubanaji S12**

### **1. Kiingereza:**

Soil erosion can be defined as the detachment and transportation of soil particles by water and wind. The present topography and distribution of soil are the results of erosion and sedimentation process over millions years (pg. 85).

### **Kiswahili:**

Mmomonyoko wa udongo unaweza kuelezwa kama ile hali ya maji au upepo kupeperusha au kusafirisha chembechembe za udongo. Umbo la sasa la ardhi limetokana na kurundikwa kwa udongo kwa kipindi cha mamilioni ya miaka (uk. 95).

Katika mfano huu, maneno ‘*topography and distribution*’ yamedondolewa na hayakutafsiriwa.

**2. Kiingereza:**

The soil conservation approach can be taken in two ways. One is the biological/cultural measures including farm management techniques and another is physical measures like terraces, usually combined with biological measures (pg. 86).

**Kiswahili:**

Uhifadhi wa udongo unaweza kutazamwa kwa mitazamo miwili. Mtazamo wa kwanza ni ule wa kimaumbile kama vile usimamizi bora wa shamba. Mtazamo huu mwingine wa pili ni kujenga matuta ambayo yanaweza kuunganishwa na ule wa maumbile (uk. 96).

Tafsiri ya maneno haya; ‘*cultural measures*’ na ‘*physical measures*’ yamezua ubanaji kwani ‘njia za kitamaduni’ na ‘njia za kimaumbile’ huenda zingefaa zaidi.

**3. Kiingereza:**

Retention ditches are dug along the contour lines and water caught is going to infiltrate into the soil. This technique is recommendable especially in dry area (pg. 87).

**Kiswahili:**

Mahandaki ya kunasa maji pia ni njia moja ya kuzuia mmomonyoko wa udongo wa fanya chini isipokuwa hii njia huzuia maji, hali ile ya mifereji huelekeza maji hadi kwenye ili kumwaga maji. Aina hii ya kuzuia mmomonyoko wa udongo hutumika sehemu kame (uk. 98).

Katika mfano huu, neno ‘*recommendable*’ halikutafsiriwa.

**4. Kiingereza:**

A bench terrace is a combination of horizontal or nearly horizontal ledges, vertical or almost vertical walls and often channels, to convert a steep slope into a series of steps (pg. 88).

**Kiswahili:**

Tuta linalokaa kama kiti (bench terrace) huwa ni mchanganyiko wa kingo za kuta zilizo wima au karibu kuwa wima na kinga zisizo wima na wakati mwingi huwa kama mfereji (uk. 98).

Hapa maneno ‘*to convert a steep slope into a series of steps*’, hayajatokezea katika tafsiri.

**5. Kiingereza:**

When cultivation is not required, as for fruit trees, smaller terraces will need less earth moving and be equally effective (pg. 88).

**Kiswahili:**

Mazao kama vile matunda ikiwa yatapandwa basi viti vya matuta visiwe pana. Matuta kama haya hayana kazi nyingi ya kusongesha udongo (uk. 99).

Hapa ile hoja inayodokezwa kwa maneno haya; '*when cultivation is not required*' haikutokezea.

**6. Kiingereza:**

Check dams made of stones must not reach the top of the gully. Stones should be carefully laid, and in-filled with earth sods. Excavate base in gully floor and fill with smaller stones (pg. 91).

**Kiswahili:**

Silanga zinazotengenezwa kwa mawe yasifike juu ya mtaro bali tu yatandazwe chini ya mtaro kwa uangalifu na kujazwa na bumba la udongo na nyasi. Chimba sakafu ya mtaro huu (uk. 102).

Katika mfano huu, neno silanga limetumiwa kama tafsiri ya maneno '*check dams*' na si Kiswahili sanifu.

**7. Kiingereza:**

Windbreaks and shelter belts are strips of and other vegetation that slow the flow of the wind, reducing wind erosion, evaporation and wind damage to crops (pg. 91).

**Kiswahili:**

Vizuizi vya upepo huwa ni safu ya miti na mingine ambayo hupunguza mwendo wa upepo na hivyo kupunguza mmomonyoko uletwao na upepo, kunyauka kwa unyevunyevu kunaletwa na upepo na hatimaye kupunguza uharibifu uletwao na upepo (uk. 103).

### 3.2.2 Kuhusu uzidishaji

#### Uzidishaji S2

Uzidishaji kama ulivyoielezwa katika sehemu za awali ni hali ya kuingiza nyongeza za maneno, maelezo au kutafsiri kwa njia ya mzunguko hivi kwamba kinachotafsiriwa huwa kimerefushwa kuliko ilivyo katika matini chanzi. Uzidishaji umetumika kwa wingi katika kutafsiri kijitabu hiki *Social Forestry Techniques (1991)*", ambacho kimetafsiriwa kama: *Mbinu za Utunzaji Miti katika Misitu ya Jamii (1991)*. Ithibati iliyoko ni kwamba uzidishaji umetokea kwa kushinikizwa na sababu kadha wa kadha kama vile udhibiti duni na kutoelewa msamiati wa kitaalam na hata wa kawaida katika matini chanzi, kupuuza kuhawilisha habari au miundo ya lugha ambayo ni muhimu katika kudhibiti habari zinazohawilishwa na vilevile kuingiza uziada usiokuwa wa lazima. Kwa sababu hizi na nyingine sawia na hizo, uhamishaji wa habari kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa kumetatizwa si haba. Kwa muktadha wa utafiti huu tunaweza kuhoji kwamba tafsiri ya *Mbinu za Utunzaji Miti katika Misitu ya Jamii (1991)* haijatosheleza majukumu mahususi ya kazi asilia, yaani kusudi la kutoa ufahamu, maarifa na ujuzi kuhusu upandaji na utunzaji miti. Mifano kadha wa kadha ya uzidishaji imetolewa hapa chini.

#### 1. Kiingereza:

We focus on trees in rural life and introduce some important species (pg. 13).

#### Kiswahili:

Tutatupa macho kwenye umuhimu wa miti katika maisha ya waishio mashambani (uk. 14).

Katika mfano huu, inastahili kujitokeza kuwa waandishi wa MC wanafikiria miti katika eneo la mashambani na kutanguliza aina muhimu ya miti, maneno mengi yametumika na hoja hizi hazikutajwa namna invyostahili. Isitoshe, watafsiri wanapotumia usemi kama "Tutatupa macho kwenye umuhimu wa miti katika maisha ya waishio mashambani" ni ishara kamili ya tafsiri chapwa badala ya kuibua tafsiri sahihi kama "Tunaangazia umuhimu wa miti katika maisha ya wakazi wa sehemu za mashambani". Kwa kimsingi tafsiri hii ina walakini wa aina mbili, uzidishaji unaoishia katika upotoshaji.

#### 2. Kiingereza:

This is a real multipurpose tree, fast growing, giving high yields of firewood and timber is also high quality for poles and construction timber (pg. 10).

**Kiswahili:**

Mti huu una manufaa sana. Unakua haraka na hutoa kuni nzuri na mbao zake ni za hali ya juu sana kwa matumizi ya nguzo na mbao za ujenzi (uk. 17).

Mfano 2 umeonyesha uzidishaji uliotokana na urudiaji wa neno ‘mbao’ ambapo haikuhitajika lirudiwe, aidha neno ‘*multipurpose*’ lililo na maana ya ‘matumimizi mengi’ halikutolewa tafsiri mwafaka. Huenda ni kwa watafsiri kukosa kisawe cha neno hilo. Dhana inayozuliwa na neno ‘manufaa’ ni tofauti kabisa.

**3. Kiingereza:**

This is one of the most widespread trees in Africa but originally came from Asia (pg. 16).

**Kiswahili:**

Huu ni mojawapo wa miti ambayo imepatikana kote barani Afrika na ambayo hapo zamani ilitokea barani Asia (uk. 17).

Katika mfano 3 uzidishaji umetokea kwa kutafsiri ‘...*but originally came from Africa...*’ kama ‘...ambayo hapo zamani ilitokea barani Afrika’ badala ya lakini asili yake ilikuwa barani Asia. Ni dhana ya asili yake tu ilihitajika kutajwa kuwa ni barani Asia na ni ukweli hata wakati huu. Hapa ni ukosefu wa umahiri wa lugha umesababisha uzidishaji kiasi ch habari.

**4. Kiingereza:**

This is a well-known agroforestry species especially for dry areas in Africa (pg. 14).

**Kiswahili:**

Hii ni aina ya miti inayojulikana sana katika kilimo cha mimea na misitu (agroforestry) haswa katika sehemu kavu za Afrika (uk. 15).

Katika mfano 4, ujumbe kuwa aina hii ya mti wa kilimomseto (*agroforestry*) haukujitokeza katika ML kwani ulivyotafsiriwa ujumbe huu umekosa kutafsiri dhana hiyo ya kitaaluma hiyo kwa usahihi. Hali hiyo imezua uzidishaji katika ML kwa sababu ya ukosefu wa istilahi hii.

**5. Kiingereza:**

Its root is deep and does not compete with crops for moisture’ (pg. 14).

**Kiswahili:**

Mizizi yake huenda chini na wakati huo huo haishindani kwa kuvuta maji na mimea mingine ya mkulima (uk. 15).

Mfano wa 5 umeonyesha uzidishaji kwani maneno; 'mimea mingine ya mkulima` hayakuwa yametajwa katika MC, hii imezua uzidishaji kwani dhana ya kumiliki mimea kwa mkulima halipo katik MC na yanjitokeza katika ML. Sababu inaweza kuwa ni ile hali ya kutaka kuhusisha shughuli hizi na mkulima.

**6. Kiingereza:**

This species is nitrogen fixing like other legumes and nutrient rich leaves can be used as fertilizers (pg. 14).

**Kiswahili:**

Mti huu huchanganya udongo na nitrogen kama vile mimea mingine kama maharagwe na majani yake huwa na chakula kingi na yanaweza kutumika kama mbolea nzuri sana 9 (uk.15).

Katika mfano wa 6, maneno *'nutrient rich'* yametafsiriwa kama 'kuwa na chakula kingi' na *'fertilizer'* imesifiwa kama mbolea kuwa nzuri sana, hali ambayo haikuwa katika MC. Tafsiri hizi zimezua hali ya uzidishaji na upotoshaji katika MC. Sababu za hali hii kutokea ni ukosefu wa istilahi za kuelezea dhana hizi.

**7. Kiingereza:**

This species loses its leaves in the rainy season (pg. 14).

**Kiswahili:**

Mti huu hupoteza na huyaangusha majani yake nyakati za mvua (uk. 15).

Katika mfano huu, neno 'huyaangusha' ni la ziada kwani 'hupoteza' ni tafsiri mwafaka wa neno 'loses'.

**8. Kiingereza:**

... 'so that the crops under the trees are never disturbed by shading' (pg. 14).

**Kiswahili:**

... 'na hivyo kuhakikisha mimea ya mkulima iliyoko chini ya mti huu haiharibiwi na majani haya' (uk. 15).

Mfano huu una maneno ya ziada ambayo ni 'mimea ya mkulima', maneno ambayo kama hayangetumiwa tafsiri ya matini hayo bado yanatosha. Sababu za kufanya hivi inaweza kuwa kujaribu kuhusisha mimea na mkulima.

**9. Kiingereza:**

This is probably the most common tree for charcoal making in dry areas of Kenya (pg. 15).

**Kiswahili:**

Aina hii ya miti aghalabu hupatikana kwa wingi katika zile sehemu kavu za Kenya na ni mashuhuri kwa uchomaji wa makaa (uk.16).

Tafsiri hii ina uzidishaji wa kiasi cha habari kwani neno mashuhuri limeongezwa katika ML na linataja dhana ambayo halipatikani katika MC. Hali huenda ulisababishwa na ukosefu wa makini.

**10. Kiingereza:**

*Acacia nilotica* (Musemei, Mugungu) has similar characteristics and uses (pg. 15).

**Kiswahili:**

*Acacia nilotica* una manufaa kama yale ya miti ya jamii iliyotajwa hapo juu (uk. 16).

Katika mfano wa 10, neno `*characteristics*` limetafsiriwa kama `*manufaa*` huenda neno `*sifa*` ungelifaa zaidi. Lakini pia maneno ya kiasili ya kurejelea mti unaotajwa yameachwa nje.

**Uzidishaji S4**

**1. Kiingereza:**

Nursery techniques (pg. 35).

**Kiswahili:**

Maarifa yanayotumiwa kwenye bustani ya miche (uk. 37).

Hapa pana urefushaji kwani neno `*techniques*` yameongezea maneno kama `*maarifa yanayotumiwa*` katika tafsiri.

**2. Kiingereza:**

Several important factors are to be considered, out of these a few fundamental factors for semi-arid areas (pg. 38).

**Kiswahili:**

Kuna mambo fulani ambayo ni sharti yafikiriwe kabla ya kuanzishwa kwa bustani, baadhi ya haya ni lazima yatimizwe haswa kwa sehemu kavu kama zile za mkoa wa mashariki ya Kenya (uk. 38).

Maneno `*kabla ya kuanzishwa kwa bustani*` na `*kama zile za mkoa wa mashariki ya Kenya*` ni nyongeza ambayo hayapo katika MC.

**3. Kiingereza:**

Protected from strong wind (pg. 36).

**Kiswahili:**

Eneo la bustani ya miche lililokingwa kutokana na upepo mkali (uk. 38).

Katika mfano huu, uziada umetokea kwa kuongezea maneno “eneo la bustani ya miche” kwani MC hayana dhana hii. Watafsiri wanaonekana kuhusisha dhana zote na bustani ya miche. Maneno ‘lilokingwa kutokana na upepo mkali’ yanatosha tu.

**4. Kiingereza:**

Sunny condition (pg. 36).

**Kiswahili:**

Jua lipatikane wakati wote (uk. 38).

Maneno zaidi yametumika hapa; ‘lipatikane wakati wote’ wani maneno ‘hali ya jua’ yage tosha tu.

**5. Kiingereza:**

Near the supervisor’s house for daily management in case of nurseries managed by groups (pg. 36).

**Kiswahili:**

Bustani liwe karibu na nyumba ya msimamizi au nyapara wa bustani kwa usimamizi bora wa bustani, ikiwa bustani ni ya vikundi vya maendeleo au ushirika (uk. 38).

Maneno yaliyo kabla ya ‘karibu na nyumba ya msimamizi’ ni ya ziada.

**6. Kiingereza:**

Fencing around the nursery for keeping the livestock out (pg. 37).

**Kiswahili:**

Kuzungushia ua bustani ya miche ili kuzuia mifugo isiharibu miche (uk. 39).

Hapa maneno ‘isiharibu miche’ ni ya ziada. Uziada huu umetokana na watafsiri kuhushisha kila hoja na ‘bustani ya miche’ na kuishia kuleta kiasi kingi cha habari katika MC.

**7. Kiingereza:**

The number and kind of essential tools depends on the scale of the nursery and number of workers (pg. 37).

**Kiswahili:**

Aina ya zana au wingi wa zana za bustani ya miche hutegemea ukubwa wa bustani au idadi ya wafanya kazi (uk. 39).

Maneno ya ziada hapa ni ‘zana za bustani ya miche’ ni ya ziada na hayakuhitajika.

**8. Kiingereza:**

The soil is dug up to about 10 cm deep using jembes after scrapping of the vegetation (pg. 37).

**Kiswahili:**

Udongo huu huchimbuliwa hadi kina cha sentimita kumi kwa kutumia jembe baada ya kuondoa nyasi na takataka yote ya ardhi (uk. 39).

Katika mfano huu maneno ‘na takataka yote ya ardhi’ ni ya ziada, kwani yamejumuishwa katika ML na hayakuwa katika MC.

**9. Kiingereza:**

Also locally available material like small or big tins, tetra-packs, milk packets, boxes, etc. can be used (uk. 39).

**Kiswahili:**

Pia vifaa vya kawaida kama vile mikebe, karatasi za maziwa, karatasi za maji ya machungwa, visanduku na kadhalika hutumiwa kwa shughuli hii (uk. 40).

Katika mfano huu; ‘karatasi za maji ya machungwa’ na ‘kwa shughuli hii’ ni maneno ya ziada.

**10. Kiingereza:**

For big seeds like *Tamarindus indica*, *Croton megalocarpus* and Cassia species, it is more economical to sow them directly into the pots (pg. 38).

**Kiswahili:**

Kwa zile jamii ambazo mbegu zake ni kubwa kama zile za *Tamarindus indica*, *Croton megalocarpus* na Cassia huwa na gharama ndogo ikiwa mbegu zitapandwa moja kwa moja (uk. 41).

Majina ya miti na hata ya wadudu ya kisayansi hapa kama vile; ‘*Tamarindus indica*’, ‘*Croton megalocarpus*’ na ‘Cassia’ hayawezi kutafsiriwa. Hata hivyo, majina ya kawaida yangetumiwa.

**11. Kiingereza:**

Make light shade using small poles and light grasses’ (pg. 39).

**Kiswahili:**

Tengeneza uvuli kupenyeza mwangaza wa juu na uliojengwa kwa nguzo ndogo ndogo na kuezekwa na nyasi zilizokauka (uk. 41).

Maneno ‘kupenyeza mwanga wa juu na uliojengwa kwa nguzo ndogo ndogo’ ni ya ziada, hayakuwa katika sentensi ya MC.

**12. Kiingereza:**

The pricking process (pg. 39).

**Kiswahili:**

Ifuatayo ndiyo ambayo njia hutumiwa kuandikiza miche (uk. 42).

Maneno ‘ifuatayo ndiyo njia ya’ hayakustahili kutumiwa kwani ni ya ziada.

**13. Kiingereza:**

If it is raining, watering might not be necessary (pg. 40).

**Kiswahili:**

Kama kuna mvua, mifuko ya miche haihitaji kunyunyiziwa maji (uk. 43).

Hapa maneno ‘mifuko ya miche’ ni ya ziada. Tafasiri kwa mfano; ‘kama kuna mvua unyunyizaji maji hauhitajiki’yangetosha tu. Hapa pana ile dhana ya kuhusisha shughuli zote na miche.

**Uzidishaji S5****1. Kiingereza:**

There are many factors affecting tree seedlings in nurseries, and they are generally categorized in three meteorological factors as follows: These are drought, high temperature, strong wind, etc. Most of disasters caused by meteorological factors can be prevented by physical countermeasures, e.g. frequent watering, shedding and windbreaks (pg. 43).

**Kiswahili:**

Kuna aina nyingi ya uharibifu na mikasa ambayo hudhuru bustani ya miche na huorodheshwa katika makundi matatu kama ifuatavyo: Madhara ambayo huletwa na hali ya hewa ni kama vile kiangazi, kiwango cha juu ya joto, upepo mkali na kadhalika (uk. 46).

Katika mfano huu, neno ‘meteorological’ lilstahili kutafsiriwa katika sentensi hiyo ya kwanza badala ya kulisongesha hadi sentensi ya pili.

**2. Kiingereza:**

Human factors. Disasters caused by men are such as trespass in a nursery and robbery of seedlings (pg. 43).

**Kiswahili:**

Mkasa au uharibifu uletwao na binadamu ni kama ule wa watu kupitia shambani bila ruhusa na kukanyaga miche (uk. 46).

Wizi wa miche pia ni uharibifu uletwao na binadamu (uk. 46). Maneno ‘kukanyaga miche’ ni ya ziada.

**3. Kiingereza:**

All weeds should be regularly uprooted and swept away (pg. 43).

**Kiswahili:**

Bustani la miche lazima liwe wakati wowote limeokotwa taka kwa kufanya kwote na ufagio (uk. 46).

Hapa maneno ‘bustani la miche lazima liwe wakati wowote limeokotwa taka’ ni ya ziada. Neno ‘kwote’ pia si sahihi.

**4. Kiingereza:**

Defoliators (Various groups of insects such as caterpillars (larvae of butterflies or moths) grubs (larvae of beetles), crickets, grasshoppers, etc. (pg. 43). They eat part of or the whole leaves and retard the photosynthetic ability of the seedlings (pg. 43).

**Kiswahili:**

Wadudu wanaoshambulia majani. Vikundi vingi vya wadudu kama vile viwavi (mabuu ya kipepeo au nondo) panzi, nzige, nyenje na kadhalika hula matawi au majani ya miti (pg. 46). Wadudu hawa hula zile sehemu ambazo hutengeneza chakula cha mti au miche kama huu hauwezi kutengeneza chakula chake wenyewe na hivyo hukauka (uk. 46).

Katika mfano huu, maneno ‘ambazo hutengeneza chakula cha mti au miche kama huu hauwezi kutengeneza chakula chake wenyewe’ ni ya ziada.

**5. Kiingereza:**

Control: It is not easy to deal with cutworms once they have started to attack (pg. 43).

**Kiswahili:**

Uzuiaji wa viwavi wa kukata mashina: siyo jambo rahisi kupambana na viwavi hawa mara wanapoanza kushambulia miche (uk. 47).

Tafsiri mwafaka ingekuwa ‘udhibiti: si rahisi kupambana viwavi mara wanapoanza ushabulizi’. Ni katika juhudi za kujaribu kurahisisha mambo ya upanji miti na kuhusisha na miche.

**6. Kiingereza:**

However, some measures such as spraying chemicals, e.g. Aldrin and Diazinon, could be effective (pg. 43).

**Kiswahili:**

Hata hivyo madawa ya kemikali kama vile Aldrin na Diazinon yaweza kuwaua viwavi hawa (uk. 47).

Katika mfano huu, maneno ‘could be effective’ yametafsiriwa kama ‘yaweza kuwaua viwavi hawa’ ambayo ni uzidishaji, kwani dhana iliyotajwa ni ‘inaweza kufaa’.

**Uzidishaji S6****1. Kiingereza:**

In case of schools, a teacher, possibly of science or agriculture, should be assigned (uk. 48).

**Kiswahili:**

Ikiwa ni bustani ya miche ya shule, mwalimu, kwa mfano wa kilimo au sayansi, atapatiwa wadhifa wa kusimamia bustani kama hii (uk. 52).

Katika mfano huu; pana uzidishaji wa neno kama, ‘bustani ya miche ya’ na kusimamia bustani kama hii’.

**2. Kiingereza:**

Selection of species: Select the species to be raised in the nursery, considering the use. In case of the groups’ nurseries, the selection and priority of the species should be discussed and agreed among the members (pg. 48).

**Kiswahili:**

Kuchagua aina ya miti itakayopandwa: Chagua aina ya miti utakayopanda katika bustani, huku ukitilia maanani ni kazi gani utaifanyia ikiwa mikubwa (uk. 52).

Hapa maneno ‘utaifanyia ikiwa mikubwa’ yameongezwa.

**3. Kiingereza:**

In schools, it is a good idea to involve the daily operation in classes or in a club activity (4K club, etc.) (pg. 49).

**Kiswahili:**

Katika bustani za shule ni jambo nzuri kuhusisha darasa nzima kwa shughuli za bustani au vyama vya shule, kwa mfano chama cha kilimo cha vijana (4K club) na kadhalika (uk. 53).

Hapa nyongeza ya maneno yamefanywa, maneno; ‘kwa mfano, chama cha kilimo cha vijana (4K club) na kadhalika’.

**4. Kiingereza:**

He/she should be a very honest and strict person because there are many valuable things in the nurseries, and sometimes even money, for operation (pg. 49).

**Kiswahili:**

Msimamizi wa bustani ni sharti awe mwaminifu na mwenye nidhamu kwa sababu bustani ya miche huwa na pesa aina za kulipia kazi au zana za kazi na kwa hiyo ni lazima awe ni mtu ambaye hawezi kujaribu kuiba (uk. 54).

Maneno ya ziada hapa ni; ‘au zana za kazi na kwa hiyo ni lazima awe ni mtu ambaye hawezi kujaribu kuiba’.

**5. Kiingereza:**

He/she does not need to be a full-time nursery worker, but should have enough time to be in the nursery (pg. 49).

**Kiswahili:**

Msimamizi wa bustani siyo lazima awe mfanyikazi wa kudumu lakini awe ni mtu ambaye ana wasaa wa kutosha ili kutumikia bustani la miche na kuwa hapo anapohitajika (uk. 54).

Maneno haya; ‘ili kutumikia bustani la miche na kuwa hapo anapohitajika’ yameongezewa kama maneno ya ziada.

**Uzidishaji S7**

**1. Kiingereza:**

Recording all the work and progress in the nursery is essential in the nursery management, i.e. management of daily operation, labour, cost, etc. (pg. 51).

**Kiswahili:**

Kuweka kumbukumbu ya kazi na maendeleo yoyote yaliyopatikana kwenye bustani ni jambo la lazima kwani hii ni muhimu kwa usimamizi wa bustani kama vile usimamizi wa kila siku wa kazi, wafanyi kazi, gharama iliyotumika na kadhalika (uk. 56).

Hapa neno ‘essential’ limetafsiriwa kama ‘ni jambo la lazima kwani hii ni muhimu’ ambayo ni kutumia maneno mengi yasiyostahili.

**2. Kiingereza:**

A large nursery needs an intimate record and many record books while a small nursery being operated by an individual farmer may need only a book (pg. 51).

**Kiswahili:**

Bustani kubwa inahitaji kumbukumbu za kila siku na vitabu vingi vya kumbukumbu na hali bustani ndogo inayoendeshwa na mkulima mmoja inahitaji kitabu kimoja cha kuandikia habari za kila siku za bustani (uk. 56).

Katika mfano huu, ‘need only a book’ imetafsiriwa kama ‘inahitaji kitabu kimoja cha kuandikia habari za kila siku za bustani’ ambayo ni uzidishaji. Pia neno ‘intimate’ halikutafsiriwa vilivyo.

**3. Kiingereza:**

This is to keep the record to show how the seedlings were distributed (pg. 52).

**Kiswahili:**

Hiki ni kitabu cha kuonyesha vile miche ilivyotolewa au kugawanywa (uk. 57).

Katika mfano huu, neno kujumuisha neno ‘kitabu’ katika ML ni uzidishaji. Lengo hapa ni kutoa ufafanuzi zaidi kwa HL.

**4. Kiingereza:**

Names of the people who receive the seedlings from nursery and their addresses should also be recorded in sufficient details to enable a follow up (pg. 52).

**Kiswahili:**

Majina ya wale wote waliopokea miche kutoka bustani hilo na anwani zao ni sharti pia ziandikwe kwa kikamilifu ili kufuatisha jambo lolote litakalotokea (uk. 57).

Hapa maneno ‘wale wote’ kama tafsiri ya neno ‘*people* kama’ ni uzidishaji. Hi ni kwa sababu katika ML hakuna dhana ya ML.

**5. Kiingereza:**

However, whenever there are some visitors, not only to ask them to sign on the book, but also to comment about your nursery and to record their suggestion which may be useful (pg. 52).

**Kiswahili:**

Lakini hata hivyo wageni wanapotembelea bustani la miche, waulize wageni hao kuandika majina yao kwenye kitabu hiki huku wakitoa maoni yao juu ya bustani yako. Maoni kama hayo yanaweza kukusaidia kuendeleza bustani yako na kusahihisha makosa yoyote ambayo umefanya (uk. 57).

Hapa maneno ambayo hayakustahili kutumiwa ni kama ‘wageni’ lililorudiwa ‘na kusahihisha makosa yoyote ambayo umefanya’. Kiingereza hicho ‘not only to ask them to sign on the book..’ ...si sahihi.

## **Uzidishaji S8**

### **1. Kiingereza:**

Natural trees grow without any care, however, their survival rate is generally very low and unstable (pg. 54).

### **Kiswahili:**

Miti ya pori inamea na kukua bila utunzaji wowote lakini hata hivyo tumaini la miti hii kukua huwa ni dogo sana kwani kustawi kwa miti hii hakuwezi kubashiriwa (uk. 59).

Hapa maneno ‘kustawi kwa mti huu hakuwezi kubashiriwa’ ni ya ziada. Uziada huu huenda ulisababishwa na lile lengo la kurahishisha mawasiliano kuhusu upandaji wa miti. Pengine tafsiri mwafaka ingekuwa ‘miti ya asili hukua bila utunzaji wowote ila kiwango cha kuendelea kukuwa hua ni ndogo na isiyo imara.

### **2. Kiingereza:**

Planting holes must be ready in time waiting for the rain and then the seedlings (pg. 54).

### **Kiswahili:**

Mashimo ya kupanda miche hii ni sharti itayarishwe mapema na kuachwa huku ikiongonja miche kupandwa majira ya mvua yajapo (uk. 59).

Hapa maneno haya ‘kuachwa huku ikingoja miche kupandwa majira ya mvua yajapo’ ni tafsiri refu sana kuliko yale maneno yaliyotumiwa. Maneno ‘ingojee mvua na miche’ yanatosha tu kutafsiri maneno hayo. Pia neno ‘ikingoja’ si sahihi kisarufi.

### **3. Kiingereza:**

If there are bushes or grasses around your planting site, clear them before in order not to disturb the digging process and also prevent the competition between seedlings to be planted on moisture and sunshine (pg. 54).

### **Kiswahili:**

Kukiwa kutakuwepo na vichaka au nyasi katika lile eneo ambalo unataka kupanda miche, fyeka kwanza ili shughuli ya uchimbaji wa mashimo iendelee bila pingamizi (uk. 59).

Hapa maneno haya; ‘competition between seedlings to be planted on moisture and sunshine’ ni ya ziada tena hayakutafsiriwa kwani ina dhana ya kung’ang’ania unyevunyevu na jua.

### **4. Kiingereza:**

Throwing the waste water into planting holes is also a good idea (pg. 54).

### **Kiswahili:**

Ni wazo jema kumwaga yale maji yasiyotumika, kama yale ya kutoka jikoni (uk. 60).

Hapa maneno ‘kama yale ya kutoka jikoni’ ni ya ziada.

**5. Kiingereza:**

..using boxes or bags are recommendable especially when the planting site is far (pg. 55).

**Kiswahili:**

Utumiaji wa chondo, misanduku na mifuko ni njia moja inayopendekezwa kusafirisha miche kama eneo la upandaji halipo karibu (uk. 60).

Hapa matumizi ya neno 'chondo' ni la ziada tena si neno la Kiswahili.

**6. Kiingereza:**

The bottle should be buried into the soil so that only a quarter of remain above the surface. 0.75 or one litre bottle is recommended (pg. 57).

**Kiswahili:**

Robo tatu ya chupa isifunikwe udongoni na ni robo tu ya chupa ndiyo itabakia juu ya ardhi. Chupa ya lita 0.75 (kwa mfano, ile chupa ya maji ya machungwa ya treetop) ndiyo inayopendekezwa (uk. 62).

Katika mfano huu, maneno ‘kwa mfano, ile chupa ya maji ya machungwa ya treetop’ ni ya ziada, pia maneno ‘robo tatu ya chupa isifunikwe udongoni ni ukanushaji wa maneno, ‘the bottle should be buried’.

**7. Kiingereza:**

This method is used where the rainfall is very scarce (pg. 57).

**Kiswahili:**

Aina hii ya kuzuia maji ya mvua haswa hutumiwa katika sehemu kame ambako mvua ni haba sana (uk. 63).

Hapa maneno ‘kuzuia maji ya mvua haswa katika sehemu kame’ ni ya ziada.

**8. Kiingereza:**

The soil surface of the planting holes is covered with some materials to avoid evaporation (pg. 57).

**Kiswahili:**

Ili kuzuia na kupunguza kiasi cha maji yanayonyaushwa na jua au upepo, mashimo yaliyopandwa miti hufunikwa na majani, mawe, nyasi, na matawi (uk. 63).

Hapa maneno ‘na kupunguza’, ‘jua au upepo’, ‘majani, mawe, nyasi na matawi’ yote ni ya ziada.

**9. Kiingereza:**

A game moat of 6 feet width by 6 feet depth surrounding the planting area may scare them off. However, it is not very realistic to construct it because the workload is too much for individual farmers or their groups (pg. 59).

**Kiswahili:**

Mtaro wa kuwazuia wanyama wa pori wa kina cha futi sita na upana wa futi sita kuzungukia eneo la miti ndio njia nzuri zaidi kwa kuwazuia wanyama wa pori. Lakini hata hivyo mtaro kama huu una kazi nyingi kwa mkulima binafsi au vikundi vya miradi ya maendeleo kwa vile gharama ni ya juu (uk. 64).

Katika mfano huu, maneno ‘wanyama wa pori’ na ‘miradi ya maendeleo kwa vile gharama ni ya juu ni ya ziada.

**10. Kiingereza:**

Field mice/rats attack the seedlings in the nursery but rarely in the field (pg. 59).

**Kiswahili:**

Panya siyo tu hula miche ya miti ikiwa kwenye bustani kwani pia hushambulia miti ikiwa shambani lakini hii ni nadra (uk. 65).

Hapa maneno ‘ya miti’ ni ya ziada. Ujumbe katika MC haukutofautisha neno ‘*seedlings*’ kama ni miche ya miti au mmea mwingine wowote.

**Uzidishaji S9**

**1. Kiingereza:**

Depending on climatic and other conditions, many different types of fruit trees have been planted, e.g. citrus, mangoes, pawpaws, guavas, bananas, etc. (pg. 61).

**Kiswahili:**

Kutegemea na hali ya hewa na mahitaji ya mmea, aina nyingi ya matunda imepandwa katika sehemu za mashambani kama vile machungwa, pai pai, maembe, ndizi, mapera na kadhalika (uk. 67).

Katika mfano huu, maneno ‘katika sehemu za mashambani’ ni ya ziada. Hii hoja ya mahali pa kupandwa imetokea katika ML na haipo katika MC. Ni katika juhudi za kutoa ufafanuzi zaidi.

**2. Kiingereza:**

Merits of fruit trees are; can be started from small scale (even only a tree!) while other crops require certain size of lands (pg. 61).

**Kiswahili:**

Mitunda inaweza kuanzishwa na mkulima hata awe mdogo vipi kwa vile hata mti mmoja unatosha sehemu ya ardhi inayohitajika ni ndogo ikilinganishwa na mimea mingine (uk. 67).

Hapa maneno ‘unatosha sehemu ya ardhi inayohitajika ni ndogo’ hayakustahili kuwa katika tafsiri kwani hayakuwa katika MC.

**3. Kiingereza:**

Control; destroy crop residents (pg. 63).

**Kiswahili:**

Jinsi ya kuzuia alama hizi; mimea au sehemu za mimea zilizobakia ziharibiwe au kuchomwa (uk. 69).

Hapa maneno matano ‘sehemu za mimea zilizobakia ziharibiwe’ yametosha tu badala ya kutumia maneno hayo mengi.

**4. Kiingereza:**

Hamlin; grows between 0 and 1,500 m. Seedless variety (pg. 63).

**Kiswahili:**

Mchungwa huu hukuzwa katika maeneo ya nyanda za chini kuanzia usawa wa bahari hadi maeneo ya miinuko ya juu ya hadi mita 1,500 (uk. 70).

Hapa maneno mengi zaidi ya Kiswahili yametumika kulingana na yale yaliyotumiwa kwa Kiingereza.

**5. Kiingereza:**

Hass; vigorous grower and bearer of black fruits. Propagates well (pg. 67).

**Kiswahili:**

Aina hii ya avocado inakua kwa haraka na huzaa matunda meusi. Aina hii ya avocado pia huwa na uzalishaji mzuri (uk. 75).

Hapa maneno mawili ‘*propagates well*’ yametafsiriwa kama ‘aina hii ya avocado pia huwa na uzalishaji mzuri’ na huu ni uzidishaji.

**6. Kiingereza:**

Select healthy, egg-sized seeds and plant them in boxes or seed beds (pg. 67).

**Kiswahili:**

Chagua mbegu bora yenye ukubwa wa yai kisha panda katika bustani ya miche au masanduku ya miche (uk. 75).

Maneno ‘bustani ya’ hayakustahili kuongezwa na hii ni uzidishaji katika ML.

**7. Kiingereza:**

Pruning - initial pruning may be done to give the tree a good shape (pg. 67).

**Kiswahili:**

Kupagua au kuchenga kwa kwanza kwa mitunda ya avocado huwa na dhamira ya kutoa umbo zuri kwa miti hii (uk. 75).

Matumizi ya maneno ‘kuchenga’ na ‘mitunda ya avocado’ ni kuzidisha idadi ya maneno. Hapa watafsiri wanauia kutoa ufafanuzi zaidi na kuhusisha hoja na ‘mitunda ya avocado’.

**Uzidishaji S10****1. Kiingereza:**

Grafting is the uniting of two separate structures, for example, the union of a stem to a root or the union of two stems (pg. 71).

**Kiswahili:**

Kupandikiza (kupanda chipukizi katika mti usio wake) ni kuunganisha shina kwa mzizi au kuunganisha mashina mawili ya mti aina fulani (uk. 80).

Hapa maneno ‘kupanda chipukizi katika mti usio wake’ ni ya ziada. Ni katika juhudi za kutoa ufafanuzi zaidi wa neno ‘*grafting*’ ni ‘kupandikiza’.

**2. Kiingereza:**

Reasons for grafting and budding (pg. 71).

**Kiswahili:**

Sababu za kuchipua na kupandikiza miti ambayo ni bora zaidi (uk. 80).

Katika mfano huu, maneno ‘miti ambayo ni bora zaidi’ ni ya ziada. Hapa watafsiri wamezidisha maneno tena kwa kuhusisha dhana hizi za ‘*grafting*’ (kupandikiza) na ‘*budding*’ (kuchipua) na miti.

**3. Kiingereza:**

Root stocks are chosen on the basis of their adaptability to various soils and soil conditions, compatibility with different scions (pg. 73).

**Kiswahili:**

Mashina asili huchaguliwa kutegemea uwezo wao wa kustahimili udongo wa aina fulani, magonjwa yatokayo udongoni, kupatana na mashina tofuati ya kupandikiza (uk. 82).

Maneno haya ‘magonjwa yatokayo udongoni’ yameongezwa, badala yake maneno hali tofauti za udongo yangefaa zaidi. Pameonekana kufanywa hivyo kwa kukosa msamiati mwafaka.

**Uzidishaji S11****1. Kiingereza:**

Agroforestry as the name implies, simply means the integration of the two concepts, agriculture (agronomy) and forestry (pg. 76).

**Kiswahili:**

Sura hii itajadili kilimo cha mimea na misitu. Kilimo hiki huunganisha wazo la mimea shambani ikichanganyika na misitu katika shamba moja (uk. 85).

Hapa maneno ya ziada yametumiwa kwa mfano; ‘sura hii itajadili kilimo cha mimea na misitu’, tafsiri ya neno ‘*agroforestry*’ inastahili kuwa kilimomseto, na sio maneno hayo mengi yaliyozidishwa. Sababu za kufanya hivi inaweza kuwa ukosefu wa msamiati na istilahi ‘kilimomseto’.

**2. Kiingereza:**

On exhaustion, this land was let to lie idle and for natural re-generation to occur for a number of years while land users use other parcels of land and later to return to this same land (pg.).

**Kiswahili:**

Shamba hili lenye kichaka au msitu liliachwa hivi na mkulima huendelea kulima sehemu zingine za shamba kukuza mimea ya chakula (uk. 85).

Hapa maneno ‘kukuza mimea ya chakula’ ni ya ziada, tena pana maneno hayakutafsiriwa: ‘*for natural regeneration to occur for a number of years*’, pengine kwa kukosa msamiati mwafaka.

**3. Kiingereza:**

The selection of tree species depends on the purpose, intended end-use and the services that the trees offer to the farmers as well as crops to be cultivated, and also land availability (pg. 76).

**Kiswahili:**

Miti hii ni lazima itazamwe kutokana na manufaa itakayotea mkulima, kwa mfano miti hii itatumiwa kwa shughuli gani na huduma miti itamtotea mkulima na mimea mingine ya vyakula shambani (uk. 85).

Hapa maneno ‘manufaa itakayoleta mkulima’ na ‘ya vyakula’ ni ya ziada. Uzidishaji huu umetokana na ile haja ya watafsiri kuonyesha manufaa ya upandaji miti na kukidhi haja ya chakula kwa mkulima.

**4. Kiingereza:**

The agroforestry systems or the modes of planting are several and the choice of system depends on the individual’s needs on benefits to be derived, end products required, crops to be intercropped, size of the farms and the mode of farming being practised (pg. 77).

**Kiswahili:**

Aina za kilimo cha mimea na chakula ni mingi na mkulima huchagua aina fulani kutegemea na mahitaji yake binafsi. Kwa mfano mkulima akipanda mti aina fulani atafanya hivyo kulingana na haja aliyo nayo wakati. Hapo basi itamlazimu kupanda aina fulani ya mimea ya chakula ili kuchukuana na miti iliyopandwa. Ukubwa pia wa shamba utakuwa ni jambo la kufikiria (uk. 86).

Maneno ya ziada hapa ni ‘kwa mfano mkulima akipanda mti aina fulani atafanya hivyo’ na ‘hapo basi itamlazimu kupanda aina fulani ya mimea ya chakula’. Uzidishaji huu pia umetokana na mkulima tena kutaja chakula kunawavutia wapokezi wengi na kuwapa motisha ya kupanda miti.

**5. Kiingereza:**

On farm tree planting provides fodder for the animals in settled farm areas (pg. 77).

**Kiswahili:**

Upandaji wa miti shambani kwa minajili ya kutoa chakula kwa mifugo katika sehemu za mashambani ni muhimu (uk. 86).

Maneno haya ‘ni muhimu’ ni ya ziada, ijapokuwa sentensi hiyo ya MC haikukamilika, nyongeza hii ya maneno inazidisha kiasi cha habari katika ML. Watafsiri walitaka kufidia upungufu huu.

**Uzidishaji S12**

**1. Kiingereza:**

Causes of soil erosion; improper farm management like continuous cropping (cultivate a crop without fallow or crop rotation (pg. 85).

**Kiswahili:**

Usimamizi mbaya wa shamba kama vile kuendelea kupanda aina moja ya mimea ya chakula mwaka baada ya mwaka katika sehemu moja italetta mmomonyoko wa udongo (uk. 95).

Maneno haya ‘ya chakula mwaka baada ya mwaka katika sehemu moja italetwa mmomonyoko wa udongo’, ni ya ziada.

**2. Kiingereza:**

Cultivation and overgrazing on riverbanks; once the vegetation is lost on riverbanks through the cultivation or grazing, there is nothing to prevent erosion or encroachment on rivers (pg. 85).

**Kiswahili:**

Kulima na kulisha mifugo kwenye kingo za mito; kutokana na shughuli hii vichaka na nyasi zilizo kando mwa mito hukakwa ilikupatikana sehemu ya kulimwa. Hivyo basi kingo hizo huachwa wazi na mto unapofurika udongo ulio kwenye kingo hizo husafirishwa na maji. Mifugo pia hula nyasi zilizo kwenye kingo hizo za mito na hivyo kuacha sehemu hizi wazi (uk. 95).

Hapa maneno ya ziada yametumika sababu ya kutoa maelezo marefu sana ya maneno ‘encroachment on rivers’.

**3. Kiingereza:**

The function of trees in soil conservation; canopies and litters catch the rain drops or reduce their force to strike the soil surface. Water once caught will be released slowly (pg. 85).

**Kiswahili:**

Namna miti huhifadhi udongo, mvua inaponyesha, matone ya mvua huanguka kwa nguvu ma matawi na majani ya miti hupunguza nguvu za matone hayo na mvua hii hufikia udongo kwa mtiririko na hivyo basi haisababishi mmomonyoko wowote wa udongo. Majani ya miti yaliyokauka na huwa yameanguka pia hupunguza nguvu ya matone ya mvua (uk. 95).

Hapa maneno ya ziada yametokana na maelezo ya kina ya maneno ya Kiingereza, ‘*canopies and litters catch the rain drops or reduce their force to strike the soil surface*’ pia maneno *will be released slowly* umepewa tafsiri ya ‘pia hupunguza nguvu ya matone ya mvua’ ambayo yamezidisha maneno.

**4. Kiingereza:**

Where trees to be planted, on the parts of farms not suitable for crop production, for watershed and as a source of poles, firewood, etc. (pg. 85).

**Kiswahili:**

Mahali pa kupanda miti, kwenye sehemu za shamba ambazo siyo nzuri kwa kilimo cha mazao ya chakula na kwenye kingo za majini kulinda chemichemi ili miti hii iwe ndiyo chanzo cha boriti, nguzo, kuni na kadhalika (uk. 96).

Maneno ya ziada hapa ni ‘mazao ya chakula’, ‘kulinda chemichemi’ na ‘boriti’.

**5. Kiingereza:**

Windward of the farms, houses, etc. to prevent the wind erosion (windbreaks) (pg. 85).

**Kiswahili:**

Kwenye sehemu ambazo upepo hutokezeza ili kupunguza nguvu za upepo huu ili usiharibu nyumba, mimea shambani na pia usipeperushe udongo (uk. 96).

Maneno haya ‘ili usiharibu nyumba, mimea shambani na pia usipeperushe udongo’ ni ya ziada.

**6. Kiingereza:**

Soil conservation techniques, contour farming; plant the crops in lines along the contours (across the slope). On gentle slopes, this may be sufficient to slow down the surface run-off (pg. 86).

**Kiswahili:**

Kilimo cha mistari kwenye miinuko; panda mimea yako ya chakula kwa mistari kwenye miinuko (kutoka kulia kuelekea kushoto). Kwenye miinuko midogo aina hii ya kilimo cha mistari hupunguza mwendo wa maji na huhakikisha mmomonyoko wa udongo umezuiwa (uk. 96).

Maneno kama ‘mimea yako ya chakula’ na ‘na huhakikisha mmomonyoko wa udongo umezuiwa’ ni ya ziada na hayakulingana na yale ya MC.

**3.3 Muhtasari wa Matokeo ya Ubanaji na Uzidishaji**

Katika sehemu hii, matokeo ya uchambuzi wa utafiti huu yametolewa kwa muhtasari katika Jedwali 3.1. Jedwali hili linajumuisha vipengele badilifu kama ubanaji na uzidishaji. Ubanaji umetokea katika sura zote kumi na mbili za kitabu ‘*Mbinu za Utunzaji Miti katika Misitu ya Jamii*’. Ubanaji umetokea mara sitini na tatu katika sura zote 12 za kitabu kilichochambuliwa. Sura ya 9 ndiyo ina ubanaji kwa kiasi kikubwa, ikifuatwa na sura ya 12. Kiasi kidogo cha ubanaji kimetokea katika sura ya 7 na ya 10. Haya yote ni kama inavyodhihirishwa katika jedwali. Haya yanajibu swali la kwanza la utafiti katika kazi hii: ‘*Je, kuna kiasi gani cha habari ambazo zimebanwa katika ML kutoka katika MC?*’ Kipengele hiki cha ubanaji kimetumiwa kwa mara nyingi ili kuleta ushawishi wa kiasi cha habari zilizotosha tu kushauri wapokezi kuhusu utunzaji wa miti katika misitu ya jamii.

**Jedwali 3.1: Muhtasari wa kutokea kwa vipengele vya ubanaji na uzidishaji**

Sura (S)	S1	S2	S3	S4	S5	S6	S7	S8	S9	S10	S11	S12	Jumla
Ubanaji	6	6	6	6	5	3	1	7	8	2	5	7	62
Uzidishaji	0	10	0	13	7	5	5	10	7	3	5	2	67
Jumla	6	16	6	19	12	8	6	17	15	5	10	9	129

Uzidishaji ndicho kipengele kilichotokea mara nyingi miongoni mwa vipengele hivi viwili katika sehemu hii, ikiwa ni mara sitini na sita (67), ikilinganishwa na ubanaji uliotokea mara sitini na mbili (62). Hata hivyo sura ya 1 na 3 hazina habari zilizozidishwa kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 3.1. Haya yanajibu swali la pili la utafiti; *'je pana kiasi gani cha habari ambazo zimezidishwa katika ML ikilinganishwa na MC?'* Matokeo haya yanaonyesha kuwa pana ufafanuzi zaidi uliotolewa kuhusu dhana mbali mbali zaidi ya ilivyokuwa katika LC. Haya yanawezakuwa yalitumiwa ili kutosheleza kusudi la kazi hiyo ambalo lilikuwa ni kutoa ushauri kuhusu mbinu mwafaka za kitaaluma kuhusu upandaji na utunzaji wa miti.

### **3.4 Hitimisho**

Katika sura hii tumechunguza ushawishi wa kiasi cha habari kutokana na ubanaji na uzidishaji vikiwa vipengele amilifu vya tafsiri. Imebainika kuwa hivi vipengele viwili vimetokea kwa kiasi kikubwa na hivyo kuchangia katika kushawishi kiasi cha habari zinazo toka katika MC hadi ML. Kwa hivyo HL huenda isipate habari namna ambavyo wasomaji asilia walivyo ipata. Ni ung'amuzi wetu kuwa ubanaji na uzidishaji ukitokea sana, ujumbe muhimu utaathiriwa na kutohawilishwa kutoka MC hadi ML, na huenda maana inayokusudiwa kupotea.

**SURA YA NNE**  
**VIPENGELE AMILIFU VYA TAFSIRI VINAVYOPOTEZA NA KUPOTOSHA**  
**HABARI**

**4.1 Utangulizi**

Katika sura hii tulichunguza na kuchanganua vipengele amilifu vya tafsiri kama vile upotezaji na upotoshaji. Pamoja na hayo, tuligundua uwepo wa masuala ibuka katika kazi hii. Masuala hayo ibuka yanajumuisha istilahi za EM na msamiati ambao haukutafsiriwa. Ujumuishaji wa vipengele hivi amilifu vinaweza kufanikisha tafsiri yenye kusudi au malengo mahususi. Tafsiri yenyewe, "*Mbinu za Utunzaji Miti Katika Misitu ya Jamii*" ilichambuliwa ili kuthibitisha ubainikaji wa malengo haya. Malengo haya yaliegemea katika kushawishi kiasi cha habari kinachopitishwa katika mchakato wa kutafsiri kama inavyojitokeza katika toleo hili.

**4.2 Kuhusu Upotezaji**

**Upotezaji S4**

**1. Kiingereza:**

‘Trees are indispensable in human environment...and the future of human beings is closely related to trees’ (pg. 11).

**Kiswahili:**

‘Binadamu hawezi kuishi bila miti na kuishi kwa binadamu duniani kunategemea miti’ (pg. 12).

Katika mfano huu, neno ‘indispensible’ halikutafsiriwa kikamilifu. Katika tafsiri hii, mtafsiri hakutafsiri kamwe neno ‘indispensable’ na hivyo kupoteza maana ya sehemu hiyo ya sentensi. Msomaji wa ML hatapata ujumbe ambao unapatikana katika MC. *‘Trees are indispensable in human environment...’* inaleta dhana ya kuwepo kwa miti kuwa lazima katika mazingira ya binadamu. Ingawa ujumbe unapatikana katika ML inaonyesha kuwa binadamu hawezi kuishi bila miti, tafsiri hiyo inapoteza maana asilia inayopatikana katika MC. Kwa mfano, inasemekana kuwa binadamu hawezi kuishi bila chakula na makao ilhali kuna watu ambao hufunga kwa misingi ya dini bila chakula na hawafi. Pia kuna watu wengi ambao hawana makao lakini bado wako hai. Kwa hivyo kutafsiri ‘*indispensable*’ kama “hawezi kuishi bila” inaishia kupoteza ujumbe uliokusudiwa.

Vile vile kutafsiri *'the future of human beings is closely related to trees'* kama 'kuishi kwa binadamu duniani kutagemea miti' si sawa. Maana iliyokusudiwa imepotezwa kabisa na maana nyingine mpya kuibuliwa. Mtafsiri angepaswa kutafsiri sehemu hiyo ya sentensi kama 'hatma ya binadamu ina uhusiano wa karibu sana na miti'.

**2. Kiingereza:**

The first step to start a nursery is to designate a site (pg. 36).

**Kiswahili:**

Jambo la kwanza la kutiliwa maanani bustani la miche linapoanzishwa ni kutenga eneo ambalo litatumiwa kwa shughuli hii (uk. 38).

Hapa maneno *'The first step'* yametafsiriwa kama 'jambo la kwanza' na hii inapoteza ile maana ya 'hatua'. Jambo ni habari inayoongelewa au kujadiliwa. Hatua kwa upande mwingine ni tendo linalochangia kuleta mafanikio. Kwa hiyo katika muktadha wa tafsiri hii 'hatua' ingekuwa mwafaka Zaidi. Kule kutumia neno 'jambo' kumeishia kupoteza maana ambayo inapatikana katika MC lakini haipo kwenye MC. Hapa hakuna jambo ambalo lilikuwa linajadiliwa ila kulikuwa na maelekezo kuhusu tendo ambalo linafaa kufanywa ili kufanikiwa katika uundaji au uanzishwaji wa bustani ya miche.

**3. Kiingereza:**

The number and kind of essential tools depends on the scale of the nursery and number of workers (pg. 37).

**Kiswahili:**

Aina ya zana au wingi wa zana za bustani ya miche hutegemea ukubwa wa bustani au idadi ya wafanya kazi (uk. 39).

Neno *'essential'* katika mfano huu lilipotezwa na halikutafsiriwa kamwe na katika hali hii basi tafsiri haikufaulu. Huenda neno hili halikutafsiriwa kwa sababu mtafsiri alikosa kisawe cha msamiati wa LC katika LL. Ama pengine alipata maneno machache sana ambayo hayawezi kuwasilisha ujumbe kikamilifu katika MC na hivyo akaamua kuacha kutafsiri badala ya kumpotosha msomaji au kuwasilisha ujumbe finyu. Hali hii pia imechangiwa na lugha hizi mbili (Kiingereza MC na Kiswahili ML) kuwa na tofauti za kiisimu na kinasaba.

**4. Kiingereza:**

Individual farmers can start their nurseries with only their farming tools in daily use (pg. 37).

**Kiswahili:**

Wakulima binafsi wanaweza kuanzisha bustani zao za kawaida za ukulima za kila siku (uk. 34).

Hapa pana maneno yaliachwa kati ya neno ‘zao’ na ‘za’, ilitahili maneno ‘na zana zao za’ yawepo. Kukosa kutafsiri ‘*with only their farming tool*’ kunawasilisha ujumbe finyu na hivyo kupoteza ujumbe asilia. Ujumbe uliokusudiwa ina maana kamili pakiwepo zana za ukulima ambayo sasa haipo kabisa katika tafsiri. Ile dhana ya zana za ukulima imepotea kabisa na badala yake nafasi yake kuchukuliwa na shughuli za kawaida za bustani.

**5. Kiingereza:**

The time to start establishing a nursery firstly depends on the time to plant seedlings (pg. 37).

**Kiswahili:**

Wakati wa kuanzisha bustani ya miche hutegemea (uk. 39).

Katika mfano huu, sehemu ya pili ya sentensi baada ya neno ‘hutegemea’ imepotezwa, kwa hivyo maneno ‘*on the time to plant seedlings*’ hayakutafsiriwa. Katika tafsiri, mtafsiri anapaswa kuwa mwaminifu kwa lugha pokezi na vilevile kwa msomaji wa makala pokezi. Lakini inadhirika kuwa mtafsiri wa kazi hii alikiuka kanuni za tafsiri na hivyo kuishia kumsaliti msomaji wa ML ya kazi hii. Kukosa kutafsiri sehemu hiyo ya sentensi na hivyo ujumbe huo kupatikana katika Kiingereza (MC) na kukosekana katika Kiswahili (ML) ni usaliti wa tafsiri. Tafsiri hiyo inapoteza ujumbe zaidi pale ambapo inamfanya msomaji kwa mara ya kwanza ataiona sentensi ile kama ambayo haijakamilika.

**6. Kiingereza:**

As already mentioned, watering in principle should be done twice a day, one in the morning and once in the evening (pg. 40).

**Kiswahili:**

Kama ilivyoonyeshwa, unyunyizaji wa maji kwenye bustani ufanywe mara mbili kwa siku moja na mara moja tena nyakati za jioni (pg. 43).

Hapa dhana ya unyunyizaji maji asubuhi imepotezwa. Ukweli na uaminifu huweza kuzingatiwa ikiwa mtafsiri ana ujuzi wa kiisimu wa lugha mbili zinazohusika. Kwa misingi hii, katika muktadha wa tafsiri ya kazi hii, inaonekana kuwa mtafsiri wa kazi hii alipugnukiwa kwa kiasi fulani katika LL. Ikiwa msomaji wa ML angependa kutumia kazi hii pale nyumbani kuunda bustani ya miche

basi kuna ujumbe atakayokosa, na hivyo bustani yake haitanawiri inavyofaa. Yule msomaji atafuata agizo la kunyunyizia jioni bali hatanyunyizia asubuhi kwa sababu sehemu ile ya unyunyiziaji maji asubuhi imepotezwa, kinyume na msomaji wa MC. Mtafsiri katika hali hii amemsaliti mwandishi asilia na vilevile msomaji ambaye ndiye muhimu zaidi kwa kuzingatia lengo la kazi hii ni umahasisho katika jamii.

**7. Kiingereza:**

Arrange the seedlings pots in one or two lines to harden their roots (pg. 41).

**Kiswahili:**

Panga mikebe ya miche katika mstari mmoja au miwili ili kuizoesha mizizi (uk. 44).

Neno '*harden*' hapa, ambalo ni mojawapo wa istilahi maalum ya EM haikutafsiriwa ipasavyo. Kukosa istilahi linganifu husababisha kukosekana kwa ulinganifu wa kimaana. Mbali na hayo, tafsiri katika taaluma maalum kama vile EM huhitaji kuchungwa kwa maana kwani maneno ya taaluma huwa na tafsiri maalum. Hata kama maneno katika Kiingereza (MC) hayana visawe au maneno sawia katika Kiswahili (ML), kuna uwezekano wa kupata neno katika Kiswahili linaloweza kutumiwa kuelezea neno '*harden*'. Mtafsiri angejitahidi pengine kutafuta maelezo au neno la kawaida katika Kiswahili na kuitumia kwa kuipea maana ya EM. Kwa mfano lingetafsiriwa kama 'Panga mikebe ya miche katika mstari mmoja au miwili ili kuifanya mizizi kuwa ngumu'.

**8. Kiingereza:**

There are many factors which cause damage to the seedlings in the nursery. Among them, biotic factors like pests are mentioned in Chapter 5 (pg. 41).

**Kiswahili:**

Kuna namna nyingi ambazo zinaletea miche uharibifu inapokuwa kwenye bustani. Uharibifu kama huo ni ule unaotajwa katika sura ya tano (uk. 44).

Hapa upotezaji umetokea wa neno '*biotic*' ambalo halikutafsiriwa. Dhana moja kuu linalowakilishwa na neno moja katika lugha moja linaweza kuwakilishwa kwa maneno kadhaa katika lugha nyingine. Pia ni ukweli kuwa dhana isiyokuwepo katika utamduni wa Kiswahili ni vigumu kuwa na neon lake la Kiswahili. Kwa hivyo katika hali hii, badala ya kuacha kutafsiri neno '*biotic*' na hivyo kupoteza maana iliyonuiwa, mtafsiri angetumia maneno kadhaa ama maelezo ya '*biotic*' katika ML. Ukosefu wa ulinganifu katika istilahi huleta ukosefu wa ulinganifu wa maana. Pengine ni kwa sababu hii ndipo mtafsiri aliamua kutotafsiri neno '*biotic*'.

**9. Kiingereza:**

Drought is a climatic disaster which cannot be anticipated (pg. 41).

**Kiswahili:**

Kiangazi ni hali ya hewa iletayo uharibifu ambao hautarajiwi (pg. 44).

Hapa maneno '*climatic disaster*' yamepotezwa katika tafsiri kwani yalistahili kutafsiriwa kama 'mkasa wa tabia nchi'. Maana asilia katika Kiingereza ni lazima ihifadhiwe na ipatikane kikamilifu katika Kiswahili. Kufahamu maana ya kifungu cha maneno ni rahisi lakini si rahisi maana hiyo kutafsiriwa kikamilifu katika Kiswahili. Kwa hivyo ni rahisi kwa mtafsiri kutotafsiri sehemu fulani ya maana inayopatikana katika Kiingereza na hatimaye kupoteza maana iliyokusudiwa.

**Upotezaji S5****1. Kiingereza:**

Physical measures can also be taken however to make the peoples' awareness is more important and effective (pg. 43).

**Kiswahili:**

Hata hivyo hatua za kimsingi zinaweza kuchukuliwa ili kuelimisha watu juu ya uharibifu ambao husababishwa na binadamu (uk. 46).

Maneno '*physical measures*' hayajatafsiriwa na yamepotezwa. Tafsiri ni kuhamisha maana kutoka LC hadi LL. Utartibu wa tafsiri ni kutafsiri hatua kwa hatua na wakati huo huo mtafsiri akizingatia maana. La muhimu kuhamishwa huwa si istilahi bali maana ndiyo huhamishwa hadi LL na lazima ihamishwe kwa udhabiti wake. Kukosa kutafsiri neno au kifungu cha maneno inawanyima wasomaji ML fursa ya kuelewa maana iliyokusudiwa na mwandishi wa MC. Mtafsiri alipokosa istilahi linganifu basi angejitahidi angalau kuhamisha maana ili ujumbe wote usipotezwe.

**Upotezaji S6****1. Kiingereza:**

List the necessary materials and tools, and think about the procurement whether your budget allows to buy or not (pg. 48).

**Kiswahili:**

Ukubwa wa bustani hasa utategemea kupatikana kwa vifaa na zana za kazi na pia wafanyakazi na ni kutokana na haya ndipo ukubwa wa bustani ya miche utakubaliwa (uk. 52).

Hapa hoja zinazohusu; '*necessary materials and tools*', '*budget*' na '*procurement*' hazikujumuishwa. Kukosa kutafsiri neno au kifungu cha maneno, hupoteza maana iliyokusudiwa. Hali hii huenda ilisababishwa na dhana hizo kupatikana katika LC ilhali dhana hizo hizo

hazipatikani katika LL. Mtafsiri anaweza akatafsiri dhana zinazokaribua tu lakini hazina uhusiano wowotw. Hata hivyo katika hali hii mtafsiri hakujaribu kutumia dhana inayokaribiana na ile inayokusudiwa na hivyo kupoteza na hata kuua sehemu ile ya kazi hii.

**2. Kiingereza:**

Consult the nearby foresters and/or extension staff if available (pg. 48).

**Kiswahili:**

Unaweza kupata ushauri kutoka kwa maafisa wa misitu au maafisa wa nyanjani walioko karibu kwa mawaidha zaidi (uk. 52).

Katika mfano huu; kule kutafuta ushauri wa maafisa wa misitu na wa nyanjani haukutajwa bali kule kuweza kupata ushauri ndio umetajwa katika tafsiri. Tafsiri inapaswa kuwasilisha kwa hadhira lengwa maana na ujumbe ulio sawa na ule uliowasilishwa na MC kwa hadhira chanzi. Kazi hii ya EM ilifanywa kwa lengo maalum na hivyo tafsiri ya kazi hii lazima pia itimize lengo hilo. Kutotafsiri kifungu cha maneno kunapoteza ujumbe uliokusudiwa na hivyo lengo ya kazi hii ya elimu msitu haiafikiwi ilivyotarajiwa.

**3. Kiingereza:**

If any technical or any other problems are encountered, consultation is available from the near-by forester and/or extension staff (pg. 49).

**Kiswahili:**

Ikiwa matatizo yoyote ya kiufundi yatapatikana, mashauri ni lazima yafanyike na maafisa wa misitu au maafisa wa nyanjani walioko karibu (uk. 53).

Katika mfano huu, maneno ‘*consultation is available*’ yametafsiriwa kama ‘mashauri ni lazima yafanyike’ ambayo haileti hiyo maana ya kuweza kupatikana na si lazima. Ushikamano wa maana na ushikamano wa matini husaidia kuafikia lengo la kutafsiri kazi fulani. Kwa hivyo mtafsiri hujitahidi kuzalisha athari sawa kwa hadhira lengwa na ile iliyozalishwa na matini asilia kwa wasomaji wa LC. Hata hivyo sehemu fulani inapokosa kutafsiriwa basi ile athari inayonuiwa kuzalishwa haitapatikana.

**4. Kiingereza:**

Make necessary record of the nursery activities and all these records should be kept with the foreman (pg. 49).

**Kiswahili:**

Shughuli zote zinazotekelezwa katika bustani ni sharti ziandikwe na kuwekwa na msimamizi wa bustani kama kumbukumbu (uk. 53).

Tafsiri ya maneno haya imetoa dhana ya shughuli ambazo sharti ziandikwe, kinyume na yalivyotolewa kama maagizo katika MC. Kwa hiyo, hadhira ya lugha lengwa huweza kupata maana na ujumbe tofauti na hadhira chanzi. Kutokana na tafsiri hii kupoteza maana inafanya hadhira lengwa kupata ujumbe ambao si sahihi kuhusu elimumsitu.

**5. Kiingereza:**

He/she should be able to keep good relation with other people and be able to lead them (pg. 49).

**Kiswahili:**

Ni sharti msimamizi wa bustani aweze kuelewana na wafanyi kazi wote katika bustani na kuwa na tabia za kiongozi (uk. 54).

Hapa MC imeeleza mahitaji ya msimamizi kuwa na mahusiano mema na watu wengine sio tu wafanya kazi kama ilivyojitokeza katika ML. Hali hii inaonyesha ukosefu wa ushikamano wa maana baina ya MC na ML. Kukosekana kwa ushikamano huo unasababisha maana kupotea katika tafsiri na kuleta utata katika maana ya halisi ya maneno.

**Upotezaji S11****1. Kiingereza:**

To prevent this competition, it is recommended to cut the side-roots of trees growing towards (pg. 79).

**Kiswahili:**

Ili kuzuia mashindano haya kati ya mimea ya chakula na miti inapendekezwa mizizi ya kando inayomea ikielekea kwenye mimea ya chakula (uk. 89).

Hapa maelezo ya mizizi ya kando hayajakamilika. Kutotafsiri dhana nzima iliyoachwa, inapoteza ujumbe wa MC. Taarifa muhimu ya namna mimea inapaswa kusaidiwa kupata chakula imeachwa kabisa pasi kutafsiriwa katika ML. Kupoteza kifungu hiki cha maneno kulifanya hadhira lengwa kukosa taarifa muhimu ambazo hadhira chanzi walipata. Pia athari zinazotarajiwa baada ya msomaji kusoma ML zinapotea kinyume na ilivyokusudiwa katika MC.

### 4.3 Kuhusu Upotoshaji

#### Upotoshaji S1

Uwepo wa habari ambazo ujumbe wake ulipotoshwa katika ML ulichunguzwa katika utafiti huu. Hapa maneno, virai na istilahi mbalimbali zilionekana kutolewa tafsiri ambayo haikulingana na maana yake inayojulikana na kudokezwa katika MC. Mifano imetolewa hapa chini.

##### 1. Kiingereza:

Trees have associated with human beings ever since our first ancestors appeared on earth, deriving our livelihood from trees in terms of food, shelter, firewood, etc. (pg. 8).

##### Kiswahili:

Miti imekuwemo tangu zama za mababu zetu wa kwanza duniani na walitumia miti kama chakula, kuni za kupikia, kujipatia joto, kujenga vibanda na kadhalika (uk. 8).

Katika mfano huu, dhana ya miti kuwa na mahusiano na binadamu imejitokeza katika Kiingereza na haikutajwa katika Kiswahili. Mtafsiri alichukua hatua hiyo pengine kwa kusudi la kustawisha maana ya ujumbe unaowasilishwa katika ML. Huenda alifanya hivi kimakusudi au kimakosa. Hata hivyo katika muktadha huu ni haiwezi kusemwa hakika ikiwa mtafsiri alipotoshwa hadhira lengwa kimakusudi au kwa makosa. Kwa sababu yoyote iliyopelekea upotoshaji huu athari inayotarajiwa kwa hadhira lengwa huwa si iliyokusudiwa na kupatikana katika hadhira chanzi.

##### 2. Kiingereza:

Before sedentary agriculture started, wild plants including trees had given people a large percentage of their diet such as fruits and nuts (pg. 8).

##### Kiswahili:

Kabla ya kilimo cha sasa kuanza, mimea ya pori ikiwa pamoja na miti ilitokea kuwa ndicho chakula kikubwa cha babu zetu.

Mfano huu unataja kilimo cha kuishi mahali pamoja kinajitokeza katika Kiingereza hali ambayo haijajitokeza katika Kiswahili kwa hivyo neno ‘*sedentary*’ halikutafsiriwa. Hii inaonyesha jinsi kulivyo na haja ya kuchagua neno sahihi. Uchaguzi wa maneno katika ML yanayosadifu maelezo yanayopatikana MC ni muhimu na inahitaji kuzingatiwa. Hata hivyo ni muhimu kusesitiza kwamba kila lugha ina makundi mengi ya maneno yanayoelezea maana kuu fulani na si kila moja ya maneno hayo linaweza likapata kisawe chake katika lugha nyingine. Hii ni kwa sababu makundi hayo pia huwa yamejikita katika misingi ya tamaduni za lugha hizo.

### **3. Kiingereza:**

There are many benefits from trees, some of which are tangible while others are intangible (pg. 8).

### **Kiswahili:**

Kuna manufaa mengi yanayopatikana kutoka kwa miti na ambayo mengine yanaonekana na mengine hayaonekani (uk.8).

Mfano huu umetaja manufaa ya miti yasiyoweza kugusika katika Kiingereza ‘*intangible*’ yametajwa kama ‘kuonekana’ kwa hivyo dhana hiyo haikutafsiriwa. Lugha huweza kutofautiana katika ubainisho na hivyo kufanya dhana mahususi kwa lugha kukosa kisawe chake au kuwa ngumu kutafsiri katika lugha nyingine. Ni muhimu kusisitiza kuwa hata kama mada itatokea kuwa ngumu, kwa maana ya kuhusika na masuala dhahania au yasiyozoeleka, ni vema mtafsiri ajaribu awezavyo kutumia maneno ya kawaida yaliyozoeleka.

### **4. Kiingereza:**

Trees are a source of timber which is used for many purposes, e.g. building houses, bridges and other architectural structures (pg. 8).

### **Kiingereza:**

Mbao hutoka kwa miti na matumizi ya mbao ni mengi, kwa mfano kujenga nyumba, daraja na vifaa vingine vya kiufundi (uk. 8).

Hapa miti inatajwa kama chimbuko cha mbao katika nakala ya Kiingereza ilhali mbao inaelezwa kama hutoka kwa miti katika matini ya Kiswahili. Katika tafsiri hata neno moja peke yake linaweza kutafsiriwa kwa maneno mbalimabli tofauti katika lugha nyingine. Hii ni kwa kuwa dhana moja kuu linalowakilishwa na neno moja katika lugha moja (MC) linaweza kuwakilishwa kwa maneno kadhaa katika lugha nyingine (MC). Kwa hiyo mtafsiri wa kazi hii iwapo alikosa neno moja kwa Kiswahili la kuwasilisha dhana ‘sedentary’ basi angetumia ufafanuzi wa maana ya neno hiyo. Iwapo hilo lingefanywa basi wasomaji wa ML hawatapotoshwa na watapata ule ujumbe ambao wasomaji wa MC wamepata.

### **5. Kiingereza:**

Government forests are hard pressed to provide posts and poles needed, and it would be cheaper and more convenient if they were produced on the farms or near the users (pg. 8).

**Kiswahili:**

Misitu ya serikali inakatwa kwa wingi ili kutoa nguzo na mihimili yanayotakikana na litakuwa ni jambo la kufaa kama mihimili na nguzo zingetolewa kwenye mashamba ya wakulima binafsi (uk. 8).

Katika mfano huu, ni wazi kuwa matini ya Kiingereza inaonyesha ugumu wa misitu ya serikali kutoa boriti ilhali ya Kiswahili inaeleza tu juu ya ukataji. Kuna maneno ambayo yamejikita katika lugha na utamaduni mahususi na huenda hayaeleweki katika lugha na utamaduni mwingine. Lugha inayolengwa huenda haina maneno yanayopatikana katika LC au vitu vinavyowakilishwa na maneno katika MC ni tofauti na vile vinavyowakilishwa katika ML. Katika hali hii mtafsiri anapaswa kuelewa lugha lengwa na utamaduni wake na kubaini ikiwa visawe vya maneno yaliyotumika katika MC yanaweza kupatikana katika ML. Bila kufanya hivyo msomaji wa ML huwa amepotoshwa kama ilivyo katika muktadha huu.

**6. Kiingereza:**

One of the major roles of trees in the rural areas is to provide fuel for cooking and heating (pg. 8).

**Kiswahili:**

Umuhimu mkubwa wa miti ni ule wa nishati ya kupikia na kutoa joto. (uk. 8).

Tafsiri ya hoja hii ya kuwa faida ya kupika na kutoa joto pekee ndiyo faida inayotajwa katika ML na haijaitokeza kama mojawapo wa nafasi muhimu.

**7. Kiingereza:**

As already pointed out, trees and their by-products are essential for rural life and have great economic value to rural households both directly and indirectly (pg. 9).

**Kiswahili:**

Kama vile tayari imeshaelezwa hapo juu, miti na bidhaa ambazo hupatikana kutoka kwa miti ni vitu vya lazima katika maisha ya mashambani na wakati huo huo huwa ni muhimu kiuchumi katika uendeshaji wa maisha mashambani (uk. 11).

Hoja ya kiwango cha juu kiuchumi cha miti na bidhaa zake kinastahili kujitokeza katika Kiswahili kama ilivyotajwa katika Kiingereza. Katika tafsiri ni muhimu kuwepo kwa ulinganifu wa visawe vya MC na ML. Ulinganifu hasa huegemea maana na ujumbe wa MC na ML. Mtafsiri anapaswa kuteua maneno mwafaka yanayolingana na maana na ujumbe wa MC. Pasi kuangazia ule ulinganifu wa ujumbe na maana, upotoshaji hutokea ambapo msomaji wa MC na ML wanapata maana na ujumbe usiolingana au kufanana.

### **8. Kiingereza:**

The Ministry of Environment and Natural Resources employs over 30,000 workers, most of them dealing directly with tree growing, protection and management of the tree resources, Non-governmental Organisations, e.g. Green Belt Movement, Care Kenya, etc. are employees in their endeavour to grow trees (pg. 11).

### **Kiswahili:**

Wizara ya Mazingira na Mali ya Asili huajiri zaidi ya wafanya kazi 30,000 wengi wao wakiwa wanasaidia kwa ukuzaji wa miti moja kwa moja, (uk. 11).

Katika mfano huu, hoja moja tu ya ukuzaji miti inajitokeza, zile nyingine mbili za kuipa miti kinga na usimamizi wake haukujitokeza katika tafsiri. Ushikamano wa maana na ujumbe unahitajika katika MC na ML ili kuwezesha na kufanikisha mawasiliano. Kukosekana kwa ushikamano katika MC na ML kunasababisha upotoshaji. Upotoshaji huu unatokea kwa sababu kukosekana kwa ushikamano wa MC na ML kunafanya matini hizi kuwa matini mbili tofauti. Maana na ujumbe unaopatikana katika MC sio ule unaopatikana katika ML kwa hivyo hizo ni matini mbili tofauti.

### **Upotoshaji S2**

#### **1. Kiingereza:**

Leaves, twigs and seeds are good fertilizer containing nitrogen and other important materials. Leaves are eaten by goats (pg. 16).

#### **Kiswahili:**

Majani, vijiti na mbegu za mti huu huwa na mbolea nzuri yenye nitrogen na vifaa vingine vingi, majani huliwa na mbuzi (pg. 17).

Katika mfano wa 1 hapo juu, neno ‘*nitrogen*’ limebebwawa kama ilivyo kwa Kiingereza, pengine lingetoholewa. Neno ‘*nitrogen*’ halikutafsiriwa.

#### **2. Kiingereza:**

Some medicine and insect `repellent` are extracted from leaves and seed (pg. 16).

#### **Kiswahili:**

Madawa mengine na madawa ya kuua wadudu hutolewa kutoka majani ya mti huu (uk. 17).

Hapa katika mfano huu wa 2, neno `*repellent*` halikupewa tafsiri mwafaka, pengine neno `*kufukuza*` lingefaa zaidi. Mtafsiri anapotafsiri anapaswa kuteua maneno yaliyo na uhusiano katika MC na ML hivi kwamba maneno hayo katika ML yakitafsiriwa kwa MC maana inayojitokeza ni ile ile. Kuna baadhi ya maneno au dhana zinazopatikana katika lugha moja na hazimo wala hazifahamiki katika

utamduni mwingine. Mtafsiri anapaswa kuchagua misamiati inayofanana kimaana katika matini zote mbili. Iwapo maneno yaliyoteuliwa yanaleta maana sawa basi tafsiri ile itakuwa imefaulu. Hata hivyo tunaona hakuna uhusiano wowote wa karibu au wa mbali kati ya maneo ‘repellant’ na kuua na hivyo kunatokea upotoshaji kwa kiasi fulani.

**3. Kiingereza:**

Oil is also extracted from seeds on commercial basis (pg. 16).

**Kiswahili:**

Mafuta pia hupatikana kutoka kwa mbegu za mti huu kwa kiwango cha biashara (uk. 17).

Katika mfano wa 3, neno ‘extracted’ limetafsiriwa kama ‘hupatikana’ neno ambalo halileti maana hiyo ya ‘kudondoa’. Makosa katika uteuzi wa maneno yanayolingana katika MC na ML wakati wa kutafsiri matini ya elimu misitu yanazua matatizo katika kufahamu na kuelewa maana iliyokusudiwa na MC. Kwa hivyo makosa ya uteuzi wa maneno yanayolingana, wasomaji wa ML hushindwa kupata maana asilia na sahihi kwa sababu msamiati ulioteuliwa si sahihi.

**Upotoshaji S4**

**1. Kiingereza:**

The main obstacle to tree planting activity in the rural area has been unavailability of tree seedlings due to lack of nearby nurseries (pg. 36).

**Kiswahili:**

Kizuizi kikubwa katika shughuli za upandaji wa miti katika sehemu za mashambani ni kwamba miche ya miti imekuwa vigumu kuipata.

Maneno ‘*lack of nearby nurseries*’ yamepotezwa kwani hayakutajwa katika tafsiri. Kupoteza maneo hayo yanaathiri maana na uelewa wa maana kwa hadhira lengwa. Katika hali hii, taarifa ya MC ambayo imekusudiwa kutolewa kwa hadhira lengwa hupotea na hivyo hadhira lengwa hupata dhana na maana tofauti na ile inayopatikana katika MC.

**2. Kiingereza:**

Water availability throughout the year (near the river, near your kitchen to utilize wasted water) (pg. 36).

**Kiswahili:**

Maji yanapatikana mwaka wote mzima kwa bustani (karibu na jikoni lako ili maji ambayo hutumii yamwagwe kwenye bustani la miche na pia karibu na mto (uk. 38).

Maneno haya; ‘maji ambayo hutumii yamwagwe kwenye bustani ya miche’ yametumiwa badala ya ‘wasted water’, jambo ambalo limezua upotoshaji kwani ‘wasted water’ ni maji yale yameshatumiwa na kustahili kumwagwa. Mtafsiri hujaribu kuzalisha athari sawa kwa wasomaji wa ML na ile iliyozalishwa na matini asilia kwa wasomaji wa MC. Hili hufanywa ili kuhakikisha kuwa kuna ushikamano wa maana na ushikamano wa matini. Hata hivyo maneno yanapopotezwa huwa panatokea upotoshaji na hivyo athari iliyokusudiwa kwa hadhira haipatikani.

### **3. Kiingereza:**

If there is no nearby water source like rivers or ponds, a water tank or a drum to keep water is necessary (pg. 37).

### **Kiswahili:**

Kama hakuna maji yaliyoko karibu kama vile ya mito au visima, tangi la maji au pipa la maji ni muhimu ili kuhifadhia maji (uk. 39).

Neno ‘*necessary*’ limetafsiriwa kama ‘muhimu’, na hii imeleta upotoshaji. Hapa kuna upotevu wa maana na ujumbe wa MC katika ML. Tafsiri hulenga kuzalisha athari sawa katika ML na ile ya MC. Hata hivyo wakati mwingine vipengele vya maana huathiriwa kwa kupotezwa na hivyo kuzua kukosekana kwa ushikamano wa MC na ML kama inavyodhihirika katika mfano huo hapo juu. Kukosekana kwa ulinganifu katika MC na ML na hivyo kuzua upotoshaji ni tatizo katika kazi ya tafsiri.

### **4. Kiingereza:**

In large nurseries, considering the work of efficiency, the use of watering cans, wheelbarrows should also be considered (pg. 37).

### **Kiswahili:**

Katika bustani za miche utumiaji wabirika za kunyunyizia maji, wilibaro na kadhalika ni sharti ziwekwe kwenye orodha ili kuhudumia bustani barabara (uk. 39).

Neno ‘*considered*’ hapa limeachwa na halikutokea katika tafsiri. Kukosa kutafsiri neno hilo basi linafanya taarifa ya MC kuwa tofauti na taarifa na ujumbe katika ML. Hivyo basi, hadhira ya lugha lengwa huweza kupata maana na ujumbe tofauti na hadhira chanzi. Kupoteza maana hufanya hadhira lengwa kupata ujumbe usiowiana na ujumbe wa MC.

### **5. Kiingereza:**

It is recommended to collect soil three months prior to the potting so that the organic matter can decay, and the seeds of weeds germinate and can be removed easily (pg. 37).

**Kiswahili:**

Inapendekezwa kukusanya udongo miezi mitatu kabla ya kuanza shughuli za kupandikiza miche kwenye mifuko ili viungu vya mimea vioze na hii itarahisisha mbegu za kwekwe kuota na kung'olewa kwa urahisi (uk. 40).

Maneno '*organic matter can decay*' yamepotezwa na hayakutokea kwenye tafsiri. Kutokana na mfano huu, hakuna ushikamano wa maana kati ya MC na ML. Kukosekana kwa ushikamano huo kunasababisha maana ya dhana ya msingi kupotea katika tafsiri na kuleta utata katika maana ya MC na ML. Kwa hiyo hadhira lengwa itashindwa kupata dhana na maana asilia ya maneno haya.

**6. Kiingereza:**

Hold the leaves of seedlings and insert a dibble underneath the root system of the seedlings to loosen the soil (pg. 39).

**Kiswahili:**

Shika majani ya miche na kisha chimba shimo karibu na miche ili kulegeza udongo (uk. 42).

Maneno '*insert a dibble*' hayakujitokeza katika tafsiri. Kilicho muhimu katika tafsiri ni maana. Tafsiri huhamisha maana kutoka lugha chanzi hadi lugha pokezi. Tafsiri zinazozingatia maana hujitahidi kuwasilisha maana ya MC katika hali halisi katika ML. Kukosa kutafisiri maneno '*insert a dibble*' kunasababisha kupotezwa kwa maana fulani iliyokusudiwa katika MC. Kupotosha maana huishia kupotosha yaliyomo kwenye ML.

**7. Kiingereza:**

Hardening up is to expose the seedlings to harsh conditions to make them so that they will be able to survive under harsh climate in the field after planting out (pg. 41).

**Kiswahili:**

Kuizoesha miche hali ya hewa ni kule kuiacha katika hali ya hewa ya kawaida ili kuimarisha na kuwa na nguvu ili iweze kukua katika hali ya hewa ya huko nyanjani baada ya kupandikiza (pg. 43).

Maneno '*hardening up*' hayakutafisiriwa na hivyo hayakutokea katika tafsiri. Ikiwa wazo lipo katika MC lakini halipo katika ML basi hakutakuwa na ulinganifu wa istilahi. Katika hali hii huenda dhana hii haikutafisiriwa kutokana na ukosefu wa istilahi inalingana na dhana hiyo kimaana katika lugha ya Kiswahili. Hali hii hata hivyo inasababisha upotoshaji wa maana na ujumbe na hadhira lengwa haipati maana na ujumbe uliokusudiwa na unaopatikana katika MC.

## Upotoshaji S5

### 1. Kiingereza:

Seedlings are delicate and susceptible to attacks by various pests and diseases as well as some meteorological conditions (pg. 43).

### Kiswahili:

Miche huwa ni nyororo na hivyo kuna uwezekano wa kuharibiwa na wadudu na magonjwa aina nyingi. Hali ya hewa pia huharibu miche (uk. 46).

Hoja kutokana na maneno ‘*delicate*’ na ‘*meteorological*’ zimepotoshwa. Upotoshwaji wa maana na ujumbe huleta utata katika hadhira lengwa kuelewa maana iliyokusudiwa. Ukosefu wa istilahi ya Kiswahili inayolingana au ni kisawe cha ‘*delicate*’ na ‘*metereological*’ unasabiabisha ukosefu wa ulinganifu wa kimaana.

### 2. Kiingereza:

All weeds should be regularly uprooted and swept away (pg. 43).

### Kiswahili:

Bustani la miche lazima liwe wakati wowote limekotwa taka kwa kufagia kwote na ufagio (uk. 46).

Hoja iliyopotoshwa ni ile inayohusu magugu kung’olewa, haikutajwa katika tafsiri. Kutotafsiri maneno haya ambaya yapo kwenye sentensi kunaleta matatizo katika uwasilishaji wa maana. Mbinu ya kuacha maneno pasi kuyatafsiri kwa kukosa istilahi linganifu katika ML hakufai katika kutafsiri matini ya EM kwa kunapotosha maana iliyokusudiwa na hatimaye kuathiri hata athari zilizokusudiwa.

## Upotoshaji S8

### 1. Kiingereza:

Healthy seedlings are probably available from your own nursery or nearby nursery, however, if the seedlings are not planted properly, the trees never grow well (pg. 54).

### Kiswahili:

Miche iliyo na afya nzuri pengine inapatikana kutoka kwa bustani yako ya miti lakini ikiwa miche hii haipandwi kufuatana na zile kanuni zilizopendekezwa, basi miti hii haitakuwa vizuri (uk. 59).

Katika mfano huu, maneno ‘*haipandwi kufuatana na zile kanuni zilizopendekezwa*’ yamepotosha habari kwani ni maneno ‘*planted properly*’ yalifaa kutafsiriwa. Badala ya kukosa kutafsiri maneno haya kabisa basi mtafsiri angetumia mbinu ya kutafsiri kwa njia ya maelezo. Kufanya vile

kungehifadhi uwasilishaji wa maana na hivyo hadhira lengwa itapata maana na ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira chanzi.

**2. Kiingereza:**

The popular size of a whole is 60 cm (2 feet) diameter by 60 cm (2 feet) in dry area, but a larger hole seems more effective (pg. 54).

**Kiswahili:**

Vipimo vya mashimo ambavyo hutumika sana ni vile vya sentimita 60 (futi mbili) kwa upana na kwa urefu wa sentimita 60 (futi mbili) katika zile sehemu kame, lakini mashimo makubwa ni afadhali (uk. 59).

Hapa maneno ‘hutumika sana’ yanaweza kupotosha ujumbe ulio kwa Kiingereza. Wakati mwingine ni rahisi kufahamu maana ya kifungu cha maneno lakini si rahisi mno kutoa maana hiyo kwa Kiswahili. Kwa mtafsiri anapaswa kuwa mwangalifu sana na kujitahidi kuhifadhi maana za maneno yalitumika katika MC.

**3. Kiingereza:**

If water penetration has reached a certain depth (about one foot from the surface) then it is time to refill the planting holes (pg. 54).

**Kiswahili:**

Ikiwa maji yamepenyeza hadi kina fulani (kama futi moja kutoka sehemu ya juu ya udongo) basi huu ndio wakati wa kupanda miche (uk. 59).

Katika mfano huu, neno ‘*refill*’ si sawa na ‘kupanda miche’ kwa hivyo dhana hii imepotoshwa. Hali hii inaleta ukosefu wa ulinganifu wa maana. Maana ni muhimu sana na lazima kitiliwa maanani wakati wa tafsiri. Maana inapokasa kulingana katika MC na ML basi hadhira ya ML haitapata maana ambayo hadhira ya MC watapata. Lengo la tafsiri ni kuwasilisha ujumbe wa MC kwa ML.

**4. Kiingereza:**

In case it needs some time until planting, the seedlings must be kept in a shade and protected from the wind. Water them if necessary to keep them moist and vigorous (pg. 55).

**Kiswahili:**

Ikiwa miche hii inahitaji kuwekwa kwa muda fulani kabla ya kupandwa, basi inahitaji kuwekwa kwenye uvuli na kuingwa kutokana na upepo. Nyunyizia miche hii maji ikihitajika ili kudumisha unyevunyevu na afya (uk. 60).

Hapa neno ‘*vigorous*’ halikutafsiriwa kwa njia mwafaka, maana yake imepotoshwa. Wakati mwingine mtafsiri anaweza kukumbana na maneno ambayo si rahisi kutoa maana yake kikamilifu kutoka MC had ML. Ugumu wa kutoa maana kamili ndio unaomhitaji mtafsiri kuwa mwangalifu ili awezw kuchunguza maana na vijimaana vinavyojitokeza katika maneno mbalmbali bila kupuuzwa uwezekano wa kukosa kutafsiri visivyo. Kwa hiyo mtafsiri anapokuwa mwangalifu anaweza kujiepusha na upotoshaji wa maana.

**5. Kiingereza:**

Many animals, insects and diseases attack the young seedlings cause certain damage. Among them, wild animals, livestock and termites pose the most serious problems according to the experience and information obtained through various field surveys (pg. 58).

**Kiswahili:**

Wanyama, wadudu na magonjwa mengi hushambulia miti michanga na husababisha uharibifu fulani. Baadhi ya maadui wakubwa wa miti ni wanyama wa pori, mifugo na mchwa. Maadui hawa huleta madhara makubwa sana kutokana na ujuzi wetu na habari zilizopokelewa kutokana na utafiti na habari za nyanjani (uk. 64).

Hapa pana upotoshaji kwani neno ‘*experience*’ lingetokezea kama ‘tajriba’.

**6. Kiingereza:**

For larger scale plantations, fencing all round the area to keep animals out is recommended. Branches of thorny trees, e.g. Acacia can be used as fencing materials, which can be readily available in rural areas (pg. 58).

**Kiswahili:**

Kwa yale mashamba makubwa ya miti, kuweka ua kote ili kuwazuia wanyama ndiyo njia inayopendekezwa. Matawi ya miti yenye miiba, kwa mfano, Acacia na kadhalika yanaweza kutumika kwa minajili ya kufungia shamba kwa vile miti aina hii inapatikana kwa wingi katika sehemu za mashambani (uk. 64).

Katika mfano huu, maneno ‘na kadhalika’ ni ya ziada na neno ‘*fencing*’ halikupewa tafsiri mwafaka.

**7. Kiingereza:**

Drowning termites by pouring water into colonies is suspicious (pg. 59).

**Kiswahili:**

Kumwagia maji mchwa wakiwa kwenye matuta siyo suluhisho la kuua mchwa (uk. 65).

Katika mfano huu neno ‘siyo suluhisho la kuua mchwa’ kama tafsiri ya neno ‘*suspicious*’ linapotosha.

### Upotoshaji S9

#### 1. Kiingereza:

Fruits are very important farm products for earning cash as well as an important source of nutrients in rural areas (pg. 61).

#### Kiswahili:

Matunda ni mazao ya shamba ambayo ni ya muhimu sana kwa vile huletea mkulima pesa na wakati huo huo matunda ni chakula bora cha vitamin (uk. 67).

Katika mfano huu, neno ‘*nutrients*’ limetafsiriwa kama ‘vitamin’ ambalo si maana yake.

#### 2. Kiingereza:

Ngowe, good quality, most popular for export, large long fruit, deep yellow (pg. 61).

#### Kiswahili:

Hii ni aina nzuri ya maembe, maarufu katika masoko ya ng`ambo, huzaa embe refu la rangi ya samawati (uk. 67).

Hapa neno ‘*yellow*’ limetafsiriwa kama ‘samawati’ ambalo linapotosha, tafsiri yake ni ‘manjano’.

#### 3. Kiingereza:

Prevent excessive growth of vegetation beneath the trees (pg. 61).

#### Kiswahili:

Hakikisha kwekwe zote zimeng`olewa na mwembe unakua bila mashindano na kwekwe (uk. 68).

Hapa neno ‘*vegetation*’ limetafsiriwa kama kwekwe na inawezekana kuwa tafsiri yake inaweza kuwa mimea yoyote.

#### 4. Kiingereza:

Mango scale, small, flat, whitish, circular scales, which excrete honey dew and sooty mould (pg. 62).

#### Kiswahili:

Magamba ya miembe, haya huwa ni magamba madogo, laini, meupe na ambayo hutoa kinyesi cheupe (uk. 68).

Hapa maneno ‘*excrete honey dew*’ yametafsiriwa kama ‘kinyesi cheupe’ ambayo inapotosha.

**5. Kiingereza:**

Deep well drained soil capable of retaining moisture (pg. 62).

**Kiswahili:**

Udongo tifutifu unaopitisha maji na ambao haukauki haraka (uk. 68).

Hapa maneno ‘*capable of retaining moisture*’ yametafsiriwa kama ‘ambao haukauki haraka’ na hivi ni kupotosha kwani uwezo wake wa kuweka unyevunyevu ndio unaelezwa.

**6. Kiingereza:**

Subsoil should be used to make a basin around the trees, after planting to retain water (pg. 63).

**Kiswahili:**

Udongo wa chini utumiwe kuzunguka mti ili kuhifadhi maji baada ya kupanda mti (uk. 70).

Hapa neno ‘*subsoil*’ limetafsiriwa kama ‘udongo wa chini’, pengine maelezo ya sehemu ya udongo huu yangefaa.

**7. Kiingereza:**

Pruning; all side shoots growing from the tree trunk below the main branches and on the root-stocks should be rubbed off. Remove dead and broken branches (pg. 63).

**Kiswahili:**

Kupunguza matawi; michipuko yote inayokua kwenye pande za mashina kwenda chini ichengwe. Mizizi pia inayochipuka kwenye mashina ya michungwa pia iondolewe (uk. 70).

Hapa neno ‘*root stock*’ imetafsiriwa kama ‘pande za mashina’ ambao ni upotoshaji.

**8. Kiingereza:**

Trace elements, deficiencies of one or more minor elements may occur in citrus orchards (pg. 63).

**Kiswahili:**

Upungufu wa madini, upungufu wa mojawapo au madini mengi unaweza ukakosekana katika bustani la michungwa (uk. 70).

Hapa maneno ‘*trace elements*’ na ‘*minor*’ limetafsiriwa kwa njia inayopotosha, tofauti na kuwa haya ni madini ambayo hutokezea kwa udogo, tena, neno ‘ukakosekana’ limetumiwa katika sentensi moja na neno ‘upungufu’, hii inamaanisha kuwa hakuna upungufu.

**9. Kiingereza:**

Citrus aphid; masses of small black or brown, soft bodied insects that concentrate on tender young shoots causing growth distortion (pg. 64).

**Kiswahili:**

Wadudu wengi wadogo ambao huwa weusi au wenye miili nyororo hushambulia michipuko ya miti na hivyo miti kama hii hukua pole pole (uk. 70).

Hapa maneno '*brown*' na '*concentrate*' hayajatafsiriwa kwa njia inayoleta habari zilizo kwenye MC kwani yanastahili kuwa 'hudhurungi' na 'hukusanyika'.

**Upotoshaji S10****1. Kiingereza:**

Root stocks are chosen on the basis of their adaptability to various soils and soil conditions, compatibility with different scions (pg. 73).

**Kiswahili:**

Mashina asili huchaguliwa kutegemea uwezo wao wa kustahimili udongo wa aina fulani, magonjwa yatokayo udongoni, kupatana na mashina tofuati ya kupandikiza (uk. 82).

Hapa maneno '*soil conditions*' yametafsiriwa kama 'magonjwa yatokayo udongoni' ambayo yanapotosha, pengine, 'hali za udongo' ingestahili.

**2. Kiingereza:**

Use the knife to open the budding slit (pg. 74).

**Kiswahili:**

Tumia kisu ili kuondoa chipukizi (uk. 83).

Katika mfano huu, maneno '*open the budding slit*' yakitafsiriwa kama 'kuondoa chipukizi' ni kupotosha maana ingekuwa '*kuchanja mahali pa kuchomoza*'.

**3. Kiingereza:**

Wax over the tape (if grafting wax is available) to prevent drying (pg. 74).

**Kiswahili:**

Weka gundi juu ya utepe (ikiwa gundi la kupandikiza halipatikani) ili kuzuia kukauka (uk. 83).

Hapa maneno '*if grafting wax is available*' yakitafsiriwa kama 'ikiwa gundi la kupandikiza halipatikani' ni kinyume cha maana yake na hivyo inapotosha.

## Upotoshaji S11

### 1. Kiingereza:

This high population pressure has resulted in excision of forests and pushing them further away from the farmers and population centres (pg. 76).

### Kiswahili:

Idadi kubwa ya watu inayoongezeka mwaka baada ya mwaka imeangamiza misitu iliyobakia sasa iko mbali na wakulima na makao ya watu (uk. 85).

Katika mfano huu, maneno ‘*population pressure*’ na ‘*population centres*’ hayajapewa tafsiri mwafaka.

### 2. Kiingereza:

The selection of tree species depends on the purpose, intended, end–use and the services that the trees offer to the farmers as well as crops to be cultivated and also land availability (pg. 76).

### Kiswahili:

Miti hii ni lazima itazamwe kutokana na manufaa itakayotea mkulima, kwa mfano miti hii itatumiwa kwa shughuli gani na huduma miti hii itamtolea mkulima na mimea mingine ya vyakula shambani (uk. 85).

Hapa maneno ‘kwa mfano miti hii itatumiwa kwa shughuli’ ni ya ziada.

### 3. Kiingereza:

In most of the very dry areas, soil becomes saline due to capillarity action. Some species, e.g. ‘*Kochia*’ can take some of these soils rendering the soil to be less alkaline and then the soil becomes more productive (pg. 76).

### Kiswahili:

Katika sehemu nyingi kame udongo huwa na chumvi nyingi. Jamii ya miti kwa mfano, ‘*kochia*’ hutumiwa kwa minajili ya kupunguza chumvi kwenye udongo (uk. 85).

Hapa maneno ‘*capillarity action*’ hayakutafsiriwa. Kutotafsiri kifungu hiki kunamfanya msomaji wa ML kukosa kupata kwa ukamilifu ujumbe na maana inayopatikana katika MC. Ni vigumu kuelewa ikiwa kutotafsiri huku kulifanywa kwa makosa au ilikuwa ni kwa sababu ya kukosa istilahi linganifu.

### 4. Kiingereza:

Borderline trees, trees and shrubs are planted as property markers to delineate individual farm fields. They do not occupy too much space, nor do they shade large areas (pg. 81).

**Kiswahili:**

Miti hupandwa mipakani ya shamba ili kuonyesha mipaka ya mali ya mkulima mmoja na mwingine. Miti hii ya kuonyesha mipaka huhitaji nafasi kubwa ya kupanda na uvuli wa miti hii huwa si kubwa (uk. 90).

Hapa neno ‘*delineate*’ halikutafsiriwa. Pana haja ya tafsiri mwafaka.

**5. Kiingereza:**

In dry areas where it is difficult to re-establish trees once they have been cleared, this adaptation is a particularly valuable characteristic (pg. 82).

**Kiswahili:**

Katika sehemu kame, miti aina hii hupendekezwa kwa vile ni vigumu kupanda miche ya miti baada ya kukata miti hii (uk. 91).

Hapa hoja inayodokezwa na ‘*this adaptation is a particularly valuable characteristic*’ haikujitokeza katika tafsiri hii badala yake ni ‘miti aina hii’, ndiyo yametumika.

**Upotoshaji S12****1. Kiingereza:**

Overcut of trees (pg. 85).

**Kiswahili:**

Kukata miti ovyo ovyo (uk. 95).

Hapa neno ovyo ovyo halikustahili kutumika kutafsiri ‘overcut’ kwani maana inayozuliwa hapa ni kule kuzidi kiasi.

**2. Kiingereza:**

Some soil conservation measures are often combined with this system (pg. 86).

**Kiswahili:**

Uhifadhi wa mmomonyoko wa udongo hutekelezwa katika kilimo hiki (uk. 96).

Hapa kinachostahili kuelezwa ni kuwa njia nyingine ya uhifadhi wa mazingira hujumuishwa na mtindo huu.

**3. Kiingereza:**

Staggered wind breaks can also provide the most effective protection around towns and villages, where they are laid out in a pattern of overlapping blocks (pg. 92).

**Kiswahili:**

Vizuizi vya upepo vilivyo kwenye safu fupi fupi hutoa kinga bora zaidi hasa katika mijini na vijijini ambako vizuizi vya mawe hujengwa huku vikipatana (uk. 104).

Lengo la tafsiri ni kuwawezesha hadhira lengwa kusoma na kuelewa taarifa zinazopatikana katika MC. Lengo la tafsiri ya kazi hii ya EM ni kuhasisha watu ili kuweza kuhifadhi mazingira. Kwa hivyo, wakati wa kutafsiri, ni bora mtafsiri kuepuka tafsiri zinazoweza kuleta utata wa maana na vile vile tafsiri sisisi. Hii ni kwa sababu utata wa maana unasababisha upungufu wa mawasiliano na hivyo lengo kuu la kazi ya EM haitaafikiwa.

**4.4 Upotezaji na Upotoshaji wa Habari katika Mchakato wa Tafsiri**

Upotezaji ndiyo unaotokea mara chache sana (16) katika sura zote kumi na mbili za kazi iliyochambuliwa kulingana na Jedwali 4.1. Hiki ndicho kipengele ambacho kina idadi kubwa ya kutotokea ikiwa na sura nane ambazo hazina upotezaji na sura nne ambazo zina upotezaji. Hi ni takriban robo tu ya jumla ya ushawishi kutokana na vipengele vyote. Matokeo haya yanahusiana vyema na swali la tatu la utafiti ambao ulikuwa; *'je kumetokea kiasi gani cha upotezaji na upotoshaji wa habari katika ML kutoka katika MC?* Haya yanamaanisha kuwa kiasi kikubwa cha habari katika MC kiliweza kupitishwa hadi katika ML. Hali hii ni nzuri kwani imeendeleza kusudi la tafsiri hii ambalo lilikuwa utoaji wa ushauri kuhusu mbinu za utunzaji miti katika misitu ya jamii. Kiasi cha habari zinazotosha kikifikia ML kitawafaidi hadhira lengwa ilivyokusudiwa na mwandishi wa MC. Inamaanisha kuwa wasomaji wa MC na ML wa sura hizo walipata ujumbe uliokusudiwa na athari zilizotarajiwa kupatikana kwa hadhira zote mbili ifaavyo. Ni vigumu kutafsiri matini za EM kutoka Kiingereza hadi Kiswahili hasa pale ambapo dhana zinazopatikana katika Kiingereza hazipo katika Kiswahili. Hali hii ndiyo hupelekea mtafsiri kukosa kutafsiri maneno au kifungu cha maneno na hatimaye kupoteza maana iliyokusudiwa katika MC. Upotezaji wa maana huleta matatizo katika uwasilishaji wa maana kwani ile maana imepotezwa kabisa.

Upotoshaji, mbali na kusababishwa na vipengele hivyo vingine, umeonekana mara arobanne na nane (48). Hi imeonyeshwa katika Jedwali 4.1, sura za 1, 8 na 9 zikiwa nayo kwa wingi zaidi. Kauli hii inajibu swali la tatu la utafiti huu, *'je kumetokea upotezaji na upotoshaji wa habari kwa kiasi*

*gani katika ML kutoka katika MC?* Katika utafiti huu, inabainika kuwa upotoshaji ukilinganishwa na upotezaji inaonekana kuwa una ushawishi mkuu kuliko upotezaji.

**Jedwali 4.1: Muhtasari wa kutokea kwa vipengele vya upotezaji na upotoshaji**

Sura (S)	S1	S2	S3	S4	S5	S6	S7	S8	S9	S10	S11	S12	Jumla
Upotezaji	0	0	0	9	1	5	0	0	0	0	1	0	16
Upotoshaji	8	3	0	7	2	0	0	8	9	3	5	3	48
Jumla	8	3	0	16	3	5	0	8	9	3	6	3	64

## 4.5 Masuala Ibuka

Utafiti huu umeonyesha kuwa, pana masuala ambayo yameibuka katika uchambuzi wa tafsiri husika. Masuala ibuka yametokea kwa aina mbili; istilahi za elimumisitu na msamiati ambao haukutafsiriwa. Haya yamewasilishwa katika Jedwali 4.2. Kwa sababu ya kutokuwa na uamilifu, baadhi ya maneno na kauli nyingine haikutafsiriwa miongoni mwa vipengele husika. Maneno na virai takriban 81 havikutasiriwa katika sura zote 12. Changamoto hii imetokea katika kila sura kwa viwango mbali mbali, sura ya 8 na 9 zikiwa na mengi zaidi na sura ya 3 ikiwa na kiwango kidogo mno. Suala jingine lilioibuka ni kuwa baadhi ya maneno na dhana zimepewa kinyume badala ya tafsiri. Hali hii huenda ikawa imesababishwa na upungufu wa msamiati na istilahi za kitaaluma na kushawishi kiasi cha habari kilichopitishwa kutoka MC hadi ML.

### 4.5.1 Msamiati na Istilahi za Elimumisitu

Katika sehemu hii tumetoa orodha ya msamiati na istilahi za elimumisitu (EM) ambazo zimejitokeza katika tafsiri iliyotafitiwa. Msamiati na istilahi hizi zimezua changamoto katika tafsiri hiyo. Pasipokuwa na matumizi ya machapisho maalum yahasuyo ukopaji, utohozi na ubunaji wa istilahi mwafaka za kutafsiria dhana za kimazingira, hapawezi kuwa na uamilifu ambao unaweza kuleta ushawishi wa kiasi cha habari zinazopitishwa katika tafsiri. Katika utafiti huu, sura moja tu kati ya sura kumi na mbili ndiyo imebainika kutokuwa na changamoto za EM. Sura za 2, 10 na 11 ndizo zinachangia kipengele hiki cha istilahi za EM kwa kiasi kikubwa, kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 4.2. Matokeo haya yanaonyesha kuwa kutokuwepo kwa istilahi za EM katika ML huenda ukasababisha ushawishi wa kiasi cha habari unaoletwa na vipengele kama uzidishaji na upotoshaji.

**Jedwali 4.2: Muhtasari wa kutokea kwa istilahi za elimumisitu na msamiati ambao haukutaafsiriwa**

Sura (S)	S1	S2	S3	S4	S5	S6	S7	S8	S9	S10	S11	S12	Jumla
<b>EM</b>	7	8	4	4	4	4	0	2	6	7	10	6	<b>62</b>
<b>Msamiati</b>	3	8	1	10	5	2	2	12	12	3	8	7	<b>81</b>
<b>Jumla</b>	10	16	5	14	9	6	2	14	18	10	18	13	<b>143</b>

Sehemu zote katika kazi iliyochambuliwa zilikosa msamiati mwafaka na hii ilizua hali hii ya kupotosha habari fulani. Hali hii imetufanya tuamini kuwa si kiasi au ukweli wote wa habari ndio umefika katika ML kwani waandishi kusudi lao ilikuwa kupitisha ujumbe fulani maalum. Uwepo wa EM katika MC ilhali baadhi haijafika katika ML ni hali ambayo inadokezea mambo matatu; kwanza, kuwa tafsiri hii ni ya kiteknolojia, pili ni kuwa mtafsiri hana ujuzi wa istilahi hizi katika LL na tatu ni kuwa kusudi la kazi ilikuwa kupitisha kiasi kinachotosha hadhira lengwa kupata na kuelewa ujuzi wa mbinu za utunzaji miti katika misitu ya jamii. Upekee wa taaluma hii umesababisha matumizi ya msamiati ambao umezua changamoto kupata tafsiri yake. Mifano ya istilahi za EM imetolewa kwenye orodha ifuatayo ya maneno na tasiri zake amilifu.

**Kiingereza****Kiswahili****S1**

By-products:

Mazao ziada

Neem:

Mwarubaini

Soil erosion:

mmomonyoko wa udongo

Fix nitrogen:

ambisha naitrojeni

Soil structure:

muundo udongo

Green manure:

mbolea ya kijani kibichi

Water catchment:

eneo la chanzo cha mto

Transplanting:

kupandikiza

**S2**

Ornamental trees:

miti pambifu

Contour lines:

mistari ya kontua

Fodder trees:

lishe ya mifugo kutoka sehemu za miti kama vile matawi

Nitrogen fixing:

yenye kuambisha naitrojeni

Coppice:

chipua

Indigenous:

ya kienyeji, -enyeji asilia au asilia

Semi-arid areas:

eneo la nusu-jangwa

Mulch:

kitandazio

**S3**

Mother tree:

mti mama au mtoa mbegu

Viable seed:

mbegu ya kukimu

Genetic superiority:

ustadi wa maumbile

Interbreeding:

kuingiliana

**S4**

Organic matter:	vitu vyenye uhai
Pricking process:	shughuli ya kupandikiza
Climatic disaster:	baa la tabia nchi
Biotic factors:	mambo ya viumbe

**S5**

Defoliators:	kinakisi majani
Photosynthetic:	usanidimwanga
Nocturnal:	ya usiku
Galls:	kidutu

**S6**

Species:	spishi
Sowing:	upandaji
Germination:	uotaji
Root pruning:	kupogoa mizizi

**S8**

Evaporation:	mvukizo
Mulching:	kutandazia

**S9**

Agroforestry:	kilimo mseto
Ecology:	ikolojia
pH:	kipimo pH
Propagation:	usambazaji
Budding:	kuchomoza
Grafting:	kusanisha

**S10**

Grafting:	kupandikiza
Scion:	kitoa vikonyo shina
Budding:	kuchomoza
Bud union:	kuunganisha kichomoza
Clones:	kloni
Defoliation:	nakisimajani
Diameter:	kipenyo

**S11**

Symbiotically:	ufaano au kwa njia ya kufaana
Shifting cultivation:	kilimo uhamishaji
Capillarity action:	mvutano kapilari

Water run-off:	maji mtiririko
Green manure:	mbolea ya kijani kibichi
Lopping off:	pogoa
Contour strips:	kipande cha kontua
Natural regeneration:	uota upya
Silvi-pastoralism:	ukuzaji miti na ufugaji
Pollarded:	kukata kilele cha mti

## **S12**

Rehabilitation:	kilichotengenezwa upya
Infiltration:	mpenyo
Soil fertility:	rutuba ya udongo
Soil structure:	muundo udongo
Contour strip:	kipande cha kontua
Terraces:	matungazi

## **4.6 Hitimisho**

Katika sura hii uchambuzi wetu uligundua ushawishi wa kiasi cha habari uliosababishwa na vipengele amilifu vya tafsiri kama vile upotezaji na upotoshaji. Pamoja na hayo, tuligundua ushawishi wa kiasi cha habari uliosababishwa na masuala ibuka katika kazi hii. Masuala hayo ibuka yanajumuisha istilahi za EM na msamiati ambao haukutafsiriwa. Ujumuishaji wa vipengele hivi amilifu vinaweza kufanikisha tafsiri yenye kusudi au malengo mahususi.

## SURA YA TANO

### MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

#### 5.1 Utangulizi

Lugha zikitafsiriwa hapana budi kutokea ubanaji, uzidishaji, upotezaji na upotoshaji, kama ilivyotokea katika utafiti huu. Pamoja na haya, msamiati na istilahi za EM na hoja nyingine pia huibuka katika tafsiri za kitaaluma. Katika sura hii tumeangazia matokeo, hitimisho na mapendekezo yanayotokana na uchambuzi wa tafsiri ya Kiswahili ya nakala ya Kiingereza ‘*Social Forestry Techniques*’.

#### 5.2 Muhtasari

1. Kuna baadhi ya maneno au sentensi ambazo zilibanwa, kuzidishwa, kupotezwa na nyingine kupotoshwa na kwa hivyo, wapokezi wa ML wakakosa kiasi cha habari kilochokusudiwa.
2. Kuna baadhi ya istilahi za EM ambazo zilikosekana na hivyo kushawishi kiasi cha habari kilichokusudiwa.
3. Pana baadhi ya maneno ambayo hayatafsiriki na mengine yangeweza kutafsiriwa lakini hayakutafsiriwa, na hivyo kushawishi kiasi cha habari kilichokusudiwa.

#### 5.3 Hitimisho

Ubanaji na uzidishaji umetokea kwa kiasi kikubwa katika kazi hii kwa kiwango kinachozidi vipengele hivyo vingine. Hii ni kwa sababu kusudi la tafsiri haisisitizi ulinganifu wa MC na ML bali linalenga kukidhi haja fulani. Haya yanalingana na maoni ya Ahmed ambaye alisema kuwa katika tafsiri za Kiarabu hadi Kiingereza ubanaji na uzidishaji unaweza kutokea ili kukidhi haja fulani katika mahitaji ya ML. Masuala ya msamiati na istilahi ambayo haikutafsiriwa pia yalizuka.

Swali la kwanza la utafiti lilikuwa: *je, kuna habari ambazo zimebanwa katika matini lengwa kutoka katika matini chanzi?* Kutokana na uchambuzi wa makala yote mawili, MC na ML, ni wazi kuwa ubanaji umetokea kwa kiwango kinachoshawishi kiasi cha habari inayohawilishwa ikilinganishwa na vipengele vingine. Sababu za ubanaji huu zinaweza kuwa mbili, kwanza ni ukosefu wa ujuzi wa msamiati na istilahi za EM na, pili ni kusudi la tafsiri hiyo ambayo ilinuiwa kutoa maelezo ya habari

za upandaji na utunzaji wa miti. Kitendo cha kuipa ML umuhimu zaidi ya MC kimependekezwa na Vermeer aliyeasisi Nadharia ya ‘Skopos’.

Swali la pili la utafiti lilikuwa: *je, pana kiasi gani cha habari ambazo zimezidishwa katika ML ikilinganishwa na MC?* Data zinazotokana na uchambuzi wa MC na ML zinadokeza kwamba uzidishaji ni kipengele kilichotokea kwa kiwango cha juu ikilinganishwa na vipengele vingine. Kwa kawaida pana baadhi ya lugha ambayo hutumia maneno mengi kuliko nyingine, kwa mfano, LL (Kiswahili) hapa ikiwa ina idadi kubwa ya maneno yanayotumiwa kuelezea dhana mahsusi kutoka LC (Kiingereza). Upungufu wa msamiati mwafaka kutokana na ukosefu wa kiwango mwafaka cha ujuzi au lugha yenyewe kileksika zinaweza kuchangia matumizi ya maneno mengi zaidi. Pamoja na haya, kusudi la tafsiri linaweza kuathiri mchakato wa tafsiri kutokana na nadharia iliypendekezwa na Vermeer, Reiss, Nord na Holz-Mantari.

Swali la tatu la utafiti lilikuwa: *je, kumetokea upotezaji na upotoshaji wa habari katika matini lengwa kutoka katika matini chanzi?* Swali hili linazungumzia vipengele viwili; upotezaji na upotoshaji. Upotezaji umetokea kwa kiwango kidogo zaidi. Watafsiri wa nakala; ‘*Social Forestry Techniques*’ wameonekana kushughulikia data karibu zote, jambo ambalo linadhihirisha fikra na maono maridhawa. Wataalam hawa wanastahili pongezi kwani tafsiri hii ilifanywa katika mwaka wa 1991, takriban miongo mitatu iliyopita, ambapo hapakuwa na kamusi mbalimbali zilizoko sasa pamoja na zana kama vile mtandao. Nyakati hizo machapisho ya msamiati na istilahi za EM hayakushamiri kama pengine ilivyo sasa, hali ambayo ingeweza kuchangia upotezaji. Upotoshaji nao umetokea kwa kiwango cha wastani katika tafsiri iliyochambuliwa ukilinganishwa na vipengele vingine. Upotoshaji umeonekana kusababishwa na kuwepo kwa vipengele vitatu vya kwanza; ubanaji, uzidishaji na upotezaji. Vipengele hivi vinne vinategemeana na kukamilishana. Hivi ni kusema kuwa kimoja kinaweza kushawishi kingine. Watafsiri hawana budi basi kusawazisha vipengele hivi vyote vinne. Upotoshaji umeonekana pia kusababishwa na ukosefu wa msamiati na istilahi za EM katika ML, hali ambayo hufanya watafsiri kutumia maelezo ambayo yanalenga kando ya maana.

Msamiati na istilahi za EM zimetumika katika baadhi ya sura za MC, ‘*Social Forestry Techniques*’, na kiwango fulani kimehamishwa na mara nyingine kukosa kufanya hivyo katika ML. Ujuzi wa EM

katika Kiswahili ukikosekana ushawishi wa kiasi cha habari unatokea kwa kiwango hafifu. Kwa sababu hii, imetubidi tuchunguze hali hii kwa makini na kufanyia utafiti zaidi. Tafsiri za kitaaluma kama hii ya kimazingira haiwezi kuimarika bila ujuzi wa msamiati na istilahi za EM.

#### 5.4 Mapendekezo

Vipengele vyote katika kazi hii vinaweza kuimarishwa katika kazi iliyochunguzwa kwa njia zitakazopendekezwa hapa. Mapendekezo haya yakitumiwa yatafanikisha kutekelezwa kwa kusudi la kazi iliyochunguzwa hapa ambayo ni wazi kuwa ni kupitisha habari zihusuzo upandaji na utunzaji wa miti kwa njia sahihi.

1. **Ubanaji** unaweza kupunguzwa kwa kufanya utafiti unaolenga kupata istilahi mwafaka wa kusaidia mchakato wa tafsiri.
2. Matini lengwa inaweza ikawa na maneno zaidi ya matini chanzi hasa ikiwa MC ni Kiingereza na ML ni Kiswahili. Hali hii ya **uzidishaji** inaweza kupunguzwa kwa kutumia msamiati wa kutosha na kiasi cha habari ambayo inahitajika tu.
3. Pana haja ya kuwa makini zaidi katika kutafsiri habari za MC, ingawa kusudi la kazi ni kupitisha tu ujumbe wa kutosha isionekane kama hoja nyingine **imepotea**. Vipengele hivi vitatu; ubanaji, uzidishaji na upotezaji zinachangia upotoshaji, ambao unatokea ikiwa maana inayolengwa na MC imepotezwa na kuelezwa kwa kuelekea kwa maana tofauti inapofika katika MC.
4. Hatuna budi kuingiza msamiati na istilahi za EM katika kazi za aina hii katika juhudi za kupunguza **upotoshaji**.
5. Utafiti zaidi ufanywe unaolenga kuimarisha EM na kitabu maalum kichapishwe cha 'Istilahi za EM nchini Kenya'.
6. Maneno ambayo hayakutafsiriwa yatafsiriwe ili kupata tafsiri ya maneno, virai na sentensi kamilifu.
7. Kitabu cha '*Social Forestry Techniques*' kinafaa kitaaluma, kinastahili kuwa na toleo la pili ambamo vipengele vilivyo na upungufu vinaweza kuimarishwa.
8. Kamusi mahususi inayojumuisha ukopaji, utohozi na ubunaji wa maneno inahitajika katika taaluma hii.

9. Maeneo ya mtandao kama vile ‘Google’ ambayo huenda yakatoa tafsiri tofauti kabisa ya visawe vinavyohitajika, yanastahili kutumika kwa uangalifu.

### **5.5 Sehemu za Kufanyiwa Utafiti Zaidi**

Upeo na mipaka ya kazi hii ulikuwa kuchunguza maswala manne; ubanaji, uzidishaji, upotezaji na upotoshaji. Uchunguzi huu ulihusu tu kuchunguza tafsiri ‘*Mbinu za Utunzaji Miti Katika Misitu ya Jamii*’, nakala ambayo ina sura kumi na mbili. Bado pana machapisho mengine yanayohimiza msamiati na istilahi za EM ambayo yanaweza kufanyiwa tafsiri na utafiti. Nchi kama Tanzania ina machapisho yahasuyo EM katika lugha ya Kiswahili, maandishi kama hayo yanahitajika nchini Kenya. Pana haja ya utafiti unaolenga kuchapisha kitabu maalum cha msamiati na Istilahi za EM cha nchi ya Kenya.

## MAREJELEO

- Abranyi, H. (2016). Translation Environment Tools. In: I. Horvath (Ed.). *Modern Translator and Interpreter* (pp. 167-181). Budapest: Eotvos University Press.
- Ahmed, S. A. (2016). *Loss and Gain in Translating Prophet Mohammed's Farewell Oration: A Comparison of Three Variant Translations*. An-Najah National University: Unpublished Masters' Thesis.
- Aissi, L. (1987). *An analytical study of the process of translation*. The University of Salford: Unpublished thesis.
- Ali, C. (1981). *The problem of translating from English into Kiswahili as exemplified by VOK news items*. University of Nairobi: MA thesis, Unpublished.
- Buliba, A., Gwachi, M., & Matinde, R. (2014). *Misingi ya Nadharia za Utafiti*. Mwanza. Serengeti Educational Publishers Ltd.
- Carmen, V. (2014). Introduction: Translating Environmental Humanities. *Ecozon*, 5(1), 1-10.
- Catford, J. (1965). *A linguistic theory on translation*. London: Oxford University Press.
- GoK (Government of Kenya). (2010). *The Constitution of Kenya 2010*. Nairobi. Government Printers.
- Holz-Manttari, J. (1984). *Translatory acting: theory and method*. Helsinki: Suomalainen Tiedeakatemia.
- Jackson, S.T, Garfin, G.M, & Anquist, C.A. (2017). Toward an effective practice of translational ecology. *Frontiers in the Ecology and Environment*, 15(10), 540.
- Jakobson, R. (1959). "On Linguistic Aspect of Translation". In: R. A. Brower (Ed.), *On Translation* (pp. 232-239). Cambridge: Harvard University Press.
- Jilala, H. (2014). *Athari za Kitamaduni katika Tafsiri. Mifano kutoka Matini za Kitalii katika Makumbusho za Tanzania*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Tasnifu ya Uzamifu haijachapishwa.
- Jilala, H. (2017). Matatizo ya tafsiri katika matini za kitalii nchini Tanzania. *UDSM Journal*, 27-47.
- Jilala, H. (2017). Tathmini ya hatua za tafsiri kama nyenzo ya ufanisi wa mawasiliano. *UDSM Journal*, 79, 118-142.
- Kamau, G. (2008). *Meaning: Translation in the Kiswahili Translation of George Orwell's Animal Farm*. Kenyatta University: MA thesis, Unpublished.

- Kenya/Japan Social Forestry Training Project. (1991). *Mbinu za Utunzaji Miti katika Misitu ya Jamii* (Sehemu ya kwanza). Nairobi.
- Kenya/Japan Social Forestry Training Project. (1991). *Social Forestry Techniques* (Part One). Nairobi.
- Kihore, Y. (2005). Uzingatifu wa sarufi katika Tafsiri. *Swahili Forum*, 109-120.
- Levy, J. (1967). *Translation as a decision process*. London and New York: Routledge.
- Merkel, M. (2001). Comparing source and target texts in a translation corpus. *NODALIDA conference*. Linköping University.
- Mghanga, M. (2011). *Kanuni Tatu za Misitu Zilizorahisishwa*. Forest Action Network. Nairobi. Apple Communications and Supplies.
- Muñoz, I.D. (2012). Analysing common mistakes in translation of tourist texts (Spanish, English and German). *Onomâzein*, 26 (2) 335-349.
- Mutie, E. K. (1997). *Sanaa katika Tafsiri: Matatizo na Athari zake*. Chuo Kikuu cha Nairobi: Tasnifu ya Uzamili, haijachapishwa.
- Muzaffar, S. & Behera, P. (2017). The concepts of equivalence, gain and loss (divergence) in English - Urdu web-based machine translation platforms. *ReasearchGate*, 1-10.
- Mwangi, D. W. (2016). Changamoto na manufaa ya kutafsiri Kiswahili katika miktadha ya wingilugha Narok Kaskazini. Chuo Kikuu cha Nairobi: Tasnifu ya Uzamili, haijachapishwa.
- Newmark, P. (1988). *A textbook of translation*. New York: Prentice Hall.
- Njenga, G. (2014). *Changamoto za kutafsiri matini za kisheria: Tathmini ya katiba ya Kenya 2010*. Chuo Kikuu cha Nairobi: Tasnifu ya Uzamili, haijachapishwa.
- Neuman, W. (1997). *Social Research Methods: Qualitative and Quantitative Approaches*. Boston: Allyn and Bacon.
- Nida, E.A. and Taber, C. (1969). *The Theory and Practice of Translation*. The Netherlands, UBS.
- Nord, C. (1991). *Skopos, Loyalty and Translation Conventions*. Amsterdam: Rodopi.
- Nord, C. (1997). *Text Analysis in Translation: Theory, Methodology and Didactic Application of a Model for Translation Oriented Text Analysis*. Amsterdam: Rodopi.
- Nord, C. (2005). *Text Analysis in Translation: Theory, Methodology and Didactic Application of a Model of Translation-oriented Text analysis* (Second ed.). Amsterdam - New York: Editions Rodopi.

- Nshubemuki, L., Mwansoko, H.J.M., & Mugasha, A.G. (1999). *Istilahi za Elimumisitu: Kiingerza - Kiswahili*. Morogoro. FORST/TAFORI.
- Patton, M. (2002). *Qualitative Research and Evaluation Methods*. London: Sage Publications Ltd.
- Pobocikova, P. (2012). *Changes in a source text during repeated translation*. Masaryk University.
- Pym, A. (1990). "A Definition of Translational Competence, Applied to the Teaching of Translation". Paper presented to the 12<sup>th</sup> World Congress of the FIT, Belgrade.
- Rahmatillah, K. (2013). Translation errors in the process of translation. *Journal of English and Education*, 7(1) 14-24.
- Reiss, K & Vermeer, H. (1984). *Groundwork for a General Theory of Translation*. Tubingen: Niemeyer.
- Reiss, K. (1984). *Towards a general theory of translation action: skopos theory explained*. Taylor and Francis.
- Reiss, K. (2000). "Type, Kind and Individuality of text: Decision making in Translation" . In: L. Venuti (Ed.). *The Translation Studies Reader* (pp. 160-171). London: Routledge.
- Vermeer, H. (1978). Skopos Theory. In M. Baker (Ed.). *Routledge Encyclopedia of Translation Studies* (pp. 219-237). London: Routledge.
- Vermeer, H. (1989a). *Scopos and commission in translational action*. London: Routledge.
- Viberg, Å. (2016). "What happens in translation? A comparison of original and translated texts containing verbs meaning SIT, STAND and LIE in the English-Swedish Parallel Corpus (ESPC)". *15*(3), 102-148.
- Watkiss, P., Pye, S., Hendriksen, G., Maclean, A. Bonjean, M., Shagude, Y., Sheikh, M & Khamis, Z. (2012). *Athari za Mabadiliko ya Tabianchi kwa Uchumi wa Zanzibar: Muhtasari wa Ripoti ya Misisitu*. Zanzibar. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## VIAMBATISHO

### Kiambatisho 1: Nakala zilizotafitiwa

